ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.

48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.

68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

BARAZA LA SABA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 24 Machi, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza karibuni sana katika mkutano wetu wa 19 ambao unaanza leo tarehe 24/03/2010 kama vile ambavyo tuliupanga. Kutakuwa na taarifa mbili moja inayohusu shughuli tulizofanya katika mkutano uliopita na ya pili ni kuhusu kuombwa radhi Baraza. Kwa hivyo, naanza na taarifa ya kwanza inayosema kwamba Waheshimiwa Wajumbe katika mkutano wa 18 wa Baraza la Saba la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 20 Januari, 2010 Baraza lilipitisha miswada miwili ya sheria kama ifuatavyo:

1) Mswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. ya mwaka 1997.
2) Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 91, kifungu kidogo cha 3 cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2009 naomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waheshimiwa Wajumbe taarifa ya pili ni kuhusu kuombwa radhi Baraza.

Waheshimiwa Wajumbe katika Baraza la Saba la Mkutano wa 18 wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar uliofanyika tarehe 26 Januari, 2010 Baraza la Wawakilishi lilipokea taarifa iliyotangazwa na Kituo cha Redio cha Zenji FM kwamba timu ya mpira ya miguu ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi iliwahi kuvaa jezi za Kampuni ya *TBL* ambayo hutengeneza pombe, kwa mantiki hiyo timu yetu ilitangaza pombe kinyume na Sera ya Serikali juu ya kupiga marufuku matangazo ya pombe katika michezo hapa Zanzibar.

Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa kauli hiyo ya Zenji FM haikuwa sahihi na kwa kuzingatia uzito wa kauli hiyo mbele ya umma dhidi ya chombo cha wananchi kinachotarajiwa kuwa mfano wa utekelezaji wa Sera za Serikali, Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Ali Mzee Ali aliyekuwa akiendesha kikao cha Baraza siku hiyo aliutaka uongozi wa Zenji FM kuliomba radhi Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, alikuwa akitilia mkazo kauli ya Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ambaye alitangulia kusema kwamba Wizara yake imeitaka Zenji FM kuliomba radhi Baraza kwa kulidhalilisha au wathibitishe kauli yao kwa ushahidi. Pia Mhe. Mwenyekiti, aliiagiza Afisi ya Baraza la Wawakilishi kuwaarifu Zenji FM kuhusu agizo hilo.

Waheshimiwa Wajumbe Afisi ya Baraza la Wawakilishi ilitekeleza agizo hilo la Baraza kwa kuwaandikia barua uongozi wa Kituo cha Redio cha Zenji FM yenye kumbukumbu Nam. BLW/B90/153/27 ya tarehe 13 Februari, 2010, barua hiyo iliutaka uongozi wa Zenji FM kuomba radhi kwa utaratibu ufuatao:

1. Kutoa taarifa ya kuomba radhi kupitia kipindi cha taarifa ya habari ya redio itakayorudiwa si chini ya mara tatu kwa siku.
2. Kutoa taarifa ya kuomba radhi kwa njia ya maandishi na
3. Kwa maagizo haya yatekelezwe si zaidi ya wiki mbili tangu tarehe ya barua hiyo ya Baraza.

Waheshimiwa Wajumbe napenda kuchukua nafasi hii kutoa taarifa kwamba uongozi wa kituo cha redio cha Zenji FM umetekeleza maagizo yote yaliyotajwa hapo juu, umeomba radhi kwa maandishi na maelezo ya taarifa ya habari ndani ya wiki mbili tangu kupewa taarifa iliyowataka kuomba radhi ambayo ilitumwa kwao tarehe 13 Februari, 2010. Taarifa ya kuomba radhi kwa maandishi imo kwenye barua ya kampuni inayomiliki kituo cha Redio cha *Zanzibar Media Cooperation* ya tarehe 25 Februari, 2010 yenye kumbukumbu Nam. ZMCL/Zenji/252 ambayo imetiwa saini na Meneja wa Kituo hicho cha Redio Ndugu Hafidh Kassim Hafidh, barua hiyo imeambatanishwa na CD ya taarifa ya habari ambayo ina maelezo ya kuliomba radhi Baraza.

Waheshimiwa Wajumbe naomba kuwasilisha taarifa hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe mimi nataka niwaulize tu kama mnaridhia kuombwa radhi taarifa hiyo.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Spika, pamoja na barua nzuri yenye nakshi lakini hii barua tunazungumza na mtu hatumjui wala hatumuoni. Ni vyema wakati mwengine au siku nyengine aje hapa mbele ya Baraza na tumuone.

Mhe. Spika: Nafikiri hilo jambo ilikuwa ni sisi tungemuarifu hapana shaka kwa kuwa ameweza kuyafanya haya ningetegemea sana na yeye angeweza kufika. Kwa hivyo, hilo ni tatizo la uongozi wetu tulipitikiwa kumuarifu kwamba barua yake ya kuomba radhi itasomwa leo na yeye angekuwepo hapa akasikia maneno yatakayotolewa na Baraza hili. Nashukuru kwa kutukumbusha kwamba mara nyengine tusisahau yule anayehusika na masuala haya tumwite ili awepo na asikie kama kuna maelezo au maagizo mengine yoyote.

Waheshimiwa Wajumbe naomba baada ya maelezo hayo sote tungeridhia suala hili.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Nakla zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 1 Februari, 2010.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Haki na Wajibu wa Serikali katika Kesi za Madai na Utaratibu wa Mwenendo wa Madai Dhidi ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Mswada wa Sheria wa Kuweka Haki na Wajibu wa Serikali katika Kesi za Madai na Utaratibu wa Mwenendo wa Madai Dhidi ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AFR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa idhini yako kwa niaba ya kambi ya upinzani na kwa niaba ya Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi naomba kuwasilisha mezani maombi ya kambi ya upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Haki na Wajibu wa Serikali katika Kesi za Madai na Utaratibu wa Mwenendo wa Madai Dhidi ya Serikali na Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 73

Vazi maalum wakati wa Kuendesha Baraza

Mhe. Ashura Abeid Faraji - Aliuliza:-

Spika wa Baraza la Wawakilishi huwa anavaa joho wakati wa shughuli za Baraza. Kwa nini Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza wao hawavai vazi hilo wakati wanapoendesha Baraza?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi) - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 73 kama hivi ifuatavyo:
Mhe. Spika, kabla sijajibu swali la Mhe. Mjumbe naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi Zanzibar shughuli zake huendeshwa kwa kufuata kanuni zilizokubaliwa na kupitishwa na Baraza lenyewe, chini ya maelekezo ya Katiba ya Zanzibar Kifungu cha 86(2). Miongini mwa Kanuni zinazotumika kuendesha Baraza ni Kanuni ya 140 inayohusu mavazi. Kanuni hiyo inatoa maelekezo juu ya mavazi yanayokubalika katika Baraza kwa Viongozi, Wajumbe, Watumishi, na Wageni wa Baraza.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatatvyo:

Mhe. Spika, kama nilivyosema katika maelezo yangu, kanuni ndizo zinazoongoza shughuli za Baraza. Spika wa Baraza amekuwa akivaa vazi la joho wakati wa kuendesha shughuli za Baraza kwa sababu Kanuni za Baraza zimekuwa zikielekeza hivyo. Lakini kwa kipindi kirefu cha uhai wa Baraza, Kanuni hizo zilikuwa hazielezi kwamba Naibu Spika na Menyekiti wa Baraza wavae joho wakati wa kuendesha Baraza. Marekebisho ya Kanuni yaliyofanywa kwenye Mkutano wa Baraza wa 17 ndiyo yaliyoweka utaratibu kwa Naibu Spika na Mwenyekiti kuvaa joho kama inavyosomeka kwenye Kanuni ya 140(2):

Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza watavaa joho na kivazi kingine chochote kati ya kanzu kwa mwanamke au suti ya kimataifa, viatu vya buti, makubadhi, au sandals za ngozi ya rangi moja.

Mhe. Spika, utekelezaji wa Kanuni hiyo utarajiwa kuanza mara moja kwani hivi sasa tayari maandalizi ya kupata mavazi hayo kwa ajili ya Naibu Spika, na Wenyeviti wa Baraza yameanza na yanaendelea vizuri.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi mimi nina swali moja dogo. Kwa kuwa vazi la Mhe. Spika, la joho ni alama ya cheo chake kama Spika. Ni kwa nini basi wakati Baraza linapoingia katika kamati ya Baraza Spika havui lile joho kwa sababu hapo cheo hicho kinakuwa hakipo na wakati huo anakuwa ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Baraza?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, muuliza swali hili ni Mbunge kupitia Baraza la Wawakilishi na katika Bunge utaratibu huo aliouleza unatekelezwa, kwa bahati sisi katika kanuni zetu hilo suala hatukuliweka lakini nafikiri Afisi ya Spika pamoja na Baraza litazingatia utekelezaji wake.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutufikisha siku ya leo. Pili nakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, hili vazi la joho asili yake ni wapi au linatokana na mabunge yote ya Jumuiya ya Madola na ikiwa hivyo ndivyo au ikiwa sivyo.

Je, Baraza husika linaweza kuvaa kivazi cha asili yao? Na kama jibu ndiyo, hatuoni kama kuna haja ya kuweka utaratibu kama Spika wetu sasa hivi avae kanzu, koti na kofia ya kiua pamoja na makubadhi?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, ni kwamba joho kwanza linapendeza, halafu linaonesha kwamba huyu mtu amependeza na hasa akiwa mnene kama Spika wetu na linaonesha kuwa ana cheo zaidi ya hawa wengine waliopo hapa. Kwa hivyo, mabunge mengi yanatumia utaratibu huo kuonesha tofauti kati ya Spika na Wajumbe wa kawaida.

Mhe. Spika, kusema kwamba kwa nini hatupitishi utaratibu wa kivazi cha kitaifa. Hilo suala kwa kweli ni uamuzi wa Baraza hili kama linataka kufanya hivyo liweke kwenye kanuni zake.

Nam. 50

Nyongeza ya Mishahara kwa Wafanyakazi

Mhe. Haji Mkema Haji – Aliuliza:-

Je, Mhe. Waziri ile nyongeza ya mishahara tuliyoidhinisha katika bajeti ya 2009/2010 na kutamkwa na Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi imeshafika kwa walengwa wote?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:

Mhe. Spika naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kumuarifu Mhe. Mwakilishi ni kweli kwamba kwa mujibu wa Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliahidi kufanya marekebisho ya mshahara kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza Serikali iliahidi kuongeza kima cha mshahara kutoka Shs. 80,000/= hadi Shs 90,000/=. Kimsingi suala hili tayari hatua zimeshachukuliwa.

Aidha, awamu ya pili ya utekelezaji wa suala hili, Serikali iliahidi kurekebisha kima cha chini kutoka Shs. 90,000 hadi Shs. 100,000/= , pamoja na kuzingatia miundo ya utumishi ya kada mbali mbali. Mhe. Spika, kimsingi suala hili pia limeshachukuliwa hatua kwa asilimia mia moja ikiwa ni pamoja na kufikiwa kima cha chini cha mshahara cha Shs. 100,000/= na kwa hivi sasa hatua zinaendelea za kuweka sawa miundo ya utumishi ya kada mbali mbali kwa kuzingatia muda wa wafanyakazi waliotumikia huko nyuma.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, wakati Serikali inapoagiza mishahara ya watumishi kupandishwa, Serikali huchukua muda mwingi kuteleza jambo hili.

a) Je, Serikali inapotoa tamko hilo huwa bado haina uhakika wa hizo fedha au inakuwa vipi?

b) Wakati tangazo la kima cha mshahara kinapotolewa na Serikali huwa kinawahusu watumishi wa Serikali, taasisi na makampuni. Lakini kwa hawa wenye makampuni agizo hili huwa wanalipuuza. Je, Serikali huchukua hatua gani kwa kampuni ambazo hazichukui hatua za kurekebisha mishahara kama serikali ilivyoagiza?

c) Mhe. Spika, sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi umetupa fursa ya kuajiri watumishi wawili na sisi tunawajibika kuwapandisha kima hawa watu, lakini mpaka hivi leo waziri wewe hajakupa uwezo wa kuweza kukimu wajumbe wako kuwakamilishia watumishi wetu. Je, juu ya suala hili Mhe. Waziri anatuahidi nini?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, *observation* ya Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali inachukua muda mwingi kutekeleza nafikiri niseme haya ni matatizo ya utekelezaji tu, siwezi kukataa kwa sababu yeye bila shaka ameshuhudia lakini sisi huwa tunajipanga vizuri na tuliposema tutaanza mwezi wa Oktoba basi tulikuwa tumeshajiandaa kifedha. Mhe. Spika, kwa fedha ya mishara sio tatizo tuliweka kwa mwezi wa Oktoba tutaanza kwa kiwango hicho.

Mhe. Spika, unajua kwenye utekelezaji kuna matatizo labda kama kuna matatizo sehemu fulani Mhe. Mwakilishi basi angetwambia tukenda kurekebisha. Lakini kwa taarifa tulizonazo kwa kweli mote mlimokusudiwa suala hili limeshachukuliwa hatua.

Mhe. Spika, matatizo ya utekelezaji ni kwamba tunayajua na sio lengo letu na kama nilivyosema tunajipanga vizuri kwa tarehe tuliyoweka basi tutowe mshahara kama ilivyopaswa.

Mhe. Spika, kuhusu matatizo ya makampuni hilo nalo ni kweli, makampuni siku zote wao wanapenda kujiongezea faida kwa hiyo wakiona kwamba waongezewe wafanyakazi wao wa chini mshahara huwa wazito. Hili nalo niseme pia ni la utekelezaji ni kwamba wale wenyewe wawe *sharp,* na pia ni kwamba wanavyo vyama vyao vya wafanyakazi na wizara ipo. Wakiona wamechelewa wapeleke malalamiko yao, naamini tutashirikiana kusaidia kulitatua.

Mhe. Spika, suala la mwisho kuhusu posho la watumishi wawili kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nafikiri nyongeza iliyotoka ni kwamba Baraza la Wawakilishi haimo kwa sababu Baraza la Wawakilishi ina muundo wake wa

utumishi maalum, sasa ukija ukipitishwa na muundo wa utumishi basi hilo litatekelezwa lakini hili nafikiri halikudhingatiwa na muundo wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, nyongeza ile Baraza la Wawakilishi haimo.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwa mujibu wa jibu lake mama alisema kwamba mshahara kima cha chini ulitoka sh. 80.000/= ukenda sh. 90.000/= na sasa wanaendelea kutoa sh. 100.000/=. Kwa hivyo, hapa mwelekeo mwaka huu wataongezwa tena sh. 10.000/= kwa hiyo zitakuwa sh. 110.000/=.

a) Je, ni kigezo gani ambacho Mhe. Waziri wanakitumia kwa kuongeza hizi sh. 10,000/= ukilinganisha na upandaji wa gharama za maisha?

b) Ni sababu zipi zilizopelekea utaratibu ule wa zamani ukaachwa wa kupewa *area?* Sasa hivi sijamsikia Mhe. Waziri kama kasema *area* zipo , yeye anasema kwamba mshahara mpya unakuwa unaanzia mwezi wa Oktoba.

Je, kuna utaratibu upi wa kuwapa hizi haki zao za nyuma au kuna utaratibu mpya kwamba mshahara mpya ukishatangazwa Juni basi kupewa kwake ni Oktoba na bila ya nyongeza (*areas*)?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Zakiya nilipokuwa natoa majibu ya msingi labda hakunifahamu. Azma ya serikali ilikuwa kutoa kutoka shilingi 80,000 kwenda kwenye shilingi 100,000, na tungekuwa na uwezo tungetoa kwa mpigo pale pale, lakini tukasema acha tujiweke vizuri twende kwa awamu. Kwa hivyo, ndio tukatoka kwenye shilingi 80,000 tukenda kwenye shilingi 90,000. sasa tunatoka 90,000 tunakwenda kwenye shilingi 100,000.

Labda pia amesema hizo shilingi elfu kumi kumi zitaongezeka mpaka lini? Hatukuweka kama hii ndio kigezo chetu kwamba tuongeze shilingi elfu kumi kumi aa!, kwa wakati huu tumekwenda hivyo tu, labda *asaa kheri* kesho kutwa mambo mazuri, mfano tu nasema usini-*quote*, naweza kusema tuongeze shilingi 35 elfu, 20 elfu, 15 elfu ikiwa hali ndogo, lakini tunakwenda kwa mujibu wa uwezo wetu na maombi ambayo tunayapata serikalini. Lakini lazima tujikite uwezo wetu ukoje tusiahidi kitu ambacho hatuwezi kukitekeleza.

Aliuliza pia suala la *areas*. Kwa kweli niliposoma kwenye hotuba nilisema kwamba *effective* tarehe hii, tungeshindwa tarehe ile kutekeleza basi tungelipa

areas, lakini tumesema kuanzia Oktoba na tumelipa Oktoba. Sasa naomba unifahamu hivyo hatukusema Julai tumesema Oktoba.

Nam. 11

Sababu za Wizi wa Fedha za Umma

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Nchi yetu imekuwa na matukio mbali mbali ya wizi wa fedha za umma ikiwemo mishahara ya watumishi maofisini. Miongoni mwa sababu zinazoweza kuhusishwa na uhalifu huo ni pamoja na uzembe na njama za watendaji, ukosefu wa vyumba imara vya kuhifadhia fedha (*strong rooms*) na ukosefu wa makasha madhubuti (*cash boxes*).

(a) Je, Mhe. Waziri, huoni kwamba kitendo cha Wizara ya Fedha chini ya Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kushindwa kuzipatia baadhi ya taasisi makasha ya kuhifadhia pesa kuwa ni udhaifu na uvunjaji wa sheria za fedha?

(b) Je, Mhe. Waziri unaelewa kuwa baadhi ya Halmashauri za Wilaya huhifadhi pesa zao katika droo za meza na mikoba ya ukili badala ya makasha?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija swali lake nambari 11 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, jitihada mbali mbali za kukumbushana zilichukuliwa na Wizara ya Fedha na Uchumi chini ya afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa nia ya kuondosha kasoro zinazojitokeza, lakini inaonekana bado sheria na taratibu ziliopo hazifuatwi ipasavyo. Hiyo ni kweli tunakiri kwamba hazifuatwi taratibu tulizoweka.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada hizo, Wizara ya Fedha imenunua Makasha makubwa na madogo (*Safes*/*Strong boxes*) na hutolewa bure pale taasisi inapotoa taarifa ya kwamba inahitajia. Si rahisi kwa Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kujua kwamba taasisi inahitaji au inahitilafu katika ofisi yake, au inataka ukubwa gani au inataka ngapi bila ya kupewa taarifa. Afisi hii huwa inashirikiana kwa karibu zaidi na taasisi husika pale panapohitajika kupatiwa ufumbuzi kwa kasoro iliyopo katika usalama na uhifadhi wa fedha za umma.

Mhe. Spika, taratibu za uhifadhi na usalama wa fedha za umma unafahamika ila tu unavunjwa, tuseme kwa makusudi kwa baadhi ya sehemu kwa malengo ya kufanyika kwa wizi. Kuna ushahidi tosha mara nyingi utakuta mlinzi wa pale anahusika au hata mhasibu mwenyewe anahusika. Wizara yangu kupitia Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ipo tayari saa zote kushirikiana na taasisi yoyote yenye upungufu katika suala la uhifadhi wa fedha za serikali, kinachotakiwa kutolewa kwa taarifa iwapo kuna hitilafu katika Afisi yenye kuhifadhia fedha za serikali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu marefu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba kunakuwa na udhaifu, na amekiri kuwa wajibu wa kutoa makasha ni wa Afisi ya Mhasibu Mkuu. Je, atakubaliana na mimi kwamba kwa kuwa zipo afisi nyingi ambazo hazina makasha afisi yake ndio itakuwa ya mwanzo kutunga sheria?

(b) kwa kuwa zipo taasisi hadi leo fedha za umma zinahifadhiwa ndani ya mikoba ya kili. Sasa wizara itapiga marufuku kuanzia leo kuhusu suala hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kusisitiza tena kwamba wizara yangu chini ya Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali itakwenda sambamba na wahasibu wote kuhakikisha kwamba makasha ya kuhifadhia fedha yamo au yapo katika kila kwenye taasisi ya fedha. Lakini ninachoomba tushirikiane zaidi katika kutoa taarifa, unajua siku hizi uchukuaji fedha kama alivyosema nitajibu kwenye swali (b) lakini umekua kwa sehemu nyingi sana, na kila mhasibu anajaribu kurahisisha. Lakini sasa pa kuziweka wapi? Sasa hilo naomba tushirikiane tutajitahidi kufuatilia sisi kuona kwamba haya makasha yanapatikana na kutunzwa ipasavyo.

Swali la pili, katika kusafirisha fedha tunaomba sana wanaosafirisha fedha watoe taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama wapate ulinzi wenye silaha katika kusafirisha fedha. Si vyema kuchukulia kwamba kuna usalama tu, ni hatari! bora kuchukua hadhari. Kwa kweli tunashukuru wahasibu wengi wanaosafirisha fedha nyingi hasa za mishahara huwa wanafanya utaratibu huo.

Kuhusu swali lake la (b) ni kweli wapo baadhi ya wahasibu wanachukulia fedha kwenye mikoba ya ukili. Hilo tumeshalisemea mara nyingi na tena tunazidi kutilia mkazo kwamba si ruhusa kuchukua fedha kwenye mikoba ya ukili, ni hatari, tena wengine mbali ya mikoba hiyo halafu wanapanda vespa

akianguka kama kapata ajali mambo yanamwagika baada ya watu kumsitiri yeye basi wanakimbilia fedha. Kwa hivyo, hili nalo tutajitahidi Mhe. Spika, tushirikiane kuona kuwa tunaliondoa kabisa kwa maslahi yetu sote.

Mhe. Spika: Unajua katika kutunza mazingira Mhe. Waziri wa Fedha huja na mkoba wa ukili. Sasa wahasibu wake naona wanamfuata yeye. (*Kicheko*)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza naipongeza serikali kwa asilimia mia moja kwa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wake wanapata mshahara kwa wakati.

Lakini pili Mhe. Spika, niishukuru wizara pia kwa jitihada zake za kuhakikisha kuwa zinakusanya mapato ili kuhakikisha kwamba walengwa zinawafikia kwa wakati pesa zile na kuondoa utata wa kujikimu kimaisha.

Swali. Je, kwa kuwa katika vyombo vya ulinzi hasa jeshini ninakotoka mimi, mara nyingi huwa siku ya mishahara ni siku maalum, wafanyakazi wanaambiwa leo ni siku ya mshahara kuanzia saa fulani hata kama mpaka usiku lakini fedha zile lazima uwepo na uchukue ili ziwe salama. Je, wizara ina mpango gani wa kuanzisha suala kama hilo katika nyanja zake zote ili kuondoa huu utata wa wizi ambao hauna usalama kwa wafanyakazi ambao hawahusiki?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwanza kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Fedha hasa sehemu za mishahara napokea pongezi zako za kuharakisha na kujitahidi kulipa mishahara kwa wakati na hiyo ndio azma yetu, mishahara ni *first charge item.* Kwa hivyo, tunahakikisha mara zote tunazichuma, tunazitunza vizuri na tunawalipa wafanyakazi. Kwa sababu nahisi kuwalipa wafanyakazi vizuri na kwa wakati wao ndio wenye mzunguko wote.

Pili kuhusu utaratibu wa siku maalum. Nakiri, ni rahisi kuweka utaratibu huo katika vikosi kwa sababu wao unajua ni vikosi vya ulinzi halafu wana taratibu zao, lakini kwa mawizara yetu ya serikali tunafanya zamu, lakini tunajitahidi hata hivyo. Kwa mfano, kuanzia jana tarehe 23, Machi tumeanza kutoa mishahara, sasa kila wizara imepangiwa siku yake, wanakwenda benki *cheque* wameshapewa wanakwenda wana-*cashe* kwa siku yake maalum. Sasa nafikiri ni suala la kujipangia tu ndani ya wizara wahasibu wale wote wanaokwenda kuchukua siku ile kwamba jamani tunaomba leo muwepo tumalize kulipa leo leo kisibaki kikalazwa.

Kwa hivyo, nafikiri ushauri wake Mheshimiwa ni mzuri, ni wa kufanyiwa kazi na sisi kama wizara tutauchukua tuhakikishe kwamba ushauri huu tuweze kuufuata mfano wa katika vikosi vyetu. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 51

Kesi za Udanganyifu Katika Mitihani

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Taarifa za Mhe. Waziri za karibuni zimekuwa zikieleza kwamba kesi za udanganyifu zimekuwa zikipungua, katika mitihani ya viwango mbali mbali vya mitihani. Kwa mfano, kwa mwaka watahiniwa wa *Form II* 2009 zilitokea kesi mbili tu na darasa la saba hakuna hata kesi moja.

Je, Mhe. Waziri ni skuli zipi zilizopatwa na kesi hizo za udanganyifu na hatua gani zilichukuliwa kwa wahusika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 51 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kesi za udanganyifu katika mitihani yetu ya darasa la Saba na Kidato cha Pili zimepungua katika mitihani ya mwaka 2009. Kwa watahiniwa wa Kidato cha Pili jumla ya kesi za udanganyifu ishirini na mbili (22) ziliripotiwa na wala sio kesi mbili (2) kama alivyosema Mhe. Mwakilishi na hakuna kesi ilioripotiwa kwa watahiniwa wa Darasa la Saba.

Skuli zilizohusika na udanganyifu wa mitihani ya Kidato cha Pili mwaka 2009 na idadi ya watahiniwa waliohusika ni kama ifuatavyo:-

	SKULI	**WILAYA**	**IDADI YA WATAHINIWA**
1.	Regeza Mwendo	Magharibi	04
2.	Mwanakwerekwe “A”	Mjini	03
3.	Kwamtipura	Mjini	01
4.	Jambiani	Kusini	03
5.	Mtende	Kusini	01
6	Marumbi	Kati	01
7.	Matemwe	Kaskazini “A”	01
8	Shumba	Micheweni	01
9	Tumbe	Micheweni	02

10	Kangagani	Wete	01
11.	Wesha	Chake Chake	03
12.	Chanjamjawiri	Chake Chake	01
	JUMLA		**22**

Wanafunzi wote waliohusika na udanganyifu huo walifutiwa matokeo yao.

Mhe. Spika, napenda kutoa wito kwa wanafunzi wote kwamba wajiepushe kabisa na vitendo vya udanganyifu katika mitihani kwani vinasababisha kufutiwa matokeo na hakuwasaidii kuinua uwezo wao wa kujifunza. Tunaagiza waendelee kufanya juhudi katika kujifunza badala ya kujiingiza katika vitendo vya udanganyifu katika mitihani. Ahsante sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Amekiri kwamba kesi hizo zimetokea kwa baadhi ya maskuli na ametaja na idadi ya wanafunzi.

(a) Je, katika udanganyifu huo hakuna walimu walioshiriki, na kama wapo wamechukuliwa hatua gain?

(b) Hivi sasa vijana wengi wamepata ari ya kujiendeleza kusoma na hukwamba *Form IV* kwenda *Form V*, lakini hununua mitihani ili waweze kusonga mbele na mtihani huo unauzwa shilingi 50 elfu. Je, haoni Mhe. Waziri kwamba hicho ni kikwazo kwa wanyonge?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, walimu ambao wamehusika na tatizo hili la udanganyifu mpaka sasa hivi hatuna taarifa nao na kwa maana hiyo hakuna hatua ambayo imechukuliwa.

Mhe. Spika, swali (b) ni kwamba, kweli napenda nikubali kuwa wanafunzi wengi ambao kwa bahati mbaya hawabahatiki kuendelea na masomo huwa wanakuwa na ari ya kujiendeleza katika madarasa ya kumi na mbili (12) hadi ya kumi na nne (14). Lakini ni kwamba kuna malipo yanayotozwa ambayo Mhe. Mwakilishi amesema ni shilingi elfu hamsini, lakini nadhani sio shilingi elfu hamsini ni shilingi 45 elfu ambazo kwa kweli mimi binafsi naziona ni nyingi, lakini kutokana na gharama za mitihani ni lazima hizo gharama tuzifidie.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba, kwa kuwa swali linasema kuhusiana na mitihani katika viwango mbali mbali, na kwa kuwa karibuni tu kumetoka matokeo ya mitihani ya kiwango cha darasa la kumi na mbili, na kwa kuwa katika matokeo hayo kunaonekana kwa ilivyozungumzwa na kutangazwa

kuna udanganyifu mkubwa sana uliotokea katika mitihani hiyo. Naomba nimuulize Mhe. Waziri.

(a) Je, wizara imelifuatiliaje suala hili lililoitwa la udanganyifu wa mitihani hii ya *Form IV*?
(b) Kama imefuatilia, imethibitisha kuwa mambo hayo ni ya kweli?
(c) Kama hilo limefanywa na kama ni kweli, ni nani mdhamini wa usimamizi wa mitihani hii na msimamizi huyo kachukuliwa hatua gain?
(d) Mwisho je, katika hili hakuna mpango wa kupunguza wanafunzi waliopasi vizuri zaidi Zanzibar?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, suala la kwanza limeulizwa kwamba je, wizara imelifuatilia suala hili la udanganyifu? Napenda kumjibu kwamba ni kweli kwamba wizara imelifuatilia na ndio maana tukatoa matokeo ambayoa tumeyatoa katika jadweli niliyoizungumza, na hatua zilizochukuliwa ni kama zile ambazo nimezisema.

Lakini kuhusu suala (b) ambalo amesema kuwa wizara imethibitisha? Ni kweli kwamba wizara imethibitisha kuwa kulikuwa na udanganyifu na waliohusika tayari wameshachukuliwa hatua.

Jibu (c) kwamba nani mdhamini wa mitihani hii? Mhe. Spika, wizara inasimamia mitihani hii lakini udanganyifu uko wa aina nyingi. Moja ya udanganyifu ni kwamba wanafunzi wenyewe huwa wanachukua vikaratasi ambavyo havitakiwi kuchukuliwa katika chumba cha mitihani, hilo ni moja la udanganyifu na sio kwamba udanganyifu wa kupata mitihani kabla lakini kwa ufupi udanganyifu uko wa aina nyingi ambao wanafunzi wenyewe kwa jumla ndio huwa wanahusika.

Jibu (d) mpango wa kuwapunguza wanafunzi huu mimi sikubaliani naye kwamba kuna mpango wa kupunguza wanafunzi waliopasi vizuri katika madarasa haya. Kila mwanafunzi ambaye amepasi vizuri anayo haki ya kuendelea na wizara inasimamia kwa makini sana kuona kwamba kila aliyepata sifa basi anapatiwa fursa katika skuli zetu mbali mbali. Hivi karibuni nadhani tumewatangaza wanafunzi wengi ambao wamepasi kidato cha nne kuingia darasa la kumi na tatu (13) hata wale waliofaulu katika matokeo ya mitihani ya faragha. Wamepata fursa katika skuli zetu mbali mbali zilizopo hapa Unguja na Pemba.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, wanafunzi wetu wanajitahidi sana katika kutafuta elimu kwa njia yeyote ile kuhakikisha kwamba anafikia

kiwango ambacho kinakubalika. Lakini kwa bahati mbaya kuna wengine hushindwa njiani kutokana na kukosa kama bahati, kwa sababu unaweza kuwa mwanafunzi mzuri katika darasa na ukashindwa na yule pocho katika mtihani wa taifa.

Kwa kuwa serikali kuanzia mwaka huu kama sikosei imeandaa mpango mpya wa kuondoa viwango au ada za mitihani kwa *Form IV* na *Form VI*. Je, kwa hawa wanafunzi wa *private* wao hutakiwa walipe shilingi 48 elfu, serikali ina mpango gani kwa wanafunzi wetu hawa kuwapunguzia fedha hizo ili na wao waweze kukukimu kufanya mitihani yao na kuhakikisha kuwa wanakwenda sambamba na wenzao.

Mhe. Spika: Swali linahusu udanganyifu wa mitihani. Hebu litafutie utaratibu wa kuliuliza kwenye swali la msingi. Tuendelee.

Nam. 42

Mhe. Subeit Khamis Faki (Kny: Mhe. Abass Juma Muhunzi) – Aliuliza:-

(a) Ni sababu gani zinazoifanya sekta binafsi na watu binafsi kutoanzisha Magazeti na TV binafsi hapa Zanzibar?

(b) Vyombo vya Habari vya binafsi vimejikita zaidi katika uanzishaji wa Radio za mawimbi ya FM, Je, ni sababu gani zinazovutia aina hii ya Vyombo vya Habari tafauti na Magazeti na Radio?

(c) Je, kuna ugumu gani kusiwe na vipindi vinavyo endeshwa kwa lugha tafauti na Kiswahili wakati utandawazi unaunganisha wasikilizaji wa mataifa na nchi nyingine za dunia?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa wazima katika kikao hiki na kujumuika pamoja tena.

Pili Mhe. Spika, naomba nipongeze kiti chako pamoja na mwenyekiti na watendaji wako wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuonesha utawala bora na kufuatilia ahadi ambazo zimezungumzwa hapa hadi kufikia ripoti ya leo asubuhi.
Tatu niwapongeze na hao waliyoomba radhi pia, kwa sababu na wao wametimiza wajibu wao katika utawala bora.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimthibitishie Mhe. Mwakilishi kuwa hakuna sababu inayozuia vituo vya televisheni binafsi au magazeti kuanzishwa hapa Zanzibar. Wizara yetu ya Habari, Utamaduni na Michezo ambayo ina Tume ya Utangazaji Zanzibar tayari hivi sasa imesajili vituo vinne vya televisheni binafsi. Kwa hivi sasa baadhi ya vituo hivyo binafsi vilivyosajiliwa vimeanza kazi kwa kutumia teknolojia ya gharama nafuu ya nyaya na sio mawimbi. Vituo hivyo binafsi vya televisheni ni *Furaha Cable* na *Zanzibar Cable Television* ambavyo pia navyo hubuni na kusambaza vipindi na matangazo yao kwa kutumia njia hiyo ya nyaya.

   Vituo vingine vya televisheni binafsi vilivyosajiliwa na ambavyo vinatarajiwa kusambaza matangazo yake kwa njia ya mawimbi itakayotumia minara pamoja na anga la mawimbi hayo.

b) Ni kweli kwamba vyombo vingi vya habari vya watu binafsi hapa Zanzibar vimejikita zaidi katika uanzishaji wa redio za mawimbi ya FM. Hii ni kwa sababu moja tu, nayoa ni kwamba teknolojia ya FM ni rahisi zaidi kuliko teknolojia nyengine zote pamoja na hata kuchapisha magazeti. Na tija inayorudi ya faida kutokana na uwekezaji huo kwa redio hizo za FM ni kubwa na haraka zaidi. Mara nyingi kutokana na uzoefu wetu wafanyabiashara wa Zanzibar wamekuwa na mazowea ya kuwekeza katika uwekezaji wa kiwango cha chini kuliko kuwekeza katika kiwango cha juu.

   Mhe. Spika, nitatoa mfano. Gharama za mtambo wa chini kabisa wa FM Redio ni shilingi milioni 20 wakati uwekezaji wa kiwango cha chini kabisa wa TV inayotumia mawimbi ni shilingi milioni 500. Bado tunaendelea kutoa wito kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kuwekeza katika uwekezaji wa kiwango cha teknolojia ya juu zaidi na sio vituo vya FM tu hapa Zanzibar.

c) Vituo vya utangazaji vinavyoanzishwa humu nchini, vinatakiwa kurusha matangazo yake kwa kutumia lugha za taifa pamoja na ya kimataifa. Lugha rasmi zinazotumika hivi sasa ni Kiswahili na Kiingereza.
   Kituo cha Utangazaji kilichosajiliwa chini ya sheria ya Tume ya Utangazaji kinaweza kutumia lugha nyengine yoyote ile, ili mradi lugha hiyo iwe inaweza kutafsiriwa moja kwa moja na iwe

miongoni mwa lugha hizo mbili (Kiswahili au Kiingereza) ili iweze kufahamika zaidi na jamii nzima ya Wazanzibari.

Kwa mfano, ni vipindi vya kujifunza lugha ambavyo hutolewa tafsiri moja kwa moja kwa Kiswahili na kwa Kiingereza. Hii ni kwa sababu matangazo ya kituo cha redio yanatakiwa kuwafikia walio wengi zaidi kwa mujibu wa sheria yetu na hivyo Kiswahili na Kiingereza ndizo lugha mbili zilizochukuliwa kwamba zinawafikia watu wengi zaidi hapa Zanzibar.

Nitatoa mfano wa redio yetu ya serikali ya STZ, kuna baadhi ya vipindi maalum ambavyo hurushwa kwa wale wapenzi wa nyimbo za Kiarabu ambazo hutolewa maudhui na tafsiri yake na maelezo yake hususan wale wapenzi wa nyimbo za Ummu Kulsum au Farid Al- Atrash ambazo hutolewa tafsiri zake, au kwa zile nyimbo za Kihindi kama vile za Moh'd Rafii na Asha Bosle au nyimbo za Kilatino, Charanga za kina Havana Cluba na Ibrahim Ferere, nazo hutolewa tafsiri zake. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi navipongeza vyombo vyote vya habari vya serikali na vya watu binafsi kwa kutupa habari mbali mbali na hasa wakati tuliokuwa na kiza katika nchi yetu, walijitahidi sana ili wananchi wapate matokeo mbali mbali juu ya nchi yao yanavyoendelea.

Pamoja na pongezi hizo nina swali dogo tu.

Mhe. Spika, kumekuwa na taarifa kwa baadhi ya vyombo vya habari kutokea makosa katika usomaji wa taarifa zao. Kwa mfano, Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano Mhe. Machano Othman Said, mfano tu huo, ikatoa taarifa hiyo lakini bila ya kuomba radhi kuwa nilikosea na wakati wenzetu Zenji FM wameomba radhi kutokana na makosa yaliyojitokeza ni uungwana mzuri. Je, wataalamu au wizara ina mpango gani wa kuwaelimisha watu wetu wanaosoma taarifa za habari pindi linapotokea kosa wakaomba radhi?

Mhe. Spika: Labda Mhe. Ali Suleiman anatupeleka katika ile lugha, sasa kama wakati mwengine lugha inakuwa siyo ndio anakuja na swali kwamba vituo hivyo vingekuwa vinaomba radhi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa naamini pongezi hizo kwa vyombo vya habari hususan wakati tukiwa na ukosefu wa umeme hapa kwetu kufanya kazi zao naamini zitafika na

wenyewe wameshazisikia kwa sababu vipo hapa sasa hivi na vinafanya kazi yake.

Mhe. Spika, la pili kwa kweli kuna semina mbali mbali huwa zinatolewa na Tume ya Utangazaji na pia kuna semina ambazo zinaendeshwa na Baraza la Kiswahili la hapa Zanzibar kuhusiana na lugha ambazo huwa zinafanywa kwa kulengwa mahsusi hawa wafanyakazi wa vyombo vya habari hususan wale wasomaji zile taarifa za habari, ili lugha iwe nzuri pamoja na taarifa nyengine.

Lakini makosa madogo madogo kama binadamu huwa yanatokea na pale wanapogundua makosa yale mara nyingi wakati wa taarifa ya habari basi huchukua hatua ya pale pale kuomba radhi. Kwa hiyo, hilo tutaliendeleza zaidi sisi kupitia semina za Tume ya Utangazaji pamoja na zile semina za lugha kupitia Baraza la Kiswahili. Lakini tutashajiisha zaidi kwamba hili lizungumziwe katika semina hizo ili waweze kutambua haya matatizo madogo madogo na kuweza kuyaondoa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, navishukuru sana vyombo vya habari vya Zanzibar kwa kuongezeka ili wananchi kupata kujua habari muhimu zinazotokea katika nchi.

Lakini Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi moja ambayo ilijiunga mapema na TV ili kuonekana na kuongeza vyombo vya habari na wananchi kupata ufanisi zaidi. Je, kuna sababu zipi za msingi zinazozuia Zanzibar kutojiunga na *satellite* ili wananchi walioko vijijini kupata habari muhimu zaidi?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kabisa miongoni mwa nchi zilizoweka historia hapa Barani Afrika katika TV ya rangi moja wapo ni Zanzibar. Kwa sababu nia ilitolewa na Rais wa Kwanza wa Serikali ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume mwaka 1971. Ile nia yake imeandikwa pale *Karume House* wakati wa kuingia tu, imeandikwa nia ambayo aliitolea kauli na mpaka leo hiyo nia imehifadhiwa iko hapo kwa wale wanaotembelea pale *Karume House*.

Kutokana na historia hiyo tumeweza kuiendesha TV hiyo hadi kuwashinda wenzetu wote pamoja na Tanzania Bara ambao wameanza TV yao miaka 25 baada yetu sisi.

Sasa kutokana na hilo na kwa kuwa hatujafanya mabadiliko makubwa sana ya mitambo ndio maana mitambo yetu imekuwa michakavu na teknolojia ile kupitwa. Hivi sasa tayari programu maalum ya kuanza mchakato imeshaanza ya kubadilisha mitambo hiyo ambayo tunataka kuelekea kwenye mfumo wa

digital. Ninaamini tutakapopata uwezo kamili kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo pamoja wafadhili, basi na serikali yenyewe naamini hicho kituo kipya kitakachokuja kitakuwa na teknolojia hiyo sio ya kuwafikia wananchi vijijini tu, hadi mwambao huu mzima *CCTV* Zanzibar tutaweza kuonekana.

Nam. 15

Afisi ya Mkemia Mkuu Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania Bara zimeamua kuboresha Afisi zao za Mkemia Mkuu wa Serikali ili kupambana na uhalifu. Mfano, Afisi ya Mkemia Mkuu wa Tanzania ina maabara zisizopungua tano ambazo huchunguza vyakula, vinasaba *(DNA)*, madawa na vipodozi, na mambo ya uhalifu wa viungo *(Forensic Laboratory)*.

(a) Je, Afisi yetu ya Zanzibar ina maabara ngapi.

(b) Je, maabara zilizopo zina uwezo wa kuchunguza vinasaba *(DNA)* na uhalifu wa viungo vya wanadamu kama *Albino*.

(c) Miongoni mwa changamoto iliyopo Zanzibar ni kukosekana kwa Mkemia Mkuu kwa muda mrefu na kwamba aliyepo amekuwa akikaimu nafasi hiyo kwa muda wote huo bila ya kuthibitishwa na kupewa stahili zake.

Je, Mhe. Waziri kwa nini Kaimu Mkemia Mkuu wa Zanzibar hajathibitishwa baada ya kupita muda mrefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar ina maabara kama zifuatazo:-

Maabara moja ipo Unguja eneo la Mwanakwerekwe na nyengine Pemba Wilaya ya Chake-Chake. Maabara hizi mbili hushirikiana na Maabara ya Afya ya Jamii *(PHL)* iliyopo Pemba kwa uchunguzi zaidi pale inapohitajika. Pia ipo Maabara nyengine ya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ambayo

inashirikiana kikamilifu na Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Zanzibar katika shughuli zake za uchunguzi. Wizara imeweza kupatiwa vifaa vingi na bora kwa kupitia ufadhili wa *ADB* na *WHO* na hivyo kuboresha utendaji wa kazi wa maabara hizo. Maabara kwa sasa haina vifaa kwa kuchunguza vinasaba mfano viungo vya *albino*. Pale inapohitajika kufanya uchunguzi kama huo, sampuli hupelekwa kwa Mkemia Mkuu Tanzania Bara kwa uchunguzi kwani yapo mashirikiano ya karibu na wenzetu wa Tanzania Bara. Lakini hadi sasa hatujapata kesi ya aina yoyote ya uchunguzi wa viungo vya *albino*. Hata hivyo, wizara ipo mbioni kushughulikia kupatikana kwa huduma ya uchunguzi wa *DNA* hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaendelea na hatua ya kulishughulikia suala la uthibitisho na stahiki za Kaimu Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba hadi sasa Zanzibar hatuna mashine ya kupimia vinasaba *(DNA).* Kwa kuwa kesi sasa zinaongezeka hadi katika ndoa. Ni lini SMZ itatutafutia mashine hii ili kupunguza migogoro katika ndoa za Wazanzibari.

Swali (b) kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba lipo tatizo katika Ofisi yetu ya Mkemia Mkuu wa Serikali, pia alikiri kwamba hadi sasa bado Mkemia Mkuu aliyepo hajathibitishwa. Je, ni muda gani hadi sasa suala hili lipo na lini atathibitishwa.

Swali © Mhe. Naibu Waziri anaweza akanambia ni sababu ipi ya msingi ambayo ilimuondosha Dk. Mashimba na kuhamia katika Ofisi ya Mkemia Mkuu Dar es Salaam.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza kuhusu mashine ya *DNA*. Suala hili la mashine hivi sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tunalishughulikia. Tulifikiria kwanza mashine iliyopo Pemba ya *PCR* inaweza kufanya shughuli za *DNA.* Kwa hivyo, tukamleta mtaalam huyu Dk. Ernest Mashimba ambaye ni Mkemia Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wataalam wake wakaja hapa hivi karibuni, wakenda Pemba wakaiangalia mashine ya *PCR. PCR* ni *Polymerize Chain Reaction* ambazo ni *DNA* lakini *DNA* zilizokuwa katika mfumo wa *chain*.

Lakini wataalam hao wakatoa ripoti kamili, ripoti yao tunayo hivi juzi nimeipokea na tunaishughulikia. Mambo waliyotuandikia katika ripoti hiyo ni manne tumetakiwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tuyashughulikie.

Naomba Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nitaje kidogo kidogo. La kwanza akasema *DNA legislation should be in place.* Yaani sheria ya *DNA* itengenezwe. Pili *Procurement of New and Modern Instrument the ABI 3100 or the ABI 3230 or ABI 3500. These are the latest state of the art technology in Human DNA testing and are used instead of outdated techniques of slab gel electrophoresis such as agar rose electrophoresis (which is tedious to manage and not accurate).*

Kwa ufupi akasema kama tunataka kuagizia basi tulete *new and modern technology* akazitaja hizo mashine zenyewe ambazo hizi ndio zinatoa matokea yaliyokuwa *accurate*. Hapa Mhe. Spika, ndio wizara tunashughulikia kwa sababu tunatafuta bei zake na nani atakayeweza kutuletea haya mambo. Baada ya kupata hizo kikamilifu tena tutaiarifu serikali kuu kama itakuwa na uwezo au tutafute mtu ambaye ataweza kutusaidia. Kwa hivyo, hatutaki kufanya mambo ya haraka haraka au kubabaisha, tunataka tufanye kitu cha uhakika kabisa.

Mhe. Spika, pili kuhusu stahiki za Kaimu Mkemia Mkuu wa Serikali hivi sasa tunalishughulikia na inshaallah karibuni atapata haki zake zote anazostahiki.

Mhe. Spika, tatu Dk. Ernest Mashimba wewe mwenyewe binafsi unamjua umesoma naye toka *form III* mpaka *form VI* katika Skuli ya Lumumba pamoja na mimi. Baadae akapewa *scholarship* akenda *University of Dar es Salaam* akafanya *degree* yake ya mwanzo. Baadae kama sijakosea akenda Australia akafanya *degree* yake ya pili, akafanya na *PhD* yake katika mambo ya *technology*.

Aliporudi hapa akateuliwa kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini likatoka tangazo la Mkemia Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akaomba akapata. Baada ya kupata kwa sababu yeye alikuwa ni mteuliwa wa Mhe. Rais wa Zanzibar ikabidi aombe mwenyewe ruhusa akakubaliwa akenda kufanya kazi huko Bara.

Kwa hivyo Mhe. Spika, sisi hatukuwa na uwezo wa kumzuia Dk. Ernest asiende Bara. Aliruhusiwa rasmi na mimi ni sahibu yangu mkubwa sana na kanambia hivi karibuni karibu atastaafu na ninatarajia akistaafu tutamchukua kwa mkataba. Huyu ni Mzanzibari, kijana mzuri, hodari na juzi tulikuwa nae pamoja Pemba. Mhe. Spika, ni matarajio yangu kwamba Dk. Ernest Mashimba iko siku atarejea nyumbani.

Nam. 25

Taa kwa Wapanda Baiskeli wakati wa Usiku

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Vyombo vya barabarani, gari, vespa, honda, ciao na baiskeli hutakiwa kuwasha taa wakati wa usiku ili watembeao barabarani waweze kuviona vyombo hivyo. Hivi sasa wapanda baiskeli wengi hawawashi taa wakati wa usiku.

(a) Je, Mhe. Waziri utaratibu huu umehalalishwa kisheria.

(b) Kwa kuwa wapanda baiskeli hupita mbele ya askari wa barabarani bila ya kuwasha taa na bila ya kuulizwa chochote. Je, Mhe. Waziri hiyo sheria inayokataza kuendesha baiskeli bila ya taa wakati wa usiku imeondoshwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba vyombo vyovyote vinavyotembea katika barabara wakati wa usiku vinatakiwa kuwasha taa ili watumiaji wote wa barabara waweze kuviona vyombo hivyo.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Utaratibu wa baiskeli kuendeshwa bila ya kuwasha taa wakati wa usiku haukubaliki kisheria.

(b) Sheria inayokataza kuendesha baiskeli bila ya kuwasha taa wakati wa usiku haijafutwa. Suala la wapanda baiskeli kupita mbele ya askari wa barabarani bila ya kuchukuliwa hatua au kuwasha taa na bila ya kuulizwa chochote, hili ni tatizo la utekelezaji wa sheria. Hivyo, ni wajibu wa taasisi zote kuhakikisha kuwa sheria hiyo inafanya kazi kama ilivyokusudiwa ili kuepusha ajali za makusudi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, swali hili nimelileta hasa tukizingatia kwamba hivi sasa kuna vilio vikubwa sana katika mji wetu na hata vijijini. Kwa sababu utaratibu wa kutembea bila ya taa kwenye baiskeli umekuwa kama sheria imefutwa wananchi wameruhusiwa kufanya hivyo.

Lakini kwa kuwa jibu lake Mhe. Waziri kasema kwamba sheria hiyo bado ipo na vyombo vinavyohusika vifanye kazi yake. Je, ana wito gani kwa wananchi hasa wanaotumia vyombo hivi kuhakikisha kwamba wanaweka taa ili baiskeli zao ziwe salama wakati wanapopita katika barabara na asiyefanikisha suala hilo achukuliwe hatua.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa kawaida baada ya kutungwa sheria watekelezaji wa sheria wanatakiwa waifuate. Natoa wito kwa wananchi wafuate sheria na kwa kosa la baiskeli faini yake ni dola tano ambayo si kidogo kwa mpanda baiskeli. Kwa hivyo, tunawaomba askari na wengine wanaohusika na suala hili wachukue sheria kama inavyotamka.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mbali ya wale wapanda baiskeli ambao wanakwenda bila ya taa hasa wakati wa usiku. Je, wale wanaoendesha magari wakawa na taa moja ya pili haiwaki. Ni hatua gani au sheria gani iliyopo dhidi yao kwa sababu hawa nao huwa wanahatarisha maisha ya watu hasa kwa wapanda vespa, wapanda baiskeli na waendesha gari wenzao. Ni wito gani unautoa na ni hatua gani zitachukuliwa dhidi yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, waendesha vyombo vya moto vya maringi manne, maringi mawili, waendesha baiskeli, sheria imepitishwa na Baraza la Wawakilishi na inasimamiwa na Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi na inatekelezwa na vyombo vya Usalama Barabarani kama Polisi. Kwa hivyo, kuwa na gari ambayo ina taa moja nalo ni kosa na kwa hivyo madereva na hata sisi ambao tunatembea kwa miguu sote tuna haki, hata raia ana haki ya kuarifiana na polisi ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tunategemea polisi ndio waweze kusimamia sheria hii. Kwa kuwa polisi wenyewe wanapanda baiskeli bila ya taa usiku. Sasa nani atatekeleza sheria hii. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba ipo haja kazi hii sasa tukawapa Kikosi cha Valantia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kama polisi wanaweza kupanda baiskeli bila ya taa, ukiwapelekea Valantia nao watapanda baiskeli bila ya taa. Sasa mimi nafikiria sheria inataja kwamba askari wa Usalama wa Barabarani na mpaka sasa hivi ni polisi, kwa hivyo tuwaachie polisi wafanye kazi yao. Nafikiri hata raia ana uhuru au haki ya kumkamata askari polisi. Kwa hivyo, pengine ukimuona askari kama huyo mheshimiwa mkamate wewe umpeleke katika vyombo vya sheria.

Ingawa jana hapa tuliambiwa polisi aliambiwa akakamate gari ya polisi ikashindikana kidogo. Lakini kwa hivi raia akimkamata polisi anakubalika na hakuna kosa.

Nam. 44

Changamoto Zinazolikabili Zao la Karafuu

Mhe. Ali Abdalla Ali - Aliuliza:-

Zao la karafuu lilikuwa ni uti wa mgongo wa uchumi na limekuwa likisaidia sana uchumi. Lakini kwa sasa linakabiliwa na changamoto nyingi kama vile mikarafuu mingi kukauka, mkakati mdogo wa upandaji wa mikarafuu mipya, bei ndogo kwa wakulima, kuuzwa kwa magendo, pamoja na kujitokeza kwa vipaumbele vingine vya kiuchumi kama vile utalii.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani wa kupunguza changamoto zilizopo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

(b) Je, kwa sasa liko zao mbadala lenye tija zaidi kiuchumi ambalo Serikali inatilia mkazo na kuchukua pahala pa karafuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba zao la karafuu linakabiliwa na changamoto nyingi, Wizara inaendelea na mikakati ya kushajiisha wakulima kupanda na kuitunza mikarafuu yao kwa kuwatumia maafisa ugavi na wataalam wake katika ngazi mbali mbali za wilaya na vijiji.

Wizara pia inazalisha miche isiyopungua laki tatu kila mwaka na kuwasambazia wananchi bila malipo.

Mhe. Spika, vile vile Wizara yangu inaendelea kushirikiana na vyombo vyengine vinavyohusika na kuona inalipatia ufumbuzi unaostahiki suala la soko la karafuu. Wizara yangu pia inaendelea kushirikiana na vyombo vya ulinzi, viongozi mbali mbali pamoja na wananchi kwa ujumla katika kuhakikisha kwamba zao hili

adhimu haliuzwi au kusafirishwa nje ya nchi kwa njia za kimagendo.

b) Mhe. Spika, pia Wizara yangu bado haijapata zao mbadala lililochukua nafasi ya zao la karafuu kwa tija. Aidha, mkazo utaendelea kuwekwa katika kuhakikisha kwamba mazao mengine yanapatikana ili kusaidia kuongeza tija kwa nchi yetu. Hata hivyo, wananchi kwa sasa wanafaidika kwa kujitokeza kwa shughuli za utalii ambazo zinashika sehemu kubwa ya kuinua uchumi wetu na wananchi kwa ujumla, pamoja na kuongezeka kwa hoteli za kisasa za kiutalii hapa nchini Zanzibar.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza na mimi nikubaliane na muuliza swali Nam. 44 kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Lakini nimesikitishwa kidogo na Mhe. Naibu Waziri alipojibu kwamba mpaka sasa hivi hakuna zao mbadala ambalo linakamata nafasi ya zao la karafuu.

Lakini katika juhudi za serikali Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ilijitahidi sana kuagiza matrekta ili kupata zao mbadala hasa mazao ya nafaka. Kwa sababu mazao ya nafaka kama mpunga yakizaliwa kwa wingi inapunguza mfumko wa bei. Itakuwa tumeacha zao la biashara tumetafuta zao la chakula. Pindipo zao la nafaka likiwa kubwa na kupunguza mfumko wa bei, serikali itakuwa haina gharama kubwa ya kufikia chakula katika nchi.

Je, Mhe. Waziri hivyo katika matrekta yale pamoja na juhudi za serikali kupunguza bei ya mbolea yaani kufidia, wizara yake katika kutathmini imefikia kiasi gani. Yaani nakusudia bado mazao kama ya mpunga yamepanda au yameshuka au yapo pale pale. Kama hayajapanda kwa nini hayakupanda wakati matrekta yameagizwa kwa wingi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba kwa ujumla ukulima wa mpunga umepanda kwa sehemu kubwa sana. Mhe. Spika, kwa kupitia Baraza lako tukufu nawapongeza sana wakulima wa Unguja na Pemba kwa juhudi wanazozichukua za kulima mpunga. Idadi kamili kiasi gani imepanda tutaweza kuileta kwa maandishi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mikarafuu imekuwa ni uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar kwa muda mrefu. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lake amekiri kwamba kuna mkakati mzuri wa wizara wa kuendeleza hili zao. Je, ni utafiti gani unaofanywa kuhusiana na vifo vya mikarafuu. Ni

kiwango gani mikarafuu inapotea kila mwaka. Ni maeneo gani ambayo mikarafuu hiyo inapotea. Ni sababu gani zinazopelekea kufa kwa mikarafuu hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba suala la mikarafuu wizara yangu ilikuwa inafanya kazi ya kutoa miche tu kama nilivyosema lilikuwa liko sehemu nyengine. Lakini sasa hivi tayari imeshafanywa tathmini kwamba na zao hili sasa hivi linaletwa katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira moja kwa moja. Yaani suala la mikarafuu yote sasa itamilikiwa na Wizara ya Kilimo.

Sasa baada ya kukabidhiwa rasmi sisi tutafanya sensa na kujua mikarafuu mingapi ina uwezo wa kuzaa na mikarafuu mingapi ambayo tayari haizai tena na mingapi imekufa.

Lakini pia Mhe. Spika, natoa wito katika Baraza hili kwa Waheshimiwa Wawakilishi sote jamani tujitahidini zaidi kule Pemba kila pembe unayopita unakuta mapande ya mikarafuu. Kwa hivyo, inaonekana uharibifu wa mikarafuu kule Pemba umeongezeka kuliko hata hapa Unguja. Sasa ile kasi ya kupanda ni kubwa lakini na kasi ya uharibifu kule Pemba ni kubwa. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi sote tujitahidi kwa ile mikarafuu tuliyonayo na tujue kwamba hili ni zao la taifa na bado linategemewa na serikali yetu pamoja na wananchi kwa ujumla, tuhakikishe kwamba wananchi hawalikati.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba bado zao la karafuu lina matatizo. Mhe. Spika, hapo zamani dunia nzima karafuu ilikuwa inalimwa katika nchi yetu, lakini sasa hivi kuna nchi zaidi ya kumi zinalima karafuu. Je, haoni hiyo ni changamoto kwetu.

Swali (b) hivi sasa kuna nchi jirani zinanunua karafuu kwa magendo na zinauza nje kwa nembo yetu sisi. Je, hilo ni kweli au tuhuma tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nataka nikubaliane naye kwamba nchi nyengine nyingi zaidi ya Zanzibar nazo zinazalisha karafuu. Lakini karafuu iliyopo Zanzibar ni bora kuliko karafuu yoyote inayotoka katika sehemu nyengine za dunia.
Jibu (b) nilijibu kwamba viongozi mbali mbali pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama tunatakiwa tuhakikishe kwamba zao letu haliuzwi nje kwa magendo. Kuna taarifa zinazosema kwamba labda Kenya ndio wachukuaji wa karafuu zetu nyingi sana na sheria zao pale nafikiri magendo ni kutoa sio kuingiza. Kwa hivyo, ina maana hakuna mkakati mzuri wa kuhakikisha sisi tusiibiwe. Hata

tukiibiwa wao nafikiri wanaweza kufurahia kwa sababu wanafaidika wanapotoa nje ya nchi.

Lakini suala la kwamba wanatumia hizi karafuu za Zanzibar kubandika nembo kama ni karafuu iliyotoka Kenya hilo sina uhakika nalo nitajibu kwa maandishi.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuweka Haki na Wajibu wa Serikali katika Kesi za Madai na Utaratibu wa Mwenendo wa Madai dhidi ya Serikali na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa wasaa wa kuja kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, Mswada wa Sheria ya Kuweka Haki na Wajibu wa Serikali katika Kesi za Madai na Utaratibu wa Mwenendo wa Madai dhidi ya Serikali na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, sina budi kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati yetu ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmin, pamoja na Naibu Mwenyekiti wake na Wajumbe wote wa kamati. Kwa kweli Mhe. Spika, tumefanyakazi nzuri sana na tumeshirikiana vizuri kuupitia mswada kifungu kwa kifungu. Michango yao na marekebisho yao imesaidia sana kufanya marekebisho ambayo yameshasambazwa na takriban wajumbe wengi wameshayapata.

Mhe. Spika, kama tulivyoona kwenye semina yetu ya jana, huu mswada sio mgumu lakini sio rahisi, unataka ufahamu tu. Naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana wewe kwanza mwenyewe Mhe. Spika na wajumbe wote kwa kushirikiana jana kwenye semina yetu ambayo nafikiri ilikwenda vizuri sana.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa na sababu hasa ya mswada huu ni kuweka utaratibu maalum wa mwenendo wa madai dhidi ya serikali. Madai yote dhidi ya serikali sasa tunayaelekeza katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Mwanasheria Mkuu mwenyewe ndiye atakayebeba haya madai yote ya serikali katika mawizara na sehemu mbali mbali. Tofauti na zamani ambapo tulikuwa tunamsimamisha Katibu Mkuu na ikiwa hakuja basi tena mashtaka yanaendelezwa dhidi yake. Sasa tunarekebisha vifungu kuweka kwamba Afisi ya Mwanasheria Mkuu ndio hasa itakayobeba dhima au Afisa ambaye

atahusika moja kwa moja, ambaye atateuliwa na mwenyewe Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, madhumuni mengine makubwa ya sheria hii ni kusaidia kuweka utaratibu kwa mtu mwenye madai sugu serikalini afanywe nini. Kwa sababu kumekuwa na mienendo kwamba mtu anakimbilia mahakamani baada ya kuona kishachoka madai yake, siku ya kwanza, ya pili na ya tatu mpaka tena anakwenda mahakamani na mahakama wanasema kwamba shika mali ya serikali iuze. Sasa hatusemi kwamba serikali isidaiwe, serikali inadaiwa na itashtakiwa lakini kwa utaratibu maalum. Jambo hili naomba kusisitiza sana hatukatai kuwa madai serikalini yapo na yataendelea kudaiwa na tunaweka utaratibu huu ili tuweze kurahisisha kila mtu apate haki yake.

Mhe. Spika, kulikuwa na Waheshimiwa Wajumbe ambao sipendi kuwataja, walikuwa ni watetezi wazuri sana wa utawala bora hasa katika mwenendo kama huu. Isiwe maana yake tunaipendelea serikali dhidi ya watu wake. Nafikiri hili ni suala zuri sana na tumelizingatia sana Mhe. Spika, katika majadiliano yetu ndani ya kamati, tumefanya marekebisho ambayo naamini kabisa yataweka mustakabali mzuri mtu anapoidai serikali achukue hatua gani na nini *role* ya mahakama. Hatupendi kwamba tunaiingilia mahakama kama mhimili mmoja wa nchi yetu katika utendaji wa kazi zake. Lakini tunahisi kwamba kuna mambo ni lazima twende sambamba kama huku serikali na kule kama ni mahakama.

Mhe. Spika, mswada huu hapa kwetu ni mgeni lakini katika nchi za kilimwengu si mgeni. Takriban nchi za *Commonwealth,* hata jirani zetu au ndani ya Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzaniza, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari umo mswada huu na umeshaanza kutekelezwa, Ghana, Uingereza yenyewe na nchi mbali mbali kama Malaysia. Kwa hivyo, niseme kuwa sisi tumechelewa kidogo lakini "chelewa ufike". Tumeona hatimaye umuhimu wa suala hili na ninaamini litatusaidia kwenye utendaji wetu katika kazi zetu za serikali za kila siku. Pia kuwawekea njia nzuri wale ambao wanaidai serikali wafanye nini.

Mhe. Spika, kwa jumla mswada huu una vifungu 25 na ni imani yangu Waheshimiwa Wajumbe hata ile tafsiri ya Kiingereza wameshaipata katika mswada mkubwa, basi watajaribu kwenda sambamba na wa Kiswahili ili kupata uelewa mzuri.

Mhe. Spika, sehemu ya kwanza ya mswada huu unazungumzia utangulizi wa sheria. Sehemu hii inajumuisha kifungu cha kwanza na cha pili, ambapo kifungu cha kwanza kinaelekeza jina la sheria yenyewe pamoja na muda wa

kuanza kutumika kwa sheria hiyo. Kifungu cha pili kinatoa tafsiri na ufafanuzi wa baadhi ya maneno yatakayotumika ndani ya sheria hiyo.

Mhe. Spika, baadhi ya maneno hayo tumeyaweka na mengine tuliyasahau. Kwa mfano 'serikali', 'waziri', 'idara maalum' na 'afisa wa serikali' tuliyasahau haya, mengine tuliyasahau na mengine tuliyafanyia marekebisho.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ina mtizamo mzima wa sheria yenyewe. Sehemu hii ina jumla ya vifungu vitatu, ambavyo ni kifungu cha tatu, cha nne na cha tano. Kifungu cha tatu Mhe. Spika kinazungumzia kuhusu wajibu wa serikali katika mashtaka ya madai.

Kwanza, serikali itawajibika kwa mikataba, makubaliano ambayo hayajafikia hadhi ya mikataba, madai ya kuchukua kitu cha mtu na kukifanya chako, yaani *date new*, madhara na masuala mengineyo sawa na anavyowajibika mtu binafsi. Lalamiko lolote linalotokana na hayo linaweza kutiwa nguvu dhidi ya serikali, lakini kwa masharti ya sheria hii.

Pili, hakuna madai dhidi ya serikali yatakayokuwepo kwa madhara yanayotokana na tendo la mtumishi au wakala wa serikali mpaka tendo hilo liwe lingepelekea kuwepo kwa sababu ya madai dhidi ya mtumishi au wakala au mali zake.

Tatu, pale ambapo serikali inawajibika kisheria kutekeleza wajibu wake ambao pia ni wajibu kwa watu wengine wasiokuwa serikali wala afisa wake basi dhidi ya masharti ya sheria hii iwapo serikali itashindwa kutekeleza wajibu wake huo, itawajibika kwa dhima zote za madhara ambazo zingemuwajibikia mtu wa kawaida, yaani mtu binafsi.

Nne, pale ambapo kazi zozote zimepewa kwa afisa wa serikali kwa sheria yoyote na afisa huyo akafanya madhara katika kutekeleza kazi hiyo, basi dhima itakuwa ya serikali.

Tano, sheria yoyote inayoondoa dhima au kupunguza kiwango cha dhima kwa idara yoyote ya serikali au afisa wa serikali, kuhusiana na madhara yoyote yaliyofanywa na afisa wa idara, basi iwapo ni madai dhidi ya serikali chini ya kifungu hiki, sheria hiyo itatumika kwa serikali kama vile ambavyo ingetumika kuhusiana na idara au afisa.

Sita, hakuna madai yatakayofunguliwa dhidi ya serikali chini ya kifungu hiki kwa jambo lililofanywa na mtu yeyote kwa kutekeleza wajibu wake wa kimahakama aliopewa na wajibu walionao kuhusiana na utekelezaji wa amri ya mahakama.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 kinaelelezea juu ya kutumika kwa sheria kuhusu ulipaji wa fidia na michango. Pale ambapo serikali inawajibika kwa dhima yoyote kwa mujibu wa sehemu hii, sheria inayohusu fidia na michango itakayotumika kwa au dhidi ya serikali kama vile serikali ni mtu wa kawaida.

Mhe. Spika, kifungu cha 5 kinazungumzia kuhusu kubakisha yaliyofanywa chini ya sheria. Yaliyomo chini ya sheria hii hayaondoi uwezo wowote au mamlaka yoyote ambayo kama si sheria hii yangetekelezwa kwa mujibu wa uwezo wowote au mamlaka aliyopewa na serikali na sheria nyengine yoyote.

Sehemu ya tatu Mhe. Spika, inazungumzia masuala mazima ya mamlaka na utaratibu. Sehemu hii Mhe. Spika, yenye kichwa cha habari "mamlaka na utaratibu", inajumuisha vifungu vinane ambapo imeanza na kifungu cha 6 hadi kifungu cha 13.

Mhe. Spika, kifungu cha 6 kinahusu madai dhidi ya serikali. Kwanza bila kujali sharti jengine lolote la sheria hii, madai dhidi ya serikali yatafunguliwa kwa sharti la kifungu hiki.

Pili, hakuna madai yatakayofunguliwa dhidi ya serikali au afisa wa serikali kuhusiana na alichokifanya katika kutekeleza uwezo wake wa kiofisi, mpaka ipite miezi miwili baada ya mdai kutoa *notice* ya maandishi kwa Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Mwanasheria Mkuu, akieleza kiini cha madai, jina, maelezo na mahala anapoishi. Mdai na shufaa ni wadai na hati ya madai itakuwa na maelezo ya kuwa *notice* hiyo imetolewa.

Tatu, madai yote dhidi ya serikali baada ya muda wa *notice* kupita, yataletwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu na nakala ya hati ya madai itawasilishwa kwa wizara. Idara au afisa wa serikali anayetuhumiwa na kufanya kosa linalodaiwa.

Nne, madai yote dhidi ya serikali yatafunguliwa mahakama kuu au mahakama ya mkoa kwa mujibu wa taratibu za kimadai na kanuni za mahakama. Chini ya masharti ya sheria hii. Serikali haitatakiwa kulipa ada yoyote katika kufungua madai au kupata mwenendo wa shauri, hukumu au amri kutoka mahakamani.

Mhe. Spika, kifungu cha saba kinazungumzia masharti kuhusiana na Idara Maalum. Mhe. Spika, kwanza lolote linalofanywa au kuachwa kufanywa na mtumishi wa vikosi akiwa kazini, halitamfanya mtumishi huyo au serikali kuwajibika kwa madhara ya kusababisha kifo cha mtu mwengine, au kusababisha madhara kwa mtu mwengine. Iwapo kifo au jeraha limetokana na kuumia kwa mtu huyo mwengine wakati akiwa mtumishi wa Idara Maalum za serikali, ikiwa;

a) Wakati dhara hilo lilipotokea alikuwa kazini kama mtumishi wa vikosi au alikuwa katika ardhi, ndege au kwenye chombo ambacho wakati huo kikitumika kwa ajili ya Idara Maalum.
b) Waziri anayehusika na idara maalum amethibitisha kwamba madhara hayo yatachukuliwa kuwa kaumia akiwa kazini kwa ajili ya malipo ya fidia kuhusiana na ulemavu au kifo cha mtumishi huyo.

Pili, kifungu cha kwanza hakimuondolei dhima ya madhara mtumishi wa kikosi iwapo mahakama itaridhika kwamba kitendo kilicholeta madhara hakikuwa katika utekelezaji wa kazi zake kama mtumishi wa kikosi.

Tatu, hakuna madai yatakayofunguliwa dhidi ya serikali kwa kifo au maumivu kwa lolote litakalotokea kwa mtumishi wa Idara Maalum ya serikali, ikiwa;

a) ameumia kutokana na maumbile au hali ya ardhi yoyote, mahala popote, meli, ndege au chombo kama ilivyotangulia kuelezwa au kutokana na maumbile au hali ya zana yoyote au kitu kilichotolewa kwa ajili ya Idara Maalum.
b) Waziri anayehusika na Idara Maalum amethibitisha kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hiki.

Aidha, hakuna tendo lolote la Afisa wa Serikali litakalomfanya kuwa na dhima ya madhara kwa kifo au maumivu yaliyotokana na jambo lolote lililomsibu mtumishi wa Idara Maalum kwa mambo na hali zilizoelezwa hapo juu.

Nne, iwapo Waziri anayehusika na Idara Maalum ataridhika kwamba:-

a) Mtu huyo hakuwa kazini kama mtumishi wa Idara Maalum ya serikali au
b) Katika wakati huo ardhi yoyote mahala meli, ndege, chombo au vitu vyovyote vilikuwa au havikuwa vikitumika kwa ajili ya idara hizo. Anaweza kutoa hati ya kuthibitisha hivyo na hati hiyo ni ushahidi wa kutosha kwa yale yaliomo.

Mhe. Spika, kifungu cha 8 kinazungumzia madai ya kutaka kutangazwa mmiliki. Wizara ya Serikali inaweza kufungua madai ya kutaka kujua mmiliki, au kuwa sehemu ya mdawa kama vile mtu wa kawaida, bila kujali kwamba madai hayo yamefunguliwa na dalali wa mahakama au afisa mwengine.

Mhe. Spika, kifungu cha 9 kinazungumzia kufungua kesi ya serikali. Kwanza kwa kuzingatia masharti ya sheria nyenginezo, madai ya serikali yatafunguliwa na Mwanasheria Mkuu au mtu mwengine aliyeidhinishwa na Mwanasheria

Mkuu kutekeleza kufungua mashtaka hayo. Pili, madai dhidi ya serikali yatafunguliwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu.

Kifungu cha 10 Mhe. Spika, kinazungumzia masuala mazima ya kuhusu kuhamisha shauri. Iwapo kesi imefunguliwa na serikali au dhidi ya serikali katika mahakama ya mkoa na ombi kwa niaba ya serikali limefanywa mahakama kuu na iwapo kuna hati ya Mwanasheria Mkuu kuthibitisha kuwa madai hayo yana suala muhimu la kisheria au linaweza kuwa muongozo wa maamuzi ya kesi nyengine kama hizo au kwa sababu nyengine ya maana, basi shauri hilo litahamishiwa Mahakama Kuu.

Mhe. Spika, kifungu cha 11 kinazungumzia namna ya shufaa. Kwanza katika shauri lolote la au dhidi ya serikali, mahakama itakuwa na uwezo wa kutoa amri zote zilizo na uwezo nazo sawa na masharti ya watu binafsi, vyenginevyo kutoa shufaa inayostahiki kama inavyohitajika katika kesi.

Pili, iwapo katika madai dhidi ya serikali shufaa imeombwa na mtu ambaye inapaswa kutolewa kwa njia ya amri ya kuzuia; yaani *injunction* au utekelezaji wa jambo maalum *specific performance*, mahakama haitatoa amri ya kuzuia au kutoa amri ya utekelezaji wa jambo maalum na badala yake itatoa amri ya kutangaza haki ya wadawa.

Tatu, iwapo ni madai dhidi ya serikali ya kurejesha ardhi au mali nyengineyo, mahakama haitatoa amri ya kurejeshwa ardhi au kutolewa mali na badala yake itatoa amri ya kutangaza kwamba mdai anastahiki ardhi au mali au kushikilia mali hiyo.

Nne, mahakama haitatoa amri ya kuzuia au kutoa amri dhidi ya afisi au serikali iwapo kutolewa kwa amri hiyo ya kuzuia au kutolewa kwa amri hiyo kutaleta athari kwa serikali ambapo isingepaswa kutolewa katika madai dhidi ya serikali.

Mhe. Spika, kifungu cha 12 kinazungumzia gharama katika kesi ambayo serikali ni mdawa. Gharama za kesi pale ambapo serikali ni mdawa zitatolewa kama vile ni madai ya watu binafsi na mahakama itakuwa na uwezo wa kutoa amri ya kulipa gharama kwa serikali au dhidi ya serikali.

Kifungu cha 13 Mhe. Spika, kinazungumzia masuala mazima ya rufaa na kucheleweshwa kwa utekelezwaji wa hukumu. Kwa sharti la sheria hii, sheria yoyote inayohusu rufaa na ucheleweshwaji, utekelezwaji wa hukumu pamoja na marekebisho muhimu yatakayotumika katika mwenendo wa madai ya au dhidi ya serikali kama vile inavyotumika kwa madai baina ya watu binafsi.

Sehemu ya nne Mhe. Spika, inazungumzia masuala ya humu humu na utekelezaji. Sehemu hii inajumuisha vifungu vitatu kuanzia kifungu cha 14 hadi cha 16. kifungu cha 14 Mhe. Spika, kinaelezea masuala ya riba. Masharti ya sheria nyengineyo kuhusiana na riba iwapo amri ni kulipa fedha na malipo ya riba kwa gharama yatatumika kwa serikali kama yanavyotumika kwa kesi za watu binafsi.

Kifungu cha 15 kinazungumzia utekelezaji amri dhidi ya serikali. Kwanza iwapo amri imetolewa dhidi ya serikali au afisa wa serikali, ikiwa ni pamoja na amri ya gharama afisa husika wa mahakama baada ya kuombwa na mdai au wakala baada ya kumalizika siku 21 toka kutolewa amri hiyo, atatoa hati kwa mtu huyo yenye maelezo ya amri hiyo. Isipokuwa kwamba iwapo mahakama itaamuru hivyo, hati pekee itatolewa kuhusiana na gharama kama zipo inayoamuru kulipwa muombaji.

Pili, iwapo amri ni kwa malipo ya fedha kwa ajili ya hasara au shufaa nyenginezo au gharama, hati itaeleza kiwango cha kulipwa na Katibu Mkuu anayehusika na fedha au afisa wa serikali kama inavyoweza kuwa, atamlipa mtu anayestahiki au kwa wakili wake kiwango kinachooneshwa katika hati pamoja na riba kama ipo inayomstahikia kisheria.

Tatu, iwapo kuna rufaa, mahakama ikiona inafaa inaweza kusitisha amri hiyo ya kulipa malipo yote au sehemu ya malipo yanayostahiki ili kusubiri rufaa.

Nne, isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki, hakuna utekelezaji wa hukumu au kama taji au hatua kama hizo zitakazotolewa na mahakama yoyote katika kulazimisha serikali kulipa fedha au gharama zilizotajwa katika kifungu hiki. Hakuna mtu atakayewajibika binafsi chini ya amri yoyote ya serikali au idara ya serikali au afisa wake chini ya amri hiyo ya kulipa.

Kifungu cha 5 Mhe. Spika, kitatumika kuhusiana na mashauri yanayosubiri hukumu au amri zilizotolewa kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii, yaani *retrospective effect,* lakini hazijatekelezwa na mashauri yatafunguliwa baadae.

Mhe. Spika, kifungu cha 6 kinazungumzia utekelezaji kwa serikali, chini ya masharti ya sheria hii, amri yoyote iliyotolewa kwa serikali dhidi ya mtu mwengine yoyote katika masharti ya madai ambapo serikali ni mdawa, itatekelezwa kama katika madai mengine ya watu binafsi. Masharti ya kifungu hiki yatatumika kwa masharti yaliopo na yatakayokuja baadae. Masharti haya hayatoathiri utaratibu ambao ulikuwepo kabla ya sheria hii kwa utekelezaji wa amri zilizotolewa kwa faida ya serikali kwa kulipwa faini au adhabu yoyote au kufilisi mali.

Mhe. Spika, sehemu ya tano masharti ya jumla. Sehemu hii inajumuisha kifungu cha 17 hadi cha 23. Mhe. Spika, kifungu cha 17 kinazungumzia utoaji hati.

Kwanza katika shauri lolote la madai ambalo serikali ni mdawa katika mahakama kuu au mahakama ya mkoa, serikali inaweza kutakiwa na mahakama kuwasilisha nyaraka kwa uchunguzi. Pia serikali inaweza kutakiwa kujibu maswali yatakayoulizwa.

Pili, kifungu hiki hakitatumika kuathiri sheria nyengineyo au taratibu za kisheria ambazo zinataka kutotolewa kwa nyaraka yoyote au kutoa jibu kwa msingi kwamba kutaathiri maslahi ya taifa.

Kifungu cha 18 kinazungumzia haki ya serikali kuegemea sheria iliopo. Sheria hii haitaathiri haki ya serikali kutumia fursa na masharti ya sheria nyengineyo yoyote, ingawa hazikutajwa humu na imeelezwa wazi kuwa sharti lolote la sheria linaweza kutumiwa na serikali kama vile inavyoweza kutumiwa kwa madai ya watu binafsi.

Kifungu cha 19 Mhe. Spika, kinazungumzia kikomo cha madai. Hakuna katika sheria hii kinachozuia serikali kuegemea katika sheria yoyote inayohusu kikomo cha muda wa kuleta mashauri.

Mhe. Spika, kifungu cha 20 *set off* ndani ya madai kwa kurejesha kodi. Mtu hatastahiki kujikatizia deni katika kujilipiza deni au madai ndani ya madai anayoidai serikali kutokana na kodi au adhabu anazopaswa kuilipa serikali.

Kifungu cha 21 Mhe. Spika, kinazungumzia mashauri yanayoendelea. Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 15 cha sheria hii, masharti ya sheria hii hayatoathiri mashauri yaliyofunguliwa kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii.

Kifungu cha 22 kinaelezea kuhusu kufutwa na kufanyiwa marekebisho kwa baadhi ya vifungu vya sheria zilizopo.

Kifungu cha 23 kinazungumzia kuhusu bakizo. Sheria hii haitoiingiza serikali katika dhima kubwa kwa matendo ya mkandarasi wa serikali anayejitegemea zaidi ya zile dhima ambazo ingeiwajibikia serikali kama ingekuwa matendo hayo ni ya mtu wa kawaida. Pia haitoathiri sheria yoyote kanuni za ushahidi au dhana ya kuwa inabanwa na sheria yoyote.

Sheria hii Mhe. Spika, haitotumika kuzuia uwezo wa mahakama kutoa shufaa kwa njia ya kuamuru kutekeleza wajibu wa sheria, yaani *mandamus* katika

mashauri ambayo shufaa imetolewa kabla ya kutumika kwa sheria hii, bila kujali kwamba kwa sababu za masharti ya sheria hii kuna shufaa nyengineyo.

Mhe. Spika, kifungu cha 24 kinazungumzia kanuni. Waziri amepewa uwezo wa kutunga kanuni ili kuifanya sheria hii itekelezeke.

Kifungu cha 25 Mhe. Spika, kinaelezea juu ya uwezo utakaokuwanao sheria hii iwapo itakuwa imeingiliana na sheria nyengine yoyote.

Mhe. Spika, kwa muhtasari mswada wetu umezungumzia vifungu hivyo nilivyovitaja na nimejitahidi kuvichambua ili tupate kama muongozo wa michangio yetu. Naamini kabisa kwamba semina ya jana imetusaidia sana kama nilivyosema kupata uelewa mzuri.

Ni matumainio yangu Mhe. Spika, kuwa Waheshimiwa Wajumbe watauchangia mswada huu na hatimaye kuupitisha kwa mustakabali wa nchi yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, ifuatayo ni hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Haki na Wajibu wa Serikali katika Kesi za Madai na Utaratibu wa Mwenendo wa Madai dhidi ya Serikali na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataallah kwa kutujaalia neema zake za kuendelea kuwa hai tukiwa wazima wa afya njema.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo kutoa maoni kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi yanayohusiana na mswada huu wa Sheria ya Kuweka Haki na Wajibu na Utaratibu wa Mwenendo wa Madai dhidi ya Serikali na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Aidha, niruhusu nitumie nafasi hii ulionipa kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mashirikiano yao ya dhati kabisa waliyonipa, kwa muda wote tulipokuwa tunafanya kazi ulizotukabidhi Mhe. Spika, ukiwemo mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, naomba niwashukuru waheshimiwa hao kwa kuwataja majina:

1. Mhe. Ali Abdalla Ali - Makamo Mwenyekiti
2. Mhe. Assaa Othman Hamad - Mjumbe

3. Mhe. Ashura Abeid Faraji - Mjumbe
4. Mhe. Said Khelef Ali - Mjumbe
5. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Mwajuma Faki Mdachi - Mjumbe
7. Mhe. Juma Duni Haji - Mjumbe
8. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mjumbe
9. Mhe. Rashid Seif Suleiman - Mjumbe
10. Ndg. Amour Moh'd Amour - Katibu
11. Ndg. Maryam Hussein Rajab - Katibu

Mhe. Spika, vile vile nitakuwa sijamtendea haki nisipomshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi kwa uwasilishaji wake mzuri wa mswada huu. Pia kwa kazi nzuri iliyofanywa na watendaji wake iliyohusiana na matayarisho yaliyomuwezesha kuufikisha mswada huu mbele ya Baraza letu tukufu *(Makofi)*.

Bila ya shaka watendaji wake hao walioongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wengineo wote kwa namna moja au nyengine wamekuwa washauri wazuri kwake yeye Mhe. Waziri binafsi, pia wametoa mashirikiano mazuri na maelekezo kwa kamati yetu muda wote tulipokuwa tunajadili na kuupitia Mswada huu. Tunawashukuru sana.

Mhe. Spika, mbali na mashirikiano mazuri na maelekezo kwa kamati yetu, Wajumbe wa Baraza lako tukufu wamepata fursa ya kupata taaluma kupitia semina iliyotayarishwa na Wizara. Ni dhahiri kwamba taaluma hiyo imewasaidia sana Waheshimiwa Wajumbe kuuelewa mswada huu na tunatarajia sana michango yao.

Serikali kwa maana yake ni watu, ni chombo kinachofanya kazi ya watu, kinacholinda na kutunza mali za watu na kinafanya mambo yake yote kwa niaba ya watu. Kwa tafsiri hiyo nyepesi tunasema kwamba chochote kile tunachojua kwamba ama kinafanywa na serikali au kinamilikiwa nayo maana yake ni cha watu kwa maana ya umma.

Mhe. Spika, Mswada huu una madhumuni makuu ya msingi matatu ambayo ni haya yafuatayo:-

- Kubainisha haki na wajibu wa serikali katika suala zima la madai,
- Kuweka utaratibu wa madai dhidi ya serikali na
- Kuhami mali za serikali katika utekelezaji wa hukumu endapo kutatokea kosa la kufikisha hatua hiyo.

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba mali za serikali zinatunzwa na kuendelezwa kupitia Taasisi mbali mbali zikiwemo Idara na Mashirika ya Serikali, kwa maana hiyo Mashirika hayo yanaweza katika utekelezaji wa shughuli zake kuingia katika mikataba mbali mbali, kushtaki na kushtakiwa na mambo mengine ambayo wakati mwengine pia hufanywa na mtu binafsi. Kifungu cha 3 cha Mswada huu kimeelekeza hayo.

Katika utekelezaji wa majukumu haya ya kila siku yanaweza wakati mwengine yakaisababishia serikali kushtakiwa. Hivyo katika kutekeleza hukumu ya madai hayo dhidi yake yanaweza kuipelekea mahakama kutoa amri ya kuuzwa kwa mali za serikali, ili kulipa fidia ya madai hayo.

Mhe. Spika, kwa kutoa mwanya huo ndani ya sheria kunaweza kuipeleka serikali pahala pabaya, kwani kwa uzembe wa baadhi ya watendaji wake mali nyingi za serikali zinaweza kupotea tena nyengine zinaweza kuwa nyeti, kwa maana hiyo ni muhimu sana kuwa na sheria madhubuti inayoilinda Serikali na kadhia hii ya uuzwaji wa mali zake. Hivyo mswada huu katika Sehemu ya Tatu, vifungu vya 6 hadi 13 vinaelekeza Mamlaka na utaratibu wa madai dhidi ya serikali .

Mswada wa sheria hii inayoombwa kutungwa itayakinga haya na itaelekeza haki na wajibu ulio mzuri kwa serikali, kuweza kulipa madai hayo bila ya kuwa na aibu hiyo.

Kwa maana hiyo, Mhe. Spika katika Sehemu ya Nne ya Mswada huu inayohusiana na hukumu na utekelezaji kuna pendekezo la nyongeza ya kijifungu cha 15(6) kinachompa nafasi Waziri anayehusika kutunga kanuni itakayoelezea utaratibu wa malipo ya utekelezaji unaohusu kijifungu cha 15(4), ambacho kinahusiana na namna ambavyo serikali kulipa madai hayo bila ya kuhusisha ukamataji au uuzaji wa mali zake.

Mhe. Spika, mswada huu haukuzingatia tu kuzuia mali za serikali zisihusishwe na malipo ya madai, pia unaangalia na upande wa pili wa shilingi, yaani haki za wale wanaoidai serikali nazo zinalidwa vipi.

Jambo jengine lililozingatiwa na mswada huu ni migongano na sheria nyengine, ndio maana kifungu cha 22 cha mswada huu kimefuta vifungu vya 59, 60, 61 na 62 vya Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura 8. Halikadhalika, umefanya marekebisho ya kifungu cha 13 cha Sheria ya Mahakama ya Ardhi Nam. 7 ya 1994 na kuongeza maneno mwishoni mwa ibara (r).

Kamati yetu wakati wa kujadili ilikuwa makini juu ya mapendekezo haya ya mswada na kuzingatia kwa kiwango kikubwa umuhimu wa sifa ya serikali

kubakia kama serikali, lakini haki za madai nazo zipatikane bila ya vikwazo vinavyopelekea suala la kukaza hukumu.

Mhe. Spika, kwa kuona umuhimu huo na baada ya mashauriano na Mhe. Waziri aliwasilisha mswada huu mbele ya kamati kukiwa na marekebisho kidogo kama tulivyoyaonesha kwenye karatasi za marekebisho, kamati iliunga mkono mswada huo uwasilishwe mbele ya Baraza lako tukufu.
Kamati inachoiomba serikali ni kuelewa kwamba suala la kuwepo kwa sheria ni muhimu, lakini kusimamia utekelezaji wake ni muhimu zaidi. Hivyo jambo la kusimamia sheria zote tunazozitunga ndio maana halisi ya kuwa na sheria na siyo wingi wa vitabu vya sheria. Ni bora tuwe na sheria chache ambazo zitasimamiwa kikweli kweli badala ya kuwa na wingi wa sheria zisizosimamiwa.

Mhe. Spika, baada ya maoni hayo ya Kamati ya Fedha na Uchumi, yaani kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni naunga mkono mswada huu na kuwaomba wajumbe wenzangu nao kuunga mkono hoja hii.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha *(Makofi).*

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Kny: Waziri Kivuli Wizara ya Fedha na Uchumi) Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote tuliomo humu Barazani, kuwa wazima na wenye afya na kuweza kuhudhuria katika kikao hiki muhimu.

Pili Mhe. Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, adhimu na adimu ya kutowa mawazo yetu ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mswada huu. Naamini kabisa kuwa mawazo yetu haya yatasaidia kabisa katika kuimarisha sheria hii, ambayo ndio mategemeo makubwa kwa wananchi ambao kwa njia moja au nyengine ni wadaawa na serikali.

Mhe. Spika, utaratibu wa sasa wa mwananchi kuidai au kudaiwa na serikali una kasoro nyingi, zaidi utaratibu huo ni wa zamani sana kama ulivyo elezewa katika vifungu vya 59 hadi 62 vya Sheria ya Mwenendo wa Madai , Sura ya 8 ya Sheria za Zanzibar. Vile vile utaratibu wa madai hayo ambao unatumika hapa Zanzibar, unatofautiana sana na utaratibu unao tumika katika nchi nyingi za Jumuiya ya Madola ambapo Zanzibar, kwa kupitia Tanzania ni mwanachama.

Kinachohitajika, kwa sisi Wazanzibari kujito katika kisiwa cha upweke kwa kuwa pamoja na wenzetu, ambao wamepiga hatua katika suala hili. Kwa maana hiyo Mhe. Spika Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni yake kama ifuatavyo:-

1. Mswada kwa jinsi ulivyo inaonekana kama unasimamiwa na waziri anaeshughulikia mambo ya fedha, lakini ni kwa nini katika kifungu cha pili kinachohusiana na tafsiri waziri imetafsiriwa kuwa ni waziri wa mambo ya sheria.

2. Kifungu cha 11 cha sheria hii nacho kinahitaji marekebisho. Hatuoni sababu ni kwa nini Mahakama ishindwe kutoa hukumu, ikiwa serikali imeshindwa katika masuala yanayohusu ardhi. Inaposema kuwa mdai anastahili ardhi hiyo, ina maana kuwa serikali inaweza kupiga chenga kwa kuona kwamba haki inayo bishaniwa ni kweli ni ya mdai. Hivyo hatuoni kuwa kwa utaratibu huu, wanachi wataona basi ni bora kusema kuwa serikali haitoshtakiwa.

3. Kifungu cha 15 na kifungu cha 16 cha mswaada huu navyo vinahitaji kutizamwa upya. Katika wakati huu wa haki za binaadamu kutiliwa maanani sana, haitowezekana kumtesa mwanachi kwa kusubiri ukiritimba wa utawala wa miezi kiasi tisa hadi mwaka, ndio Katibu Mkuu akitaka afanye malipo kwa mwananchi aliyepata hukumu dhidi ya serikali.

   Lakini ikiwa ni serikali iliopata hukumu hiyo dhidi ya mwananchi, basi serikali ipewe fidia yake mara moja. Mhe. Spika, hii itakuwa ni maonevu makubwa kwa mwananchi huyo.

4. Mhe. Spika, utaratibu wa sheria ulivyo katika karne hii, kwa misingi ile ile ya uwajibikaji kiutawala, basi hairuhusiwi na hakuna sheria itakayo tumika kuanzia nyuma ya pale sheria hiyo ilipo tungwa, yaani *retrospective application*.

   Sasa kifungu cha 21 kinaonesha wazi kuwa kesi zote zilizopo hivi sasa, ambazo zinaendelea hata kama kesi ilianza kabla ya kupitishwa sheria hii, basi hukumu yake itatolewa kwa mujibu wa sheria hii. Mhe. Spika, utaratibu huu haukubaliki na tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atupe ufafanuzi wa kutosha kuhusu kasoro hii kubwa ya kisheria.

5. Mhe. Spika, utaratibu uliofuatwa kuhusu urekebishaji wa sheria nao si utaratibu mzuri. Kwa nini tusifuate mfumo mzuri unaotumiwa na majirani zetu wengi wa kuwa na *Miscellaneous Amendment Act*, ambapo kila mtu ataona kilichofanywa na kutakiwa akifuate. Hii inahusisha hasa kifungu cha 13 cha

sheria ya Mahakama ya Ardhi, ambapo kifungu hicho cha 13 kimefutwa na Sheria hii ya Madai ya au Madai dhidi ya Serikali

Mhe. Spika, unapoangalia sheria za wenzetu, ambao nao walirithi mfumo huo huo wa kikoloni ambao kwa sasa sote tuko chini ya mwamvuli wa Jumuiya ya Madola (*Commonwealth*), basi sheria zao zimewajali ijapokuwa kwa kiwango kidogo tu cha haki watu wao au kwa maana pana wananchi wao. Sheria ambazo tumezipitia ni pamoja na ya Tanzania, Ghana, Uiengereza na Kenya.

Mhe. Spika, kwa utaratibu uliowekwa ndani ya sheria hii, basi ni dhahiri kuwa wananchi wetu watatishika hata kuwekeana mikataba na serikali, kwa kuogopa kucheleweshwa malipo yao hata kama utapeleka shauri lako hapo mahakani. Matokeo yake ni kusimamisha huduma muhimu zinazotolewa kwa serikali kama vile chakula hospitalini, vyakula vinavyopelekwa dakhalia na sehemu kama hizo.

Mhe. Spika, naomba kumalizia kwa kusema kuwa mswada huu utakuwa mzuri na wenye manufaa makubwa kwa wote serikali na mwananchi wa kawaida, ikiwa maelezo tuliyoyatoa basi yatazingatiwa na kufanyiwa marekebisho yanayofaa.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa nakushukuru na naomba kuwasilisha *(Makofi)*.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu mdogo. Kwa kuwa mimi ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, mswada huu tuliupitia na tuliweza kufanya marekebisho mengi katika kikao. Kwa hivyo, napenda kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, kwa sababu walikuwa *free* na kutuelewa vile ambavyo tulichangia.

Kabla sijaingia kwenye sehemu tatu za mswada huu ambazo napenda kuzisisitiza, Mhe. Spika kwa ruhusa yako napenda kutoa utangulizi ufuatao.

Mhe. Spika, pakiwa na watu wawili basi kuna misemo mingi imepita katika karne na karne, ili watu wawili wale waweze kuishi vizuri. Miongoni mwa misemo hiyo mmoja unaosema hivi “ukitaka uheshimiwe na wewe ujiheshimu”.

Kwa kweli hili ni jambo zuri tena ni la muhimu sana, kulinda mali za serikali, ingawa mimi binafsi Mhe. Spika mara nyingi katika Baraza lako hili hupendekeza kwamba tuondokane na kutaja masuala ya mambo ya mali ya au

fedha za serikali na badala yake tutumie mali ya umma. Kwa sababu mara nyingi serikali inachukuliwa ni wale viongozi walioko kwenye madaraka.

Kutokana na hali hiyo hata wao wenyewe hujichukulia hivyo hivyo, ndio maana niliposema ukitaka kuheshimiwa kwanza ujiheshimu wewe mwenyewe. Kwa sababu wanajichukulia hivyo basi hutumia ovyo mali za serikali na wakati mwengine hutiwa mikataba ambayo inayojulikana si sahihi na kuisababishia serikali gharama kubwa, lakini yule afisa aliyesababisha vile anabaki kuwa salama.

Lakini wakati mwengine hata sera zetu Mhe. Spika hatuzifuati na badala yake husababisha hiyo mikataba mibovu. Kwa mfano, tunacho kituo tulichokiweka cha Uwekezaji na hapa kuna dalili ya kuanza mikataba baina ya sisi na wawekezaji mbali mbali na kituo hiki kinaitwa *ZIPA*. Hivi karibuni kilitangaziwa kiwe ni *One Stop Centre*, yaani ni pahala unapofikia muwekezaji na kumaliza shughuli zake zote na baada ya hapo anaendelea na shughuli za uwekezaji kama alivyopanga mwenyewe kwenye *programs* zake pamoja na kufuata sheria za nchi.

Lakini matokeo yake kimebadilika sasa na kuwa *Fully Stop Centre* badala ya *One Stop Centre*, maana yake ukifika hapo ndio umekwama. Kwa hivyo, badala ya *One Stop Centre* kimekuwa ni *Fully Stop Centre*. Kwa kweli hali hii inaleta matatizo, kwa sababu tayari hivi sasa wapo wanaodai haki yao katika ardhi pamoja na mambo mengine, kwa kuwa wamefika pale na wala hawakushughulikiwa kama walivyoambiwa kule nyuma.

Mhe. Spika, masuala haya ushahidi upo wa kutosha, kwa sababu ripoti tuliyopewa juzi katika wiki mbili zilizopita ilionesha dalili hiyo kwamba Kituo cha Uwekezaji hakiko katika hali nzuri.

Kwa maana hiyo, Mhe. Spika pamoja na serikali kujing'ang'anua kwamba haitaki kushtakiwa ovyo, maana hata ikifika hali ya kushtakiwa basi ishtakiwe kwa jambo ambalo ni zito na wala hakuna budi. Kwa hivyo, kama haitaki kushtakiwa ovyo, basi serikali inabidi ibadilishe mwenendo wake na iwajibike zaidi. Kwa mfano, kuanzia mawaziri, watendaji wakuu wawajibike zaidi.
Vile vile masuala yanayohusiana na rushwa au nipe changu kabisa, haya ni mambo ambayo lazima tuyapige vita vyenginevyo sheria hii itakuwa haileti maana, kwa sababu sheria inatungwa ili isivunjwe. Kwa sababu wataalamu wanasema siku zote sheria inatungwa ili isivunjwe, lakini unapotunga sheria na kuhakikisha kwamba sheria hii inavunjwa, basi ile itakuwa haina maana tokea siku ile ya mwanzo.

Kwa kweli sisi tuko nyuma katika kuleta sheria hii na serikali imefika wakati kushtakiwa na kutaka kuuzwa hata serikali yenyewe.

Nadhani tujiulize pamoja na sheria hii tuliyoiweka, kuna mabadiliko gani ya kisera yaliyofanyika ambayo yatapelekea kukosekana kwa mikataba mibovu na itakayoitia serikali katika mashtaka. Wananchi wa nchi hii ni wavumilivu sana.

Mhe. Spika, jana wakati tulipokuwa tukipitia mswada huu kwenye semina tuliambiwa kwamba tukiachilia mbali madai ya kawaida, ambayo inaweza kuwa ni *property* au umekopesha kitu *physical*.

Lakini tunaweza kuishtaki serikali kwa kutotimiza wajibu wake tu, sasa tujaaliye Mhe. Spika watu laki mbili walioungiwa umeme, wangeamua kuishtaki serikali kwa kuwakosesha umeme miezi mitatu serikali ingelipa kiasi gain? Kwa kweli watu ni wavumilivu sana. Kwa sababu ule ni wajibu wa serikali kusambaza umeme kwa wale watu, lakini wameshindwa kwa muda wa miezi mitatu.

Kwa maana hiyo, nasema mambo haya tusiyachukulie kwa udogo wake, na tuyachukulie na ule ukubwa wake. Kwa hivyo, sheria hii tunaposema ni nzuri kwa kuwa inalinda mali ya serikali ambayo ni mali ya kila mtu. Vile vile inahitaji *complimentary executions*, yaani kuwe na mambo sambamba na haya yanatekelezwa.

Kwa mfano, serikali ijipange vizuri na kuhakikisha kwamba watendaji wa serikali wanatekeleza wajibu wao. Pia chini ya Waziri Kiongozi kuwa Mawaziri wanatekeleza wajibu wao na wala mikataba ovyo haitiwi, lakini bila ya kwenda na mambo mengine sambamba, basi sheria hii itakuwa haina maana. Kwa sababu mambo madogo madogo yanayoshtakiwa serikali ni aibu, kama vile serikali haikulipa hiki na kile. Kwa nini tunakopa masikini, nadhani kama sisi tunataka kukopa basi tukawakope wale matajiri.

Mhe. Spika, sijawahi kusikia hapa hata siku moja kwamba Marekani au Uingereza wala Abudhabi imekuja hapa na kuishtaki serikali, lakini ukisikia serikali inashtakiwa na mtu ambaye hana hata dola bilioni moja hana kwenye benki. Nadhani tusikope masikini na tunapotaka kukopa basi kukope matajiri na wala hawawezi kutushtaki.

Kwa hivyo, hata wale watu wa kukopa serikali ichague na isiende kukopa masikini, kwa sababu atakushtaki tu kwani hana kitu na yeye anataka kupata kutoka kwako. Kwa mfano, kule mitaani basi masikini kwa masikini hatukopeshani isipokuwa tunasema tunaridhiana tu, maana yake siku ya pili

unamrejeshea mwenyewe. Lakini ikiwa utamkopa kweli basi hata ukivaa shati atasema shati ile fedha zangu zimo ambazo amechukua.

Kwa ufupi katika utanguzili huu nakusudia kwamba serikali yenyewe ijipange na iwe na mambo yanayokwenda sambamba kwenye mienendo yake, ili sheria hii iwe na maana. Japo hilo la mwanzo.

Pili kuna zile kesi ambazo zipo mahakamani na tunajua zinaletwa mahakamani, kwa sababu tumekubaliana kwenye kamati Mhe. Waziri atunge Kanuni kama alivyosema Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi) kwenye kifungu cha 13(4) kwamba Mhe. Waziri atunge Kanuni itayoweka wazi utaratibu gani wa kufuatilia wale wadai kama serikali ni mdaiwa. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji hapa alisema kwamba sheria hii ni *retrospective* kwa maana inakusanya na yale mambo ya nyuma.

Sasa yeye ameuliza swali na mimi naongeza kwamba na hicho kifungu cha kanuni basi ki-*include* na hayo mambo ambayo tayari yapo kwenye meza, yaani *special case* kwa mambo hayo, yatakuwa *controled* kwa muda gani kwa sababu hatuwezi tena kwenda hivi na hiyo riba yenyewe iko *compound entrest*, kwa hivyo kila ukikaa unazidishiwa.

Jambo la tatu nizungumzie baadhi ya vifungu ambavyo napenda niongezee chochote kwa ajili ya kuangaliwa zaidi. Kifungu cha 11(4) cha mswada huu Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 11(4) kinachosema hivi:

> "Mahakama katika shauri lolote haitotoa amri ya kuzuia au kutoa amri yoyote dhidi ya afisi wa serikali iwapo kutolewa kwa amri hiyo kutaleta athari kwa serikali ambapo isingepaswa kutolewa katika madai dhidi ya serikali".

Mhe. Spika, wakati tulipokuwa tukijadili wataalamu walisema kwamba hii inazuia ile serikali kupewa *injection order* ya kuzuia jambo lake. Nadhani kifungu hiki kina matatizo, kwa sababu *injection order* ya kawaida ya kuzuia jambo inakuwa *unlimited time* mpaka jambo lile litakapotatuliwa, lakini kwa serikali ingefanywa na wakati maalum, yaani *time limit*.

Lakini bado uwezo wa mahakama wa kuzuia jambo japo kuwa dhidi ya serikali ungekuwepo, isipokuwa itakachorekebishwa ni wakati maalum tu, badala ya kuwekwa kwa nini. Kwa sababu mahakama inao uwezo wa kuzuia jambo lililopelekwa na mdai kwa muda usiozidi mwezi mmoja kwa mfano.

Sasa hali ile itawapa fursa serikali kulishughulikia suala lile kwa haraka ndani ya mwezi mmoja, lakini kusema mahakama iondolewe kabisa uwezo wake wa kuzuia jambo wakati mtu ameshanyang'anywa ardhi yake au kipindi kile *bulldozers* zipo zinasuburi mtu akisema hivi na vile huku tayari nyumba yake imeshaondoka, sasa ikiwa yeye anayo haki na nyumba yake imeshaondoka sasa itatathminiwa na nani? Katika mwezi mmoja ule hata kama ingekuwa itakuwa na haki ya kwamba ile nyumba iondoke lakini ndani ya mwezi mmoja ule basi ile nyumba itapata kutathminiwa. Lakini *bulldozer* ikishakuiondosha itatathminiwa na nani?

Kwa hivyo, mimi nahisi ilivyo hasa hii *junction order* kwa upande wa serikali iwepo lakini iwepo kwa muda maalum, tofauti na hii *junction order* ambayo inatolewa kwa mtu mwengine, hii italinda haki ya mtu tofauti na hizo nyengine. Kwa hivyo, Mahakama nahisi mimi katika kifungu hiki isipokonywe uwezo wa kuzuia jambo kwa sababu wakati mwengine inakuwa kama hivyo nilivyosema kama inatakiwa thamani ya vitu au mali iliyokuwepo pale, lakini ikishakuondolewa huwa haipatikani. Kwa hivyo, mwenyewe akishaona asubuhi ma-*bulldozer* yanakusanyika anakwenda Mahakamani basi serikali ipewe mwezi mmoja kwa sababu ni serikali.

Mhe. Spika, ndio maana hapa tukasema kwamba na sisi tunafanya makosa kwa sababu tukisema serikali na yule aliyepeleka *junction order* mara nyingi na yeye anakuwa yumo. Kwa hivyo, ina maana yeye amezuiwa na ile serikali lakini amezuiwa ndani ya haki yake. Kwa hivyo, amezuia haki mbili, amezuiwa na serikali ambayo yeye mwenyewe yumo, pia amezuiwa kwa ile mali yake ambayo yeye mwenyewe ndiye mmilikaji.

Mhe. Spika, jambo langu mimi la mwisho ni kwamba utekelezaji wa sheria hii unatakiwa uende na misingi mitatu mikubwa. Kwanza utawala bora, jambo la pili ni uwazi na jambo la tatu ni uadilifu. Mhe. Spika, tukiweza kutekeleza sheria hii katika mambo matatu hayo kila mmoja atatuunga mkono atatujua kwamba kweli tulikuwa nyuma na tumekuja kulingana na wenzetu lakini tumekusudia kutokuvunja haki za watu wengine za utawala bora, uwazi na uadilifu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia na mimi fursa hii kuchangia machache sana katika mswada huu wenye utata juu ya sheria hii.

Mhe. Spika, mimi kabla ya kuchangia kwenye mswada wenyewe kwanza nilijibebesha dhima kwa sababu mimi sio mtaalamu wa sheria ni mwalimu na pia naweza kusema ni mwana siasa nilipitia juu juu kidogo kuona ile misingi ya

utawala wa sheria, niliipitia mwanzo baadae ndio nikaja katika hiyo sheria wenyewe. Kwa hivyo, nikatafuta makala ya mtaalamu mmoja wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yeye ameorodhesha misingi minane ya utawala wa sheria. Lakini mimi kwa muhtadha wa hapa nitazungumzia mitatu tu.

Kwanza katika hiyo mitatu niliyoiteua kuizungumza yenye muhtadha na mazungumzo yetu, yeye amezungumzia *supremacy of the law* ambayo kwa ufupi kanuni hii inasema kila mtu au mtumishi wa umma anawajibika kufuata sheria iliyopo na anapokiuka ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, ya pili anazungumzia *concept of justice and equality before the law* na tatu kazungumzia kitu ambacho Mhe. Fatma amekizungumzia yeye anasema sasa hivi hakuna mambo ya *retrospective legislation* lakini ni wakati wa *prospective legislation* nasema hayo yanatosha kuyataja mengine hayana maana sana nikiyataja. Mimi nikiangalia kidogo katika sheria hii naona mapungufu haya matatu nayaona yamejitokeza katika sheria hii kwa sababu hii sheria kuna vipengele vilivyotajwa kuadhibiwa Maafisa wa Serikali, lakini pale watakapozembea katika kuiwakilisha serikali. Mhe. Spika, ikiwa Afisa wa Serikali ameiwakilisha vibaya pengine katika mikataba au mambo mengine pale imetajwa adhabu. Lakini pale anapokuwa amemdhulumu raia inakuwa hakuna adhabu. Mhe. Spika, mimi naona hapo pana mapungufu.

Mhe. Spika, ukiiangalia hii sheria inayoi-*benefit* ni serikali lakini sio mwananchi wa kawaida ambao hao raia ukiwachukua mmoja mmoja ndio kwa ujumla wao wanayoifanya hiyo serikali. Kwa hivyo, utaona kwa athari yake ubaguzi upo.

Mhe. Spika, jambo jengine kama nilivyozungumzia kuna nafikiri kifungu cha 15 kama alivyokitaja Mhe. Fatma hiyo tuliyozungumza ambayo ni *retrospective legislation* sasa hivi wataalamu hawa wanatukataza tuondokane na hili. Mimi nasema haya sio mawazo yangu ni mawazo ya wataalamu ambao ndio waliobobea kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa hivyo, baada ya kuona mapungufu hayo nataka nije katika ile sheria yenyewe.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze katika kifungu cha 3 kuhusu serikali kuwajibika kama mtu. Hapa wameanza vizuri na maelezo yaliyopo pale katika kijifungu cha 1 na 2 ukiyasoma kweli unaona kama sheria ni nzuri, utaiona kama serikali ina dhima kama mwananchi wa kawaida ndio inavyozungumzwa hapa. Lakini ukiisoma yote hii sheria ile athari yake halafu ukiangalia kwenye madhumuni na sababu yanatosha kukupa ujumbe kwamba kinachokusudiwa hasa na nimefurahi sana hapa katika marekebisho haya madhumuni na sababu tuliyopewa asubuhi kwani yanakupa sababu ya kutosha kwamba madhumuni ya sheria hii ni kuzuia mali ya serikali kutokukamatwa.

Lakini mali ya raia je? Kwa sababu ukisema unaunda sheria kwamba mali ya serikali isikamatwe je, huyu mwananchi mwengine kwa nini umewekee sheria mali yake isikamatwe huu ndio usawa wenyewe. Mhe. Spika, sheria unapoiweka upande mmoja basi upande wa pili utakuwa huutendei haki lazima iwe *address* kwa wahusika wote.

Mhe. Spika, mimi nadhani kama tunalinda mali ya serikali basi pia tulinde na mali ya raia wetu kama mwananchi anaidai serikali au serikali inapodaiwa na mwananchi Mahakama inazuiwa isikamate mali ya serikali ikauzwa. Je, sasa serikali inapomdaia mwananchi nayo ilikuwa ilindwe. Mhe. Spika, hapo tungefanya mchezo ungekuwa mzuri zaidi na ungekuwa wa haki zaidi. Lakini ikiwa serikali unailindia mali yake isikamatwe, sawa mimi nakubali kwamba utakuwa unajenga heshima kwa serikali, lakini haitoshi kujenga heshima kwa serikali na huyu mwananchi mlipa kodi naye umjengee heshima kwamba hata huyu naye mali yake tuilinde kama inavyolindwa ya serikali.

Mhe. Spika, jengine nataka niulize katika kifungu cha 6, kijifungu cha 5 kidogo. Hapa tunaambiwa kwamba kesi zitafunguliwa katika Mahakama Kuu au Mahakama ya Mkoa. Jana mtaalamu alitwambia kwamba Mahakama za Mkoa ambazo zitakuwa na uwezo ni zile ambazo kuna Mahakimu waliokuwa wana *extended jurisdiction*. Suala langu mimi nauliza jamani katika hii labda Mhe. Waziri atatusaidia hivyo katika Mahakama zetu za hapa ni Mahakimu wangapi wenye *extended jurisdiction***.** Nauliza suala hili kwa sababu nina hofu kwamba pengine inawezekana katika hawa Mahakimu wa Mikoa ikawa hawapo wenye *extended jurisdiction* ikawa bado watu wanakwenda kule kule Mahakama Kuu.

Kwa hivyo, ikawa ule usumbufu wa kufungua kesi bado ikawa upo ama ikiwa hao Mahakimu wenye *extended jurisdiction* wako huko katika Mahakama za Mikoa ambao mimi kama hawapo basi nadhani ni suala la mazingatio kwa sababu mwananchi kumtoa mbali kuja kumlazimisha mpaka kufika Mahakama Kuu nayo ina matatizo yake.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kuzungumza ni kwamba nataka niipongeze serikali katika kifungu cha 7, hapa imezungumza wazi kwamba wale maafisa watakaoisababishia serikali hasara kama nilipozungumza mwanzo watapata adhabu. Sawa ni suala zuri, lakini mimi nasema hili ninalozungumza sio la kisheria zaidi lakini ni la kiutendaji zaidi. Mhe. Spika, serikali ikitaka isipate hasara kwanza ni kuteuwa Maafisa wenye uwezo, kuwa na wanasheria wenye uwezo na wenye uadilifu. Mhe. Spika, ikiwa wanakwenda kupeleka watu kufunga mkataba ambao wewe mwenyewe unajua kwamba huyu hana uwezo, halafu ukaja ukam-*punish* kwa sababu ameshindwa kuiwakilisha serikali vizuri.

Hivyo utakuwa unamuonea kwani yeye hakujiteua mwenyewe, wewe ndiye uliyemteua.

Kwa hivyo, hapa ni pahala pa mazingatio au hata unapotafuta mawakili wa kujitegemea ukawapa kazi halafu wakashindwa ukaja ukawaadhibu utakuwa umewaonea kuwafanyia haki. Kwa hivyo, nadhani haya ili kuyaepuka yasitokee basi ni wajibu wa serikali yenyewe kuhakikisha kwamba inapoteua watu wake basi watafute watu waliokuwa ni wa uhakika haya madhara ili yasitokee halafu tukaja tukawapa adhabu. Mhe. Spika, mtu unampa kazi ambayo sio kiasi chake halafu ashindwe kuiwakilisha serikali, hivyo itakuwa unamuonea. Hili nadhani nilitaka nilizungumze katika mtazamo huo.

Mhe. Spika, sasa nataka nije katika kifungu cha 11 (3) ambacho jana katika semina nimekizungumza lakini sikuridhika hata kidogo kwa sababu pale jana ilikuwa ni semina tu, lakini leo nataka nikizungumze tena. Mhe. Spika, kifungu hiki cha 11 (3) ni kile ambacho naomba nikinukuu.

"Katika madai yoyote dhidi ya serikali kwa ajili ya kurejesha ardhi au mali nyengineyo Mahakama haitotoa amri ya kurejeshwa ardhi au kurejesha mali lakini badala yake inaweza kutoa amri ya kutangaza kwamba mdai anastahiki ardhi au mali au kushikilia mali hiyo".

Mhe. Spika, kwa kweli jana hiki katika semina tumekilalamikia karibu sote tuliochangia semina, mimi kwa kweli nasema bado sijaridhika hata kidogo kuona kwamba Mahakama imeshaona kwamba hii mali ni ya Haji Faki Shaali lakini bado iwekewe masharti au kigugumizi juu ya kutoa amri kwamba nipewe mali yangu. Mimi sioni umuhimu wa kutoa *declaration* Mahakama kwamba hii ni mali ya Haji Faki Shaali lakini isishindwe kunipa mimi mali yangu. Ndio nikasema kwamba hii sheria inaipendelea zaidi upande wa serikali na inawanyima haki wananchi, wakati hao wananchi kwa umoja wao ndio wanayoifanya hiyo serikali. Mimi nadhani mambo haya yanataka mazingatio sana.

Mhe. Spika, hapo hapo pana kifungu cha 11 (4) kinasema Mahakama katika shauri lolote haitotoa amri ya kuzuia au kutoa amri yoyote dhidi ya Afisa wa Serikali iwapo kutolewa kwa amri hiyo ya kuzuia au kutolewa kwa amri hiyo kutaleta athari kwa serikali ambapo isingepaswa kutolewa katika madai dhidi ya serikali. Mhe. Spika, hapa kwa kweli inayolindwa ni serikali peke yake isipate madhara, apate madhara mwananchi.

Mhe. Spika, kwani hawa wananchi sio wetu sisi. Ndio nikasema hii sheria zaidi imekwenda upande wa serikali badala ya raia wake ambao hao raia ndio wanayoifanya hiyo serikali yenyewe iwepo. Mimi naona haya ni mapungufu na

ndio nikaanza mwanzo kutaja ile misingi mitatu ya utawala wa sheria. Nimetaja kwa makusudi kuona kwamba kidogo ukitoa maelezo ndio zile *concept* zinapokuja barabara kwamba kweli hapa mapungufu yapo.

Mhe. Spika, pia nije katika kifungu cha 12 (3). Mhe. Spika, kifungu hiki kinasomeka hivi kwamba hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachoathiri uwezo wa Mahakama kuamuru au sheria nyengine yoyote inayoweka malipo ya gharama kutokana na mfuko wowote au mali maalum au sheria yoyote inayoendelea wazi wazi idara au afisa yoyote wa serikali dhima ya kulipa gharama. Hapa mimi sijafahamu kwa sababu huku nyuma kuna vifungu vinakataza Mahakama inapewa nguvu kufanya maamuzi fulani, lakini hapa inapewa uhuru na inasema hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachoathiri uwezo wa Mahakama kuamuru. Hiki ni kifungu kinachozungumzia gharama katika madai ambayo serikali ni mdau.

Kwa hivyo, ndio nasema kidogo hapa napata mashaka kwa sababu kuna vifungu vyengine tayari Mahakama imezuiwa kutoa amri. Lakini hapa Mahakama inaonekana inapewa uhuru hapa kidogo sijui ni gharama zipi zilizokusudiwa lakini kidogo napata kigugumizi labda nitapata ufafanuzi kwamba kule ni mambo yepi ambayo yana uhuru wa kuyafanya na mambo yepi hayana uhuru wa kuyafanya. Mhe. Spika, pengine mimi sijafahamu vizuri kwa hiyo naomba nifahamishwe vizuri.

Mhe. Spika, ukiangalia kile kifungu cha 3 kinakupa matumaini kwamba kumbe Mahakama ina uhuru lakini ukiangalia vile vifungu vyengine vya nyuma utakuta hakuna baadhi ya mambo. Hapo kidogo nitahitaji nisaidiwe zaidi.

Mhe. Spika, vile vile nije katika kifungu cha 15 (4) ndio hasa katika madhumuni na sababu naomba nikinukuu.

“Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki, hakuna utekelezaji wa hukumu, mauzo, ukamataji wa mali inayohamishika na isiyohamishika ya serikali au hatua ya aina hiyo ambayo itatolewa na Mahakama yoyote kwa ajili ya kuilazimisha serikali kulipa fedha zozote au gharama zilizotajwa katika kifungu hiki na hakuna mtu anayewajibika binafsi kwa amri yoyote ya serikali kulipa, au idara yoyote ya serikali au afisa wa serikali kwa fedha au gharama hizo”. Mimi nasema kwamba heshima ya serikali itapatikana.

Mhe. Spika, hapa serikali itajijengea heshima maana sasa hakuna gari ya Spika itakayokamatwa, Katibu Mkuu itakayokamatwa kwa hivyo huko ni kujijengea heshima kwa serikali kwamba itakuwa haiadhiriwi. Lakini nataka niungane na Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej pamoja na Mhe. Hamad Masoud Hamad jana katika semina kwamba wananchi wataogopa kuikopesha serikali, hasa wale

wananchi wanaopeleka vitu katika mahospitali, *boarding* na katika vikosi, kwa kweli wengi wao wataogopa watajua mimi sasa hivi kuidai serikali sio kitu cha mchezo ni kitu kigumu.

Mhe. Spika, nasema kifungu hiki kimeijengea heshima kubwa sana serikali yetu. Lakini kifungu hiki kitatorosha *supplies* wengi katika serikali kwa sababu mwananchi kutokana na masharti ya sasa hivi ya kuidai serikali yalivyokuwa magumu sitegemei kwamba mtu masikini atakuwa tayari ku-*supply* chochote katika serikali yetu. Kwa hivyo, itakuwa tumejijengea heshima kwamba mali zetu hazikamatwi, tumejijengea kinga na pia tumefukuza watu ambao ni wasambazaji wetu katika serikali.

Mhe. Spika, sasa hivi nije katika kifungu cha 20 ambacho kinazungumzia kujilipizia deni na madai ndani ya ulipaji kodi. Hapa mswada huu wa sheria unasema kwamba mtu hatapaswa kujivua au kujilipizia deni lolote au madai ndani ya madai katika shauri lolote ambalo anadaiwa na serikali kwa ajili ya kulipa kodi. Nadhani na hapa napo serikali imefanya jambo zuri, lakini je, serikali kwa nini iwe *supply* hata kwa mwananchi? Mhe. Spika, ingekuwa ni bora kama serikali haitaki mwananchi ajilipizie deni basi na serikali nayo ingempa mwananchi fursa hii. Mimi nafikiri hii tungeifanya kwa wote wawili kwa serikali na kwa mwananchi hapo ndipo itakapokuwa sheria isiwe upande mmoja tu iwe kwa wote.

Mhe. Spika, sio kwamba serikali hatuipendi tunaipenda. Serikali ni yetu lakini na wananchi ni wetu ,basi ile heshima tuijenge kote mimi hapo ndio penye hoja yangu. Mhe. Spika, mimi kama nilivyozungumza sina mchango mkubwa mawazo yangu ndio hayo naiona kwamba sheria hii itajenga heshima kwa serikali kwamba mali zake zitakuwa katika hali ya usalama. Mahakama sasa hivi baada ya kufuta vile vifungu vya 59,60,61 na 62 vya *civil procedure* na kuweka vyengine hivi nadhani serikali itakuwa imepata afueni kidogo ya usalama wa mali zake. Mhe. Spika, mimi sifurahii sheria hii kwa suala moja tu, hii kwamba imeelemea zaidi upande mmoja kuliko upande wa pili. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi kuweza kutoa mchango wangu katika mswada huu uliowasilishwa hivi asubuhi. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi kubwa waliofanya ya kuleta mswada huu na mswada umekuja wakati muafaka.

Mhe. Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi na tayari Mwenyekiti wa Kamati ameshawasilisha maoni yetu, lakini na mimi nilikuwa na *point* mbili nataka nizizungumze nilizotumwa na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini. Lakini kwa bahati mbaya sana msemaji aliyemaliza zote

ameshazizungumza lakini nilikuwa nishatia nia na mimi nitazungumza kama vile nilivyokusudia.

Mhe. Spika, kwanza nije katika ukurasa 41 kwenye sababu na madhumuni. Sababu na madhumuni zimewekwa wazi kwamba sheria hii imeletwa kwa minajili ya kuweza kuzilinda mali za serikali na kama mtu ana madai basi lazima afuate taratibu zilizowekwa. Nadhani hilo sio jambo baya kwa sababu hivi karibuni tumesikia mambo mengi tu kwamba Hoteli ya Bwawani inataka kuuzwa kwa sababu serikali inadaiwa pesa za mchele, gari sijui ya nani inataka kukamatwa? Nafikiri kwa utaratibu huu sasa hivi kidogo haya yatapungua kwani kutafuatwa utaratibu pande zote mbili mdai na mdaiwa ili mtu aweze kupata haki yake kuliko huko nyuma mambo yalivyokuwa yanakwenda.

Mhe. Spika, nashukuru jana hapa tumefanyiwa semina wengi wetu tumefahamu juu ya makusudio na malengo ya sheria hii na semina ile imetufunua vichwa wengi na tumeweza kuelewa madhumuni makubwa yaliyokusudiwa katika sheria hii. Mhe. Spika, mimi nikiingia kwenye mswada kwanza kuna neno mdawa limetumiwa sana katika sheria hii, lakini mimi mwenyewe maana yake mpaka hivi sasa bado linashughulisha silijui. Kwa hivyo, ningeshauri kwamba labda kwenye ufafanuzi na hili lingewekwa maana yake kwamba mdawa imekusudiwa nini? Pengine ingesaidia kama mtu sio mwanasheria kama mimi akipata ufafanuzi wa mdawa anajua na mdaiwa anajua nini, hiyo itasaidia kidogo kuleta ufafanuzi wa suala hili.

Mhe. Spika, jengine nililokusudia kuchangia mswada huu lipo katika ukurasa wa 40 kifungu cha 20 ambacho kinajieleza naomba nikinukuu. “Kujilipizia deni na madai ndani ya madai kwa ulipaji kodi”. Hii imekusudiwa hapa kwamba zaidi imekwenda upande mmoja kwa mfano, mimi nafanya biashara halafu pengine nimechukua tenda serikalini lakini imetokezea bahati mbaya ama nzuri mimi nadai na mimi nadaiwa inategemea sasa nani aliyemzidi mwenzake kumdai. Lakini hapa kubwa limekuja kwa mdaiwa zaidi mfano kama mimi mwananchi kwenye serikali.

Kwa hivyo, mimi ningelishauri kwamba wataalamu bado wapo ikitokezea kesi kama hii mimi mwananchi nadai serikali na serikali inanidai basi nadhani angeliwekwa mtu wa tatu wa kuweza kutizama vipi ifanywe ili haya matatizo yaondoke. Kwa sababu hapa nilivyofahamu mimi sheria zaidi imekwenda kumbana mwananchi, lakini kawaida ya sheria na penye utawala bora intakiwa pande zote mbili ziwe sawa. Sasa wanasheria kama wanaweza kututafutia lugha nzuri au njia nzuri kwamba ikitokea mambo ya *draw* kama haya mimi mwananchi naidai serikali na serikali inanidai basi papite usuluhu kwa njia nyengine ili tatizo liondoke kwa ulaini zaidi.

Wenzangu wengi waliotangulia wameona kwamba wananchi watafanya hofu sasa hivi kutoa *tender* labda kuisaidia serikali katika mambo mbali mbali, kwa sababu bado wananchi wanaisaidia serikali yao katika mambo mengi tu, kama vile vifaa, hospitali, chakula na sehemu nyengine. Sasa kwa utaratibu huu nadhani mimi wakisikia hao wahusika watafanya hofu na tutazidi kuitwika mzigo serikali. Lengo ni kwenda vizuri lakini tutakuwa tunajitia mazonge.

Sasa nashauri kwa wanasheria kama kutakuwa na njia nyengine nzuri likitokea jambo kama hilo basi pawe na mtu wa watatu wa kuweza kutumalizia suala hili bila kuingia mgogoro mkubwa zaidi na pande zote mbili ziweze kuridhika.

Mhe. Spika, *point* yangu ya pili niliyokusudia kuizungumza katika mswada huu iko ukurasa wa 35 na inazungumzia juu ya Sehemu ya Tatu, Mamlaka na Utaratibu. Maneno ya pembeni yanasema, Madai zidi ya serikali na kadhalika, lakini nia yangu ni nambari 7 kifungu cha (a) ambacho hapa kinamzungumzia afisa yeyote wa serikali atakayepewa majukumu pengine akasababisha hasara kuingia kwenye serikali.

Mimi nilipoisoma hii nimeona kidogo haki haijatendeka. Kwa sababu kama mimi ni afisa wa serikali na nimetumwa nifanye shughuli fulani, nadhani kama nitashindwa kuna sababu za msingi pengine zimetokea, pengine nje ya uwezo wangu.

Kwa mfano nimeambiwa niende Makunduchi saa 7 kuna kazi muhimu nikaifanye, lakini gari sikupata kutoka kwenye shirika au taasisi ninayofanyia kazi. Nimefika kule saa 12 wahusika hawapo tumepata hasara, sasa ukitizama suala kama lile mimi siye niliyehusika kutia hasara lakini nimesababishwa niingie kwenye hasara ile.

Sasa ningeshauri serikali ama watunga sheria hii ikamtizama zaidi huyu afisa anayetumwa na serikali juu ya masuala hayo. La kama nimefahamu vyengine basi, lakini kama ni hivyo basi yako mengine ana nia ya kufanya kama alivyotumwa lakini vikwazo vinakuja viko nje ya uwezo wake. Hilo nalo lingezingatiwa lingeweza kusaidia pande zote mbili kupunguza hasara lakini pia na kumuazibu yeye wakati hakutegemea kufanya vile. Alikuwa na nia nzuri lakini kuna sababu zilizomfanya ashindwe kutekelezewa yale ambayo yangefaa kuyatumia mpaka akafika kule kulikokusudiwa.

Mhe. Spika, sikuwa na maneno mengi lakini na mimi nimetia baraka katika mswada huu. Mimi kwa niaba ya wananchi wangu naunga mkono mswada nashukuru.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia kidogo katika hoja hii iliyoletwa hapa. Mimi nataka kutoa tahadhari tu, kwamba sheria hii kwa kweli itakuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa wafanyabiashara wa ndani na wa nje kutoa mikopo kwa serikali.
Utaratibu wa sheria unakubalika kimaudhui, kwamba serikali ili iwe na hadhi basi ni bora pawe na mipango mizuri ambayo kwamba haitokaa tu ikaadhiriwa kama mtu mwengine yeyote yule. Hilo linakubalika.

Lakini ukienda katika hukumu, hukumu ikitolewa kwa mujibu wa sheria hii kwa kweli inampa haki ndogo sana mdai hasa akiwa ameikopesha serikali. Mwananchi wa kawaida atakuwa anashungulika na mambo ya ardhi na *compensation* za mambo ya kawaida. Lakini nasema hapa basi serikali inashughulika sana na mfanyabiashara wa ndani na wa nje, hii kwa kweli serikali inapata msaada mkubwa sana wa kupata nyezo nyingi kwa njia za mikopo.

Wafanyabiashara wa ndani na nje wanakopesha vyakula, *building materials*, majengo, hata ukiangalia sisi Baraza la Wawakilishi tayari tuna mtu anajenga Baraza la Wawakilishi na ndani yake mna *element* ya mkopo. Sasa mtu akisikia kuna sheria ambayo hakimu akishatoa hukumu baadae waziri anaitungia kanuni ile hukumu, bado waziri nje ya Mahkama ana madaraka ya kutunga kanuni juu ya ile hukumu iliyotolewa katika Mahkama.

Inaonesha kwamba Mahkama haikuwa chombo cha mwisho cha kutoa haki bado waziri anayo haki ya kutoa kanuni kwa ajili ya ulipaji wa yale madai ya mdai. Hali hii inatia wasi wasi sana. Kwa hivyo, mimi ningeomba kwamba katika suala la hukumu au katika suala la kutoa haki hata ikawa kwamba hakuna kufilisiwa moja kwa moja kwa ile mali ya serikali. Lakini bado itoke hukumu halali kabisa kwamba mfanyabiashara huyu au shirika hili lina haki yake na lilipwe na utolewe muda wa kulipwa na Mahkama na sio waziri aipangie, inaweza ikachukua miaka 20 bado huyo mdai hajapata haki zake.

Jengine wawekezaji wote wanapokuja katika nchi wanaangalia miundombinu, lakini muundombinu mmoja wapo muhimu sana ambao kwamba sote huuusahau, huangalia kwanza barabara, maji, sijui nini?, lakini wengi wanaangalia *legal frame work* za ile nchi. Kwa hivyo, mimi naamini kwamba hii sheria imetungwa kwa kuangalia mlengo mmoja tu, kwamba kumekuja sheria sasa kuwa zikija hukumu nyingi kwamba mdai anadai kauza mchele Bwawani itataifishwa, gari ya Mkuu wa Mkoa, gari ya Mkuu wa Wilaya, ya Spika, lakini haikuangalia *another side of the coin*, kwamba *legal frame work* ni vitu muhimu sana kwa wawekezaji na kwa kweli wakija wakiangalia wakiona kwamba sheria hii imeegemea upande mmoja, imeipa mamlaka

makubwa zaidi serikali kuliko mdai mwengine yoyote, hii inatushushia hadhi kidogo katika masuala haya ya uwekezaji katika nchi yetu.

Tumesema kwamba mashirikiano ya kibiashara baina ya serikali na wafanyabiashara wa ndani na nje itaathirika kwa kiwango kikubwa sana kuletwa kwa sheria hii hasa katika suala la hukumu ya kesi hizo.

La pili uwekezaji, vile vile wawekezaji watakuwa *very argumentative* kwenye suala hili. Mimi ningetaka *just* kuwa *attention* na kuona kwamba ipo haja ya kuangalia namna gani ya kuweza kurekebisha kuona kuwa katika sehemu mbili hizo ziko wazi zaidi na zinatoa imani nzuri kwa wafanyabiashara na wawekezaji. Ahsante sana.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, kwanza na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi, nimshukuru waziri na mwenyekiti wangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Tulipokutana kama nilivyoeleza jana kwenye kamati tulifanya uchambuzi wa kutosha na mara nyengine ilikuwa mjadala mkubwa sana juu ya kutafuta jinsi ya kurekebisha sheria hii. Jana nilisema tena kwamba mimi kinachonisumbua si suala la kulinda mali ya serikali kama vijana wetu walivyokuwa wakijibu, sisi tunajua kwamba mali ya serikali ni mali yetu sote, lakini hiyo serikali yenyewe haiwi kama hakuna watu na hao watu wenyewe vile vile wanalindwa na katiba.

Jana nilisema pale kwamba katiba inatulinda nikajibiwa kuwa mbona sikusema wapi panapolinda. Kuna *chapter* nzima sura ya tatu ya katiba yetu inayolinda haki za raia wetu na bila ya kuvisoma vyote naomba nisome kifungu cha 12(1), (2) na (3).

Kifungu cha 12(1),(2),(3):

> "Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. Hakuna sheria itakayokuwa na kifungu chochote ambacho ni cha ubaguzi wa moja kwa moja au kwa taathira yake".

Hapo taathira ni mwili au mali zake, haki za raia ambao ndio sisi, wajibu na maslahi ya kila mtu yatalindwa na kuamuliwa na Mahkama, *my emphasis*, kuamuliwa na Mahkama pamoja na vyombo vya nchi na vyenginevyo vilivyowekwa na sheria.

Sasa kinachonipa shida mimi ni kwamba Mahkama inatakiwa ilinde haki zangu na ione kwamba vile vile haki au mali ya serikali inalindwa. Sasa Mahkama yenye maamuzi ya kusema huyu ana haki inawekewa sheria inaambiwa huna

haki ya kusema hivyo, hapa kidogo ndipo panaponipa shida na naomba nisome nimeviweka hivyo vifungu na mwisho nitatoa maoni yangu kwa ushauri.

Kifungu cha 11 kimesema sana hapa, Mahkama katika shauri lolote haitatoa amri, sasa atoe nani mwengine? Maana zaidi ya Mahkama hakuna labda msamaha wa rais, lakini hapa ndipo niliposema jana kwamba sote tukiona tumeonewa tunakwenda kwenye Mahkama. Sasa hapo inasema haitotoa amri kuzuia au kutoa.

Mhe. Mazrui kasema kwamba barabara inatakiwa kujengwa ipite karibu na nyumba yangu, sasa nyumba yangu kwa mujibu wa barabara mpya Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi anasema hii vunja, linakuja *bulldozer* linavunja. Jamani lakini nina nyaraka zangu hizi mimi sikujenga kwa nguvu hapa, ninazo, unaambiwa ala! Ondoka, ondoka, ondoka chuma kinavuruga. Naona nikimbilie Mahkamani lakini nako naambiwa huna ruhusa hata kuiruhusu *injection*. Hili kidogo Mhe. Spika, naona ni tatizo.

La pili nimeki-*circle,* kifungu cha 15(4) "Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki, hakuna utekelezaji wa hukumu. Sasa hukumu ishaamuliwa isitekelezwe, aliyetoa hukumu ni Mahkama, kidogo napata tabu. Sasa kama hukumu isitekelezwe mimi nangojea mpaka lini mnyonge.

Lakini tatu kifungu cha 16 kinasema kwamba, "Chini ya masharti ya sheria hii amri yoyote iliyotolewa kwa maslahi ya serikali zidi ya mtu yeyote katika kesi yoyote ya madai ambayo serikali inadaiwa itatekelezwa. Ndio jana nikasema huku kila kitu fanya, huku huna ruhusa, yaani madhali serikali inanidai basi inaweza kufanya kitu chochote lakini kama mimi nadai hata Mahkama haina uwezo. Hicho ni cha tatu Mhe, Spika.

Mwisho kifungu cha 16(3) nadhani ni hivyo vitatu. Sasa tulipokuwa tunazungumza kwenye kamati tulichogundua kwamba hii sheria ilikuja kwa sababu fulani matokeo ya mambo mengi. Matokeo ya kwanza ni kwamba serikali tunadaiwa na matajiri wa nje, lakini ingekuwa ni matajiri wa nje tu ndio tunaoshindwa kuwalipa au ndio tunao matatizo nao ningeweza kuona kwamba kuna huo ugumu wa uwezo wa kulipa. Lakini pia tunadaiwa na wananchi wa kawaida. Sasa wananchi wa kawaida kuidai serikali huwezi kuiunganisha na watu wa nje kutudai, yule mtu wa nje nasikia alitaka hata sote tukiuzwa sisi hatuwezi kumlipa ni upumbavu**,** lakini anadai.

Na hata akifika hapo kulikuwa na kipindi kilichopita, jana nilisema hapa Mhe. Spika, lakini nikawa sipendi kutaja watu, nimesema nina mifano hai hivi ninavyosema, mwananchi anadai si mtu wa nje na wala hadai mabilioni anadai pesa tu kwa sababu ardhi yake imechukuliwa hakuambiwa na imejengwa kwa

maslahi ya serikali ni sawa, lakini na mimi nina nyaraka hizi nimerithi kwa babu yangu. Kenda Mahkamani na ikaamua alipwe halipwi, karudi Mahkamani ka-*appeal* tena halipwi.

Jana nilisema hapa polisi wenyewe walifanya dudu hilo wakachukua ardhi ya watu jamaa kenda Mahkamani halipwi, karudi Mahkamani hajui afanye nini, basi Mahkama wakasema kama polisi nao wasimamiaji wa sheria wanafanya jeuri zuia gari yao, ndio ile aliyosema Mheshimiwa. Sasa polisi anaambiwa akamate gari ya polisi. Sasa huyu raia mwishowe aende wapi? *Infect* kwa taarifa yako Mhe. Spika, ilibidi ende kwa mkubwa wa wakubwa wa polisi kumwambia nadai silipwi.

Sasa ninachoataka kusema hapa ni kwamba kuna pengine maafisa kutokutekeleza amri hizi kwa sababu wanajiona wako serikalini, maana ile ya mtu wa nje na hii ya nje mpaka ikafika hatua hii ni kwamba kumekuwa na tatizo hilo. Sasa ushauri wangu ni kwamba mimi tunakwenda Mahkamani na serikali tukifika pale serikalini mwenzangu tayari yeye ana magoli mawili bila, mimi ndio kwanza nina *zero.* Nakwenda Mahkamani kushindana naye yeye keshaambiwa yule Mahkama huyu bwana akitaka kudai akifika Mahkamani usitekeleze. Kwa hivyo, nakwenda pale keshanishinda hata hatujafanya hukumu.

Tulishauri kwenye kamati kwamba waziri atunge kanuni na hapa ndio nakubaliana na mwenzangu Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba kunahitaji vile vile kuingiza kama kwenye sheria hii au wapi huu ukomo wa kudai. Kuwe na wajibu na yule serikali anapodaiwa, waziri ajifunge kwamba katika utaratibu huu tunaouweka wa kudaiwa serikali basi serikali itawajibika si zaidi ya kipindi fulani kumlipa mdai vyenginevyo mdai masikini ya Mungu anaweza kudai miaka mitano mpaka sita mpaka anakufa, wengine wanadai mpaka wanakufa, wanakuja warithi wanadai na wao wanakufa na zipo kesi Mhe. Spika, wanadai watu *family* mpaka yule anayedai anafariki na bado haki zake hapati.

Sasa katika huko kulinda heshima ya serikali basi tujifunge na sisi serikali kwa wajibu ule ule, kwamba tuna wajibu wa kulinda mali ya serikali kama maafisa waandamizi tuliyoko kwenye madaraka, lakini vile vile wajibu wa pili tuna wajibu wa kulinda raia ambao ndio waliotufanya tuwepo kwenye zile nafasi kiutawala, vyenginevyo itakuwa ni kudhulumu.

Hivi karibuni kuna afisa mmoja alinambia kwa jeuri tu, afisa anamwambia mtu sitaki, nikapiga hee! Akanambia ndio babu Juma, afisa anasema sitaki, ni kwa sababu yuko pale na ana ile *power* ya ku-*executy* ile sheria. Basi yule jamaa akanyamaza kimya na mambo yakaharibika akatoka. Sasa kunahitaji hiki kibri nacho kiwekewe mipaka Mhe. Spika, ili tupate heshima kama serikali. Kwa

sababu kudaiwa mabilioni na kufilisiwa ni vibaya, lakini kudaiwa milioni kumi mpaka kumi na tano mpaka ikawa inataka kuwekwa *tanji* ya mali ya serikali kwa milioni ishirini vile vile nayo si nzuri.

Kwa hivyo, kwa mchango huo Mhe. Spika, jambo langu la mwisho basi labda kuwe na kitu kinachoitwa *arbitrator*. Sasa sijui labda wanasheria hapa watatusaidia. Kuwe na kitu *arbitrator,* basi kuwe na mtu wa tatu ninayeweza kwenda nikalalamika na tukakutana hapo ili kuhakikisha kwamba tunalinda maslahi ya serikali lakini wakati huo huo tunalinda maslahi ya raia wetu. Mimi natizama zaidi raia wetu kwa sababu sheria hii haijasema kwamba anawekewa mgeni tu, imesema ni sheria tu, na siku huwa nasema mimi.

Jana aliji-*commit* hapa kwamba yeye katunga kanuni za Baraza za Miji , yeye mwenyewe akajikuta zimemtia adabu. Kwa hivyo, tunatunga hii pengine vilembwe vyetu, vijukuu au watoto wetu watakuwa *victim* wa sheria hii. Sasa tunahitaji kuwalinda si kwa sababu tuwalinde ni kwa sababu na wao wana haki ya kulipwa. Ahsante Mhe. Spika, naunga mkono sheria.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuzungumza machache kama wenzangu. Kwa sababu mengi yameshazungumzwa na pengine isingehitaji wengine kusimama lakini kwa sababu tuna wajibu huo ni vyema na sisi tuwe tumezungumza chochote.

Mhe. Spika, napenda nichukue nafasi hii pia kukushukuru kwa kunipa nafasi lakini niwashukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake, lakini pia niungane mkono pia na kaimu waziri kivuli wangu, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwa mchango wake mwanana kabisa.

Mhe. Spika, nianze mchangu wangu kwanza kwa kukubaliana sana mia kwa mia na Mhe. Rashid Seif pale aliposema kwamba serikali ijitahidi kadiri inavyowezekana isikope kwa watu masikini. Kwa sababu matokeo yake ndio yanaifikisha serikali kuleta sheria kama hii. Ni sheria nzuri Mhe. Spika, kwa madhumuni na kwa sababu, lakini jinsi ilivyo bado inakuwa na mashaka kiasi ambacho nadhani kwa hekima kubwa ya Mhe. Waziri atakubaliana na sisi kufanya marekebisho ili sheria hii iweze kutekelezeka na iweze pia kutekeleza haki za kila mmoja, kwa upande wa serikali na upande wa wananchi mmoja mmoja au ikiwa kwa vikundi.

Serikali itakapokuwa inakopa kwa matajiri na hii sijawahi hata siku moja kama alivyosema Mhe. Rashid Seif kusikia imetoka huko dola ya Kiingereza au Marekani na kwengineko kuja wakaishitaki, si Zanzibar tu, lakini hata Tanzania, lakini wanachofanya na tulichozowea kusikia ni kwamba wanafuta madeni wanasamehe. Kwa hivyo, kwa sababu ya umasikini wetu pengine na

udogo unazidi kutilisha huruma tukiwakopa wakubwa hao na kufika pahala wakaona hawa watu huu unakuwa mzigo kwao acha tuwasaidie.

Kwa maana hiyo basi, zinatoka kauli za kutusamehe na tutaepukana na hii kukimbizana na watu katika vichochoro na kukamata magari kutaka kufilisi mali mbali mbali za serikali jambo ambalo si aibu kwa serikali tu, lakini hata mimi kama Mzanzibari nitajisikia vibaya vile vile mtu atakapokuwa anazungumzia kuhusu kadhia fulani inayohusu kuchukuliwa mali za serikali au ikiwa ni taasisi kama hizo Polisi, Mkuu wa Mkoa au Waziri na kadhalika. Kwa hivyo, tungeomba sana serikali iwe inaachana na hilo suala.

Sasa katika kutazama hilo pia niungane na waheshimiwa wenzangu kuhusiana na sheria. Mhe. Spika, sheria hii bado imetazama upande mmoja tu wa shilingi haikugeuza upande wa pili. ndio maana kunatokea vitu kama hivi pengine mpaka tunajisahau katika kuihami serikali tunajikuta tunasahau wajibu wa wengine, mihimili ya dola kila mmoja hautaki kuingiliwa. Lakini ni dhahiri kwenye mswada huu kwamba Mahkama imenyooshewa kidole kama mtoto vile anagombwa.

Nasema hivyo Mhe. Spika, katika kifungu cha 15 cha sheria hii sipendi nirudie lakini kifungu hicho kinachozungumzia utekelezaji, kuna kifungu cha 15(3) inaonesha hapo na nimekipigia mstari suala la kwamba, ikiona ni busara kufanya hivyo. Kwa sababu sio kwamba ikiona kuna haki ya kufanya hivyo, lakini ikiona ni busara, maana yake sawa sawa na mtoto pengine na mtu mkubwa. Mtu mkubwa kamkosea mtoto lakini kwa sababu ya kutumia busara mtoto ndio achapwe ili kulinda heshima ya mkubwa. Sasa hapa haikulengwa haki kutendeka lakini imelengwa kutumia busara katika kuhami mtu mzima asiadhirike.

Sasa kisheria Mhe. Spika, hili nadhani tulitizame mara mbili na tatu na tuone kwamba tunaliweka katika mstari unaostahiki kuwekwa na sio tu kulichukua kwa sababu madhumuni ni kuilinda serikali. Sote tuna wajibu wa kuilinda serikali na kuona kwamba tunalinda mali zake ambazo ni zetu pamoja. Lakini wakati huo huo serikali nayo ione kwamba raia kwa ujumla na wao wana haki ambazo zinastahiki kulindwa.

Mifano imetolewa hapa, mtu ameshabomolewa nyumba yake kwa sababu hawakuwekewa muda serikali wa kutekeleza mambo fulani fulani na pengine haki ikaweza kutendeka, matokeo yake Mhe. Spika, nitoe mfano wa mtu kunyongwa lakini baada ya kukaa kutafakari unakuta amenyongwa kimakosa, lakini ameshakufa, nani analipa sasa?

Ni kweli kama alivyozungumza Mhe. Juma Duni Haji kuna watu ambao wanaidai serikali na hawapo sasa hivi duniani, na warithi wao pengine miongoni mwao hawajamalizika wote lakini wapo ambao wameshakufa bila ya kulipwa haki zao. Je, hili tunaliweka katika utaratibu upi. Sasa nadhani ni vyema sana wakati tunapoona limetokea kosa kwa sababu kufanya kosa si kosa ila kosa ni kurejea kosa, tunataka kuihami serikali lakini wakati huo huo na upande wa pili serikali nayo ina kosea, inawezekana si kwa makusudi lakini ndio inatokezea inakosea kama ambavyo imekosea hapa sasa hivi.

Serikali imeingilia uhuru wa Mahkama na hii inajionesha kama nilivyosema kwamba imekwenda kinyume hata na katiba kifungu cha 12. kifungu cha 15(4) kinajionesha dhahiri, sitaki nirudie maneno yote lakini kifungu hiki kinaelezea haya ambayo nayasema.

Mhe. Spika, mimi jana katika semina hapa nilisema na ndio maana sikutaka kusema mambo mengi nilitaka angalau nije niseme leo kidogo, kwamba hii sheria kwa ilivyo haikuhitaji kuwa na maneno mengi ilikuwa iseme tu kama serikali isishtakiwe. Alinitisha zaidi bwana Katibu Mkuu alipokuja kutoa ufafanuzi wake pale akasema nimeogopa kidogo na bado naogopa mpaka nipate ufafanuzi vizuri. Anasema hatuko mbali sana na wenzetu wa Jumuiya ya Madola wanaofanya shughuli hizi.

Nadhani alikusudia na kwa nilivyofahamu mimi aliwa-*quote* watu wa Ulaya na pengine inawezekana Uingereza au sehemu nyengine ambazo ni za Ulaya. Akasema sisi tumetoka katika kushtaki serikali kidogo kidogo tunakuja kuielekeza kama kifungu cha 15 kinavyojieleza kwamba sasa serikali inaelekea isishtakiwe. Sasa mpaka hapo sikuwa nimeogopa, lakini nilipoogopa ni yale maneno aliyoongeza kwamba wenzetu wametoka katika kutokuishtaki serikali sasa wanakuja katika kuishtaki.

Mhe. Spika, sasa nikaona mbona sisi tunarudi nyuma, tunarudi nyuma kwa maana ya kwamba mimi nikitoa mfano kama wa dola ya United Kingdom naiona kama kidogo kidogo inataka kuondokana na mambo ya ufalme hivi, kwa mbali inaonesha hivyo. Sasa ikiwa wenzetu wanatoka kwenye hiyo wanakuja katika upande ambao unakuwa ni wa kidemokrasia zaidi na kwa sababu katika hali hizi kunatakiwa *symbol* ya utawala bora wa sheria, sioni kama kutakuwa na haja ya kuogopa kuishtaki serikali. Serikali bado ni sisi tunaoongoza, sasa tunapoifikisha pahala wenzetu ambao tunawaita ndio walioendelea wanatoka huko wanakuja tuliko sisi, sisi tunatoka tunakwenda kule nyuma ambako wao wamekuacha inanipa mashaka kidogo.

Sasa nadhani mfano ule vyenginevyo nije nifahamishwe vizuri pengine ni kutokufahamu kwangu tu, lakini kunanipelekea kwamba sisi sasa ndio tunarudi

nyuma zaidi ya hapa tulipo. Kama tunaanza kutoka katika upande wa demokrasia sasa tunarudi nyuma katika ule upande ambao kila mtu ndio anatoka anakuja huku kidogo inanipa mashaka na ningependa hili niondoshewe wasi wasi wangu isiwe inatuelekeza huko

Sisi kwa kiasi fulani tumeona si vizuri kuwa na utawala kama wa kikoloni wa kisultani ambako ndiko tulikotoka. Lakini leo kama sheria zetu zinatuelekeza kidogo kidogo hatua kwa hatua kurudi huko nadhani tuangalie mara mbili.

Mhe. Spika, mimi nataka nikubaliane sana na ninakaribia kuunga mkono mia kwa mia lakini tu nipate maoni ya jinsi gani Mhe. Waziri anayachukua maoni yetu pamoja na mengine mengi ambayo yametolewa hapa kuhusiana na upande wa pili wa shilingi unaangaliwa vipi, ili tuone kwamba kipengele cha katiba ya nchi hii kinakwenda sambamba na sheria hii. Vyenginevyo itakuwa hii sheria ni batili kwa sababu itakuwa inapingana na hiki kipengele cha 12 (1) nafikiri mpaka (6) ambacho ndio katiba tunayoendelea kuitumia.

Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na ningependa sana na ningemsihi sana Mhe. Waziri ili sheria yake ipite bila ya matatizo. Kwa sababu kimsingi ni jambo zuri lakini lazima shilingi yake aigeuze upande wa pili na tuweze kuona ameyazingatia kiasi gani. Ahsante.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, *Bismillahi Rahmani Rahiym*. Mhe. Spika, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana baada ya kipindi kirefu cha mapumziko ya Baraza. Ni ukarimu wake tu hatukumlazimisha akatuwezesha tukaweza kukutana tena baada ya muda huu.

Mhe. Spika, nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na nawashukuru walioleta mswada na waliouchangia. Lakini zaidi namshukuru Mhe. Waziri anayehusika na mswada huu kwa kutufanyia semina akatuelimisha vya kutosha kuhusiana na mswada huu na tukaweza kugundua kasoro zilizomo na uzuri uliomo katika mswada huu. Kutokana na semina hiyo uelewa wetu wa mswada umekuwa mkubwa zaidi kuliko tulivyokuwa tukiuelewa mwanzo. Kwa sababu uelewa wetu umekuwa mkubwa zaidi basi hata michango yetu inakuwa mikubwa zaidi kuliko ambavyo tungechangia kama hatukuelimishwa.

Sasa Mhe. Spika, kwa maoni ya jumla kabla sijaanza katika kuchangia sehemu moja moja ya mswada huu yamenijia tu mawazo kuwa huu mswada unataka kufanya kama vile wazee walivyokuwa wakifanya zamani. Watu wazima wakikaa pahala na mtoto akakaa, mtu mzima mmoja akaponwa basi hupigwa mikwaju yule mtoto, kumbe sie aliyefanya wala hana kosa lolote lakini nini analipa mtu mzima.

Mhe. Spika, huu mswada naona kama unaelekea katika mantiki hiyo kuwa mtu mzima ni serikali na raia wake ndio watoto, sasa akiponwa asiambiwe mtu mzima kama mzee mbona hivi, hapana apate mtoto bakora kidogo. Kwa ujumla hivi ndio ilivyonijia dhana nzima ya huu mswada tunaoujadili.

Mhe. Spika, nikiendelea labda yatajitokeza kidogo kidogo hayo niliyotangulia kuyasema. Labda nianzie pale kwenye kifungu cha kushtakiwa serikali kwamba anayeshtakiwa katika serikali ni Mwanasheria Mkuu na si mtu mwengine. Lakini katika kifungu cha 15 anayetakiwa alipe si Mwanasheria Mkuu, anaweza akatakiwa Katibu Mkuu, anaweza akatakiwa Mhasibu kulipa, lakini wale sio walioshtakiwa aliyeshtakiwa ni Mwanasheria Mkuu.

Sasa je, haionekani kuwa anayeshughulikia kesi ni mtu mwengine haidhuru ni serikali hiyo hiyo moja na anayepaswa kulipa ni mtu mwengine. Kwa hivyo, huyu anayepaswa kulipa kwa sababu sie aliyeshughulikia kesi, ule umuhimu wa kulipa yeye atauona. Kwa sababu hakupanda yeye kizimbani wala sie yeye aliyefunguliwa shtaka, kwa hivyo na umuhimu wa kulipa anaweza asiuone. Lakini yule aliyeshtakiwa yeye anaweza akaona umuhimu wa kulipa kwa sababu ndie atakayeona kesi imekwendaje, kuna mambo gani yanayomhusu moja kwa moja yeye lakini huyu hayaoni yote yale. Ndio maana Mahakama zinatoa uamuzi hapo nyuma kabla ya sheria hii, lakini uamuzi ule ulikuwa unashindwa kutekelezwa.

Kushindwa kule si kwa kushindwa kutekelezwa kwa sababu serikali ilikuwa haina pesa, ilishindwa kutekeleza kwa sababu ya kudharau. Sasa unapofika pahala ukadharau kile ambacho ni mhimili mmoja wa nchi na ambao ni mhimili uliowekwa kutoa haki, mhimili ule ukaagiza kuwa haki hii itolewe apewe fulani lakini bado mhimili mwengine ukapuuza. Kwa kweli tunakwenda katika njia mbaya isiyostahiki.

Mhe. Spika, kutokana na hayo yaliyotokea inaonekana sasa tunayatafutia vichochoro, yatakapotokea tena tuwe na vichochoro vya kupita. Sasa vichochoro hivi vitasaidia, sisemi kama havitasaidia, lakini msaada wake ni leo na kesho, kesho kutwa msaada huo haupo. Aliyesababisha ukosefu wa haki ya mtu haki ile ajue atakwenda kuilipa yeye pahala fulani. Hili naomba ieleweke kwa sababu watu wengi wanaelewa kuwa serikali ikishazuia hiki kitu hakupewa mtu ile haki itawajibika serikali. Huko haiwajibiki serikali, huko atawajibika aliyehusika ndani ya serikali kulifanya lile.

Kwa hivyo, hili Mhe. Spika, nimesema nitoe kidogo indhari ili sisi tunaofanya shughuli humo ndani ya serikali tujue kwamba kila haki utakayomnyima mwenzako, basi haki ile huko haiendi kuhojiwa serikali utahojiwa wewe

uliyekuwa haki ile uitoe. Sasa hili Mhe. Spika, nilitaka kidogo nilielimishe ili tuweze kwenda vizuri watendaji wa serikali.

Lakini Mhe. Spika, nikirudi katika suala la Mahakama na utoaji wa haki na mswada huu. Mhe. Spika, kwa kuwa Mahakama kikatiba, kisheria ndio iliyopewa kazi ya utoaji wa haki, basi ilikuwa iachiwe kazi ya kutoa haki. Nadhani kwa mswada huu Mahakama imepunguziwa madaraka yake.

Mhe. Spika, twende kwa mfano lile suala lililozungumzwa kuwa ikiwa mali anayestahiki ni haki ya Mhe. Haji Faki Shaali, ikiwa ni ardhi, mtu au nyumba. Lakini Mahakama imethibitisha kuwa Mhe. Haji ndie mwenyewe, ndie mmiliki halali. Basi iseme tu Mahakama kuwa huyu ndie mmiliki halali? Kwani Mahakama ikishasema huyu mmiliki halali ndio imeshaamua. Kwani kesi iliyopelekwa ni ya kutafuta nani mwenyewe na nani si mwenyewe? Kesi iliyopelekwa si ya kumtafuta mwenyewe ni nani. Kesi iliyopelekwa ni ya kudai mtu haki yake apewe. Sasa Mahakama ikishaona kuwa hii mali ni ya fulani mimi nadhani haijamaliza kazi haijatoa hukumu bado, imeona kitu kimoja lakini hukumu bado haijatoka kwa sababu lililodaiwa sio hilo, lililodaiwa ni haki.

Kwa hivyo, pale Mahakama ndio inapotakiwa itoe hukumu. Hii mali ni ya fulani je, ifanywe nini sasa? Kitu gani kifuate kuhusiana na mali hii na mwenyewe? Hili nafikiri ndio linalotafutwa watu wanapokwenda Mahakamani, hawatafuti tu kujulikana mali hii ni ya nani.

Sasa kuweka kifungu cha sheria kwa kuwa Mahakama iweze kusema tu kuwa mali hii mwenyewe nani lakini baada ya hapo isiendelee kusema kufanywe nini. Kwa sababu kuna hukumu nyingi ndani ya mali ya mtu. Inaweza Mahakama ikasema hii mali yake arudishiwe, inaweza Mahakama baada ya kusikiliza mambo yote yale ndani ya kesi ikaona hii mali ni ya fulani. Lakini kutokana na umuhimu wa utumizi wake kwa maslahi ya umma kama serikali ilivyoieleza Mahakama, Mahakama ikaona kuwa hii asirudishiwe mwenyewe lakini apewe fidia. Wakatafutwa watu wa kufanya thamani ya fidia kiasi gani apewe kwa mujibu wa sheria.

Mahakama iamue kuwa hii mali ni ya fulani lakini kutokana na umuhimu wake katika taifa na shughuli zinazotaka kufanywa, basi hii mali asirudishiwe mwenyewe lakini apewe fidia ya kiasi fulani. Nafikiri hapo Mahakama itakuwa imefikia pahala imeamua. Nadhani hapo bado serikali itakuwa haijanyanyaswa wala haijawekwa pahala pabaya, lakini pia itakuwa Mahakama imepata nafasi yake ya kutoa haki. Kwa sababu haki inaweza ikatoka katika rangi mbali mbali lakini haki na itakuwa imetoka.

Kwa hivyo, nadhani kuna haja muhimu sana ya Mahakama bado kupewa nafasi yake ya kutoa haki. Sasa Mahakama itatoa vipi haki ile itategemea kesi itakavyoendeshwa na Mahakama itakavyoona ndani ya hiyo kesi yenyewe. Ninahakika kuwa Mahakama hata siku moja haitanyanyasa serikali na pia itaangalia umuhimu wa maslahi ya taifa.

Sasa kama ni hivyo basi ilikuwa kuna haja ya Mahakama kuachiwa isikomee kwenye kumsema mwenye mali, lakini ikomee kwenye kusema mwenye mali apewe nini au afanywe nini. Mhe. Spika, hili ni moja katika mambo ambayo nadhani kuna haja ya kuingizwa katika sheria hii.

Mhe. Spika, hapo hapo kuna suala la kwamba kutakuwa na kanuni za uharakishaji malipo. Naomba labda niseme yale maneno niliyoyasikia siku moja “Ikiwa kilemba kinroa je, nkuti uhali gani?”

Yaani wewe unakwenda ndani ya mto umevaa seruni yako au shuka na juu una kilemba, kilemba kikaroa kilichoko juu je, hii shuka iliyoko chini. Sasa hii ni sawa sawa na kusema kuwa ikiwa sheria yenyewe imezuia isifanye habari hizo je, kanuni. Nafikiri hili nalo bado hatujafanya jambo la maana. Kwa mambo mazito kama haya yasingewekwa kwenye kanuni yangebaki kwenye sheria yenyewe.

Kwa hivyo, hili mimi nasema kuwekwa kwenye kanuni si pahala pake, pahala pake ni kuwekwa kwenye sheria. Likiwekwa kwenye sheria ndio litakapofanya watu wawajibike. Tatizo la kutowajibika ni kwa sababu watu wanajua kama mimi sifanywi kitu. Mtu akishajua mimi sifanywi kitu hawajibiki ikiwa si muadilifu. Baadhi ya watu si waadilifu wanatumia hisia zao binafsi katika shughuli zao za kazi. Sasa hizi hisia binafsi lazima tuzidhibiti ili wasiipate ile nafasi ya kutumia ule unafsi wao katika kuwakandamiza wenzao. Mhe. Spika, hili naona nalo ni miongoni mwa mambo muhimu ambayo yangezingatiwa na sheria hii.

Mhe. Spika, kuna mambo ambayo yaanzia kesi kwenye Mahakama ya Kadhi kwa mfano mambo ya mirathi. Mhe. Spika, Mahakama ya Kadhi inaweza ikenda pahala imeshaamua sasa mirathi hii iwe hivi. Lakini katika mirathi ile kabla haijarithiwa serikali baadae ikaja ikaona hapa kuna kiwanda cha sabuni tunataka kukijenga. Ikachukua ikajenga kiwanda cha sabuni wenyewe wakidai hawajalipwa watakwenda Mahakamani.

Sasa huku kuna uamuzi wa Mahakama ya Kadhi haujatekelezwa, huku sasa kuna kesi nyengine inafunguliwa ya kudai eneo lile. Hatuoni kama bado kuna mambo tunayachanganya changanya hapa. Maana yake unapoangalia mambo usiyaangalie kwa ufinyu kidogo yaangalie kwa upana wake, hiyo itakuwa kesi

ndani ya kesi, sasa tutakuwa na kesi mbili, kesi moja ya urithi, kesi moja ya kudai kwenye serikali. Sasa hapa tutakuwa na kesi mbili tofauti, itakuwa kesi ndani ya kesi.

Mhe. Spika, litakapotokea hilo tunafanya nini. Humu haijaeleza kwenye sheria. Naomba na hili nalo lizingatiwe katika sheria hii, itakapotokea kesi ndani ya kesi ya aina hii itakuwaje.

Lakini Mhe. Spika, ukiachilia mbali suala hili la kesi ndani ya kesi kuna mambo mengine ambayo lazima nayo yazingatiwe. Mahakama inaweza ikaamua, ikishaamua ikawa utekelezaji ndio haukufanywa. Je, baada ya hapo tunafanya nini na tumeshaambiwa Mahakama hii iseme tu kama hii ni haki ya fulani. Baada ya hapo yule mdaiwa serikali kwa mfano hajalipa na kule Mahakama tumeshaizuia isitoe uamuzi mwengine, yule mwenye haki yake aende wapi. Mahakama imeshasema kama haki ni yake, serikali haijamlipa wala haijaelekea kama itamlipa, sasa je, mtu yule kuipata haki yake aende wapi.

Lakini pia tuangalie hapa hapa kuwa haki unapoichelewesha unasababisha matatizo mengine mengi. Haki unapoichelewesha unamuumiza kimwili, kiakili na katika kila hali yule uliyemcheleweshea ile haki. Kwa sababu pengine kile kitu yeye kakitegemea katika maisha yake wewe umekizuia, maisha yake yataharibika ikiwa wewe ndio sababu. Sasa hili nalo Mhe. Spika, ilikuwa lionekane ijulikane kama ndio hiyo imeshaamuliwa na haikutekelezwa je, tunakwenda wapi. Likijulikana hilo angalau pengine tutajua tufanye nini.

Mhe. Spika, kuna suala zima hili la kesi zilizokwishahukumiwa nyuma lakini hazijatekelezwa na kesi ambazo tayari ziko Mahakamani zinaendelea kuhukumiwa lakini bado hazijatolewa hukumu. Kwa mujibu wa sheria hii utekelezaji utafuata sheria hii mpya. Ninalojiuliza na ninaloliuliza ni mantiki gani inayosababisha kesi iliyokwishahukumiwa miaka miwili nyuma na ilikuwa ilipwe miaka miwili nyuma haikulipwa kwa makusudi, leo tuje tuseme ilipwe kwa mujibu wa sheria hii ya leo. Ni mantiki gani.

Maana lazima tuwe na mantiki. Kesi hii imeshahukumiwa miaka miwili nyuma, malipaji yake ilikuwa yafanywe miaka miwili nyuma kama Mahakama ilivyoamua, hayakulipwa tunangojea sheria mpya. Hatuoni kama hiyo ni kwenda kinyume na sheria. Mbona tunataka kulazimisha kitu ambacho ni kinyume na sheria.

Sasa hili nadhani hatuwatendei haki waliokwishahukumiwa, wala hatuwatendei haki ambao kesi zao zinaendelea kwa sababu kesi zimefunguliwa chini ya sheria nyengine ilikuwa zihukumiwe chini ya sheria ile ile iliyofunguliwa. Hii

itumike kwa kesi zitakazofunguliwa chini ya sheria hii. Mhe. Spika, hili nalo nadhani lingestahiki kuzingatiwa na katika mazingatio hayo likarekebishwa ili kulinda haki.

Mhe. Spika, haki kucheleshwa ni haki kunyimwa. Ndivyo walivyosema wataalam wa sheria, mimi nimesema Kiswahili lakini wao wamesema Kiingereza. Sasa tunapocheleweshe haki maana yake tunamnyima yule mwenye haki.

Kwa mfano, mtu anaidai serikali milioni 5 tu, ni mfanyabiashara mdogo anapeleka vitu kidogo tu pengine hospitali na skuli. Lakini mtaji wake ndio ule umemcheleweshea kumlipa na yule ndie aliyepatikana wa kupeleka vitu vile hakupatikana mwengine mwenye pesa nyingi. Unapomcheleweshea haki yake maana yake ni kuwa umemnyima haki yake kwa sababu angefanyia biashara zile pesa angepata na faida nyengine zaidi akaongezea katika mtaji wake na akapata kuendeshea maisha yake.

Kwa hivyo, kweli hawakusema uongo hawa, waliosema kuwa haki kucheleweshwa ni haki kunyimwa. Kwa sababu sehemu ya haki itakuwa tayari umeshamnyima haipati tena ile, wewe ukimlipa unalipa zile zile ulizokopa hutamlipa kingine. Unapochukua vitu hamkatibiani kuwa utamlipa na riba, unamlipa pesa zile zile ulizokopa. Lakini umemnyima kwa sababu angeweza kuzifanyia kazi zile akapata zaidi kuliko zile. Kwa hivyo, bado haki yake itakuwa umemnyima kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, katika kufungua kesi kuishtaki serikali, tunasema anashtakiwa Mwanasheria Mkuu. Lakini serikali kufungua kesi si lazima afungue Mwanasheria Mkuu, anaweza akafungua Mwanasheria Mkuu au anaweza akafungua mtu mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Mwanasheria Mkuu afungue.

Sasa kwa nini hatulifanyi likawa sare. Kuwekewa kesi Mwanasheria Mkuu anaweza akamwambia Katibu Mkuu wa Wizara, anaweza akamwambia Mkurugenzi fungua kesi kuhusiana na jambo hili. Basi kwa nini na upande huu wa kushtakiwa serikali nao pia hatuweki wazi tu ikawa na ofisa mwengine yeyote anaweza akashtakiwa kwa niaba ya serikali. Kwa sababu kuishtaki serikali ofisa yeyote yule akishapewa ruhusa anashtaki. Kwa hivyo, kushtakiwa serikali nayo pia tuiwekee nafasi ashtakiwe yeyote yule ambaye kahusika moja kwa moja na lile suala.

Sasa baada ya kushtakiwa huyo aliyeshtakiwa Mwanasheria Mkuu kazi yake ni kwenda kuitetea kesi Mahakamani. Itakuwa imeshtakiwa ile ile serikali, ikiwa kashtakiwa Mwanasheria Mkuu, ikiwa kashtakiwa Katibu Mkuu imeshtakiwa

serikali na kazi ya Mwanasheria Mkuu kwenda kuitetea serikali Mahakamani. Mhe. Spika, hili nalo kuna haja lifanyiwe kazi vizuri sana.

Mhe. Spika, mwisho naomba niseme kwamba katika mambo yote tunayoyafanya tukiwa ndani ya serikali, tukiwa nje ya serikali tunapaswa kupendana. Katika kupendana Mhe. Spika, ni kupendeleana mema. Katika kupendeleana mema ni kuweka sheria nzuri kwa upande wa serikali. Kwa sababu tutakapoweka sheria nzuri maana yake tumempendelea na yule tuliyemuwekea sheria nzuri. Lakini tutakapoweka sheria ya kumbana mtu katika mambo ya haki, maana sisemi kila sheria impendelee mtu, hapana jambazi usimpendelee. Lakini katika haki yake mtu basi tumpendelee.

Serikali tuilinde kwa upande wake, lakini ili serikali tuilinde nayo ijilinde. Serikali kujilinda sio kwa sheria bali ijilinde kwa kuwajibika na kwa vitendo vizuri kuwafanyia raia zake.

Mhe. Spika, kwa maneno haya niliyoyazungumza mwisho nakushukuru, ahsante.

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Mohamed Ali Salim kuwa mchangiaji wa mwisho kwa kipindi hiki. Jioni mchangiaji wa kwanza atakuwa Mhe. Hamad Masoud Hamad.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia mkutano huu wa kumi na tisa kuwa wajumbe wote tuliokuwepo katika mkutano wa kumi na nane tulikuwa hai na wazima na leo hii Alhamdulillah tuko vile vile.

Vile vile nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa jioni hii kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza. Mhe. Spika, baada ya kuisoma sheria hii au mswada huu na semina ya jana ya wajumbe wako wa Baraza ambapo semina hiyo kulikuwa na wataalamu wa sheria waliobobea na kwa kiasi kikubwa michango inayotoka leo ilitokana na uwasilishaji wa wanasheria wetu, ili sisi wajumbe tunaotakiwa tufanye *final decision* ya mswada huu tuelewe vizuri. Alhamdulillah ni imani yangu kwamba tumeelewa.

Lakini mimi nilikuwa ninatafakari ni kwa nini mswada huu ukaja katika siku hizi, nafikiri mswada huu umekuja kwa sababu ya mambo ambayo yametokea ya madai makubwa makubwa serikali kudaiwa na ama waliotiliana mkataba nao au waliofungana katika mambo mbali mbali.

Mhe. Spika, hivi karibuni kumekuwa na taarifa kwamba serikali baada ya kupelekwa mahakamani, mahakama imeamua serikali ilipe na ni baada ya muda huo uliowekwa na mahakama serikali kushindwa kulipa na kwa hivyo, baadhi ya mali za serikali yakiwemo magari, majumba na kadhalika kupigwa tanji au kuwekewa matangazo kwamba mali hizi sasa zinauzwa.

Lakini jengine ambalo ni la siku nyingi kabisa ni hili la mkopo wa mchele wa zaidi ya miaka sijui 20 au zaidi, ambalo lilihusiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Lemtong.

Mhe. Spika, yote haya yamekuja kwa sababu kubwa moja, serikali ilishindwa kutii hukumu za mahakama. Hapa sasa mswada huu wa sheria, wengine akiwemo Maalim Moh'd Ali Salim na mimi mwenyewe wanaofananisha kwamba ni sawa na mtoto aliyetoa upepo mbele ya watu wazima. Naomba samahani. Ni sawa sawa na mtu mzima aliyetoa upepo mbele ya wenzake lakini kukawa kuna watoto. Sasa anayelaumiwa na ikiwezekana hata kufukuzwa na kupigwa vikofi ni yule mtoto.

Sasa hii nataka niiunganishe kidogo na hadithi moja ya busara. Huyu mtoto yeye hana kosa, lakini kwa sababu lile kosa kafanya mzee na ni kosa la kashfa, ingawa sio kashfa maana yake kutoa upepo kumeumbwa na inategemea mazingira, wengine wanaharisha kwenye mabasi, ni watu wazima na ni mambo ya kawaida. Lakini sasa hili linaonekana ni kosa na mtu mzima hawezi kutoa upepo mbele ya wenzake. Kwa hivyo, mzigo huu mzito atwikwe mtoto.

Nataka niongeze hadithi moja ni ya hekima vile vile ambayo sisi kama wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni vizuri nayo tujuwe. Huyu huyu mtoto, kuna mzee mmoja alikuwa na mwanawe anampenda sana ni kidonda chake hasa, kwa hivyo kila palipokuwa na shughuli kubwa kubwa huwa anamchukua. Siku moja mtoto huyo akachukuliwa na baba yake kwenye karamu, kwa bahati karamu ile hakukuwa na watoto, ikabidi sasa katika sahani watu watatu katika kujipanga basi huyu mtoto ikabidi achanganyike na baba yake na wazee wengine.

Sasa katika adabu za kula, huyu mzee kwa sababu anakula na wazee wenzake lakini ana mwanawe ambaye hangeweza kumtenga na hakuna sahani ya peke yake kwamba mpunguzieni, basi mzee akamnong'oneza mwanawe, mtoto huyu huyu ambaye hupigwa makofi au hutukanwa au hufukuzwa akisingiziwa kuwa

katoa upepo kumbe siye, sasa mtoto huyu akanong'onezwa na baba yake kwamba mwanangu tunakula na watu wazima, nakuomba tafadhali jiheshimu, uzingatie adabu za kula, ukila kula usoni kwako, ukila usitie vidole vyote ndani ya mdomo na mambo mengine yote na jengine ni kwamba usije ukatowea kama hujatowezwa. Kutoea nadhani mnafahamu nyote, sio Kiswahili kigeni hiki.

Basi wazee wakaendelea kula pilau yao na pilau ilikuwa na nyama hiyo, tonge nyama. Sasa wanakula wanakula wazee wanapiga matonge na huku wakichukua vipande vya nyama, yule mtoto hajapewa chochote na kaambiwa asije akagusa nyama kama hajatowezwa. Ndipo alipoona mtoto kwamba nyama inakwisha, hajapata chochote na yeye akamnong'oneza baba mtu, akamwambia baba nitoweze au nitatoa upepo.

Yupo mwalimu wangu Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, atanikosoa nitakapokosa. Sasa baba mtu akaghumiwa, hakuna kashfa kama hii mwanangu leo ambaye nina amini ana adabu za kutosha, leo napewa changamoto kama hii. Kama sikumtoweza atatoa upepo.

Mhe. Spika, nikisema kujamba sio matusi. Lakini kule Pemba kujamba ni kule priiiii. Lakini yeye hakumwambia kujamba, nimeibana kidogo. Alimwambia nitoweze au nitafusa. Kufusa ni kutoa ushuzi ambao hakuna atakayesikia lakini nyote mtaondoka. Baba mtu akaone hii ni kashfa kubwa leo. Kilichotokea akatafuta *the way forward*, akachukuwa kipande kimoja kikubwa akamtupia paa.

Kwa hivyo, naunganisha na pale Maalim Moh'd Ali Salim alipofika. Sheria hii iko siku, huyu huyu mtoto ambaye tunamsingizia atakuja kukupa sharti ambalo huna vya kufanya isipokuwa kumridhia.

Mhe. Spika, sheria hii haikuzingatia hata kidogo utawala bora, hii imezingatia utawala kwa sheria dhidi ya utawala wa sheria. *Rule of Law* na *Rule by Law*. Sisi tuna wizara nzima yenye waziri, wana sheria waliobobea na inayohusiana na utawala bora, hivi kweli sheria hii inatupeleka huko. Wakati tunaijadili sheria hii Mhe. Spika, na hata kabla sheria hii haijaletwa ilikwishaenea, vipi ilienea mimi sijui. Lakini ilikwishaenea kwamba Serikali ya Zanzibar inatunga sheria ambayo imejilinda kupita kiasi na imenyima sana haki ya wengine ambao sio serikali. Yakiwemo mashirika, taasisi na hasa wafanyabiashara wa nje na hata wa ndani.

Mhe. Spika, unaweza ukajiwekea ulinzi mpaka ule ulinzi ukawa ndio kifo chako. Mfano mdogo upo. Siku hizi majumba mengi sana mazuri na ya fahari, yamejengewa mageti ya vyuma utafikiri jela. Imeshatokea hapa sio mara moja

wala mbili, mtu na wanawe. Sitaki kukumbushia hili, lakini nataka vile vile mkumbuke. Mtu na wanawe wamo katika nyumba, kwa kuogopa wezi wakajitia jela, jela kwa maana kwamba mageti yale ya vyuma, milango imewekwa makufuli. Mhe. Spika, kwa bahati mbaya kwa athari za umeme kama tulivyoambiwa ikaungua, watu wakakurupuka kitandani mageti ya vyuma, hakuna awezae kutoka nje na kilichotokea ni msiba mkubwa wa baba na watoto kufariki. Kwa hivyo, mimi natahadharisha kwamba *anything excessive is dangerous* na hapa mimi nasema serikali imejikinga kupita kiasi.

Mhe. Spika, hebu fikiria kwamba wakati serikali inashtakiwa na inahukumiwa serikali hiyo hailipi, sheria iliopo sio hii tunayojadili, lakini hiyo ambayo inatumika hadi sheria hii itakapoanza serikali inashtakiwa na ilikuwa inashtakiwa na imeshtakiwa. Mahakama ikatoa hukumu dhidi ya serikali kwamba walipe na haikulipa. Haya je leo, sheria hii ambayo serikali itashtakiwa lakini hata ikihukumiwa suala la kulipa, maana utekelezaji ni vile ambavyo umejiwekea kinga.

Mhe. Spika, mimi kwa maneno mafupi naiona sheria hii ni ya kidikteta sana. Kwa manufaa ya serikali hii na sifa zake inayoheshimu haki za binadamu na hapa juzi Alhamdulillah Rabilallamina, watu wote wa nje na ndani walivutika na haya mambo ambayo yanaendelea ya maridhiano. Lakini leo sasa maridhiano ni sawa sawa na kwamba tumefunga dirisha halafu tunafungua mlango. Mhe. Spika, sisi tunaliona ni dogo hili lakini ni kubwa, ni kubwa kwa kitaifa na kwa kimataifa. Inapokuwa Shirika la Kimataifa au hata la Kitaifa au taasisi yoyote ile inaogopa kuingiliana na mikataba ya kibiashara au yoyote ile ambayo inahusu suala la hatimaye pengine kufikishana mahakamani na kwa sababu suala lenyewe litakuwa limefanyika hapa, lakini sheria hapa serikali itashtakiwa kwa *The Hague* lakini hapa limefanyika. Kwa hivyo, mashtaka yafanywe hapa.

Mhe. Spika, mimi nafikiri waziri atafakari vizuri kabisa ili mswada huu vyovyote itakavyokua utakapopita, basi wale ambao walikuwa na imani na serikali hii katika mambo ya biashara, hata kama bado wanadai. Maana yake bado wanadai lakini bado wanaimani, lakini hii itapunguza na itaondoa imani kabisa. Sasa tuangalie inapokuwa mashirika ambayo mlikuwa mnafahamiana, mnaelewana na mnakopeshana hawana tena imani kwa sababu ya mswada huu tutakuwa tunafanya nini.

Lakini Mhe. Spika, niende mbali zaidi, mswada huu kama walivyosema wenzangu hauna unafuu kabisa hata kwa wananchi wa kawaida dhidi ya serikali. Sisi hapa, hawa wanasheria wame-*draft*, sisi tunafanya maamuzi hapa, tunaweza tukafanya maamuzi kwa mujibu wa sheria na kanuni zetu, mswada

huu waziri rudi nao, tukikubaliana kwamba waziri rudi nao, basi atarudi nao tu. Tukisema hapa tulipofika unamalizika tunaukubali, basi ni hivyo.

Kwa ufupi Baraza hili maamuzi yake ni ya mwisho, ingawa *subject to accept* ya Rais, lakini hapa ndio pakubwa, Rais keshauona huu, umeshapita Baraza la Mapinduzi na yeye ndio mwenyekiti. Kwa hivyo, sisi hapa marekebisho tutakayofanya pengine ni madogo, lakini marekebisho ni lazima yawe na umuhimu ili kuhakikisha kwamba hawa ambao wametuleta hapa wasije kuona kwamba wametupa ihsani tunawalipa nukhsani. Huyu mwananchi wa kawaida haumsaidii chochote kabisa, na hivyo kweli hii ndio kazi yetu ya kupewa ihsani tukalipa nukhsani.

Mhe. Spika, sote hapa au wengi wetu sisi hapa kila mtu saa hizi roho inakwenda kama chura, mwili uko hapa, lakini akili iko jimboni, isipokuwa Mkuu wa Mkoa, Mhe. Moh'd Ali Salim na wewe Mhe. Spika. Lakini vile vile na wewe unatutegemea sisi, kwa hivyo na wewe roho yako hivyo hivyo iko kwetu sisi na sisi roho zetu ziko majimboni. Hivi kweli hawa ambao roho zetu ziko kule na mwili uko hapa, maana yake hapa Zanzibar hakuna siri kiasi hicho, kabla mswada haujaletwa hapa basi watu wote wanajua kwamba kuna mswada unaokuja kuwabana watu na serikali kujikumbizia na kujilinda kupita kiasi. Sikwambii tukishajadili hapa. Hapa patajadiliwa, pataamuliwa. Lakini maamuzi haya ukiyachukua ukenda huko nje maamuzi yalioko nje ni tofauti, *very destructive*. Kuna mambo hata hayajajadiliwa hapa, lakini huko majimboni na mitaani yapo. Sasa mimi nina washauri sana wenzangu na zaidi waziri akaufanyie kazi kabisa. Asiurudishe, kwa sababu hapa hapa panaweza pakafanywa maamuzi ambayo kweli yataridhisha, serikali itapata fungu lake hivyo hivyo kwa kujilinda na wananchi watakuwa na imani kwamba kumbe serikali unaweza ukaingiliana nao kabisa katika masuala haya.

Mhe. Spika, kama mtu hajiheshimu maana yake anakaribisha watu wasimuheshimu. Serikali kutolipa madeni haya kwa visingizio mbali mbali ni kutojiheshimu, mfano huo nautoa. Kwa hivyo, serikali kushtakiwa sio kuvunjiwa heshma, aliyekushtaki umemkaribisha akushtaki. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba sana wajumbe wako tutafakari katika suala hili ambalo sio dogo, ni kubwa katika nchi hii na ni kubwa nje ya nchi hii.

Mhe. Spika, kwa kifupi ni kwamba ingekuwa serikali inalipa madeni yake basi isingeshtakiwa. Mhe. Spika, sio kwamba serikali hailipi, lakini fedha zinaingizwa kwamba hizi lipeni hapa, serikali hiyo hiyo na waliopewa dhamana ya kulipa wanazi- *divert* fedha zile, deni linakuwa kubwa.

Mhe. Spika, hivi ninavyokuambia kuna kampuni za kienyeji kabisa zimeuliwa na serikali, kwa sababu gani, kwa sababu hazilipwi. Wewe mtu atakwenda

kuingia katika madeni ya milioni 120 kampuni ya kawaida, yenye waajiriwa hawafiki pengine hata 20, halafu unachukua miaka miwili au mitatu, halafu kampuni hiyo haina hata tamaa ya kulipwa, hivi kampuni hiyo itakua, haiwezi kukua. Chanzo cha kuuwa kampuni ile ya kienyeji ni nini, itakuwa ni serikali. Kwa hivyo, mimi nafikiri jambo kubwa ilikuwa ni serikali kukaa kitako ikasema jamani kwa nini kunatokea haya ya serikali kushtakiwa. Ni kwa sababu serikali hailipi, njia ziko nyingi za kufanya haya.

Mhe. Spika, zamani utaratibu wa kulipa mishahara Mhe. Waziri jirani yangu na ni rafiki yangu, anajua, amebadilisha utaratibu mzima wa malipo. Hivi sasa kuna *central payment office.* Zamani fedha za mishahara zilikuwa zinakwenda tu, mara zimeshaibiwa, mara hazipatikani, hawa wamelipwa nusu, huyu ametiwa kabali. Lakini leo hayo yameondoka. Sasa kwa madeni hayo ya serikali na makampuni katika *contract* zote. Mimi nafikiri serikali ingekaa kitako ikaona kwamba yoyote anaye-*contract* na mtu, iwe ni kampuni, iwe ni shirika na iwe ni taasisi yoyote ile, basi *payment* tunafanya sisi Wizara ya Fedha na Uchumi na hapo Wizara ya Fedha haiwezi ku-*divert* fedha zile kama zile za Mkuu wa Mkoa au za Mkuu wa Wilaya au za idara moja kwenda kwengine. Kwa hivyo, mtu anajua, au shirika linajua au *contractor* anajua kwamba mimi najenga nyumba hii, lakini malipo yangu sio kwa Mkuu wa Mkoa, malipo yangu sio kwa Mkuu wa Wilaya ila malipo yangu ni kwa Waziri anayeshughulika na mambo ya fedha basi. Naamini watu wangelipwa, makosa madogo madogo yanayotokea yangevumilika na mswada huu Mhe. Spika, usingeletwa.

Mhe. Spika, mimi nasema kitu kizuri hata kama ni kikongwe sana kama ni kizuri kuna haja gani tena ya kukibadilisha. Tunaambiwa kwamba sheria hii ipo kwa miaka mingi sana na wenzetu nchi jirani wamebadilisha wamekuwa na sheria ambayo imerekebisha sheria zao katika suala hili. Lakini mimi nasema kama mwendo huu ni mzuri hata kama ni mkongwe kiasi gani kuna haja gani ya kubadilisha.

Mhe. Spika, mimi nashauri kuna haja ya kubadilisha mambo madogo madogo, na ni utaratibu wa *system* ya serikali yenyewe. Kwa hivyo, bado mpira uko kwa serikali, ufanye utaratibu wa kuweza kulipa. Lakini vinginevyo nasema tena kwa maoni yangu, hii ita-*jeopardize* sifa ya serikali ambayo sasa hivi tunaelekea mahali pengine kupya na kuzuri zaidi. Kwa hivyo, tusiwe na *positive 10* tukawa na *negative 12* tukawa tuna *negative 2, this is very unfair.* Mhe. Spika, sitaki niseme sana, lakini nashauri tena na tena.

Mhe. Spika, la mwisho ni suala la yeyote ambaye amefanywa jambo na ikabidi ashtaki kwamba lazima awe anamshtaki Mwanasheria Mkuu wa serikali. Mhe. Spika, hiki ni kichekesho, mimi nikijua kwamba hata kama nikifanya kosa

bakora hainipati, atakayepigwa ni mwengine sasa mimi naogopa nini basi. Mimi hata nikifanyaje sishtakiwi bwana, mimi ni *untouchable.* Hapa nafikiri kuna kasoro, jamani unaposikia mkurugenzi kashtakiwa wa idara hii, huyu mkurugenzi mwenyewe haidhuru ni cheo lakini ni mtu, keshafuja mali ya umma, keshaiba na kila kitu hakulipa serikalini, serikali inashtakiwa. Huyu huyu ambaye ni Mkurugenzi wa Idara X ameshtakiwa, huyu halali tena, anakaa anatafakari, anakwenda kwa watu wenye mikia na vibuyu, wanakwenda mapangoni. Ndio, kwa sababu anajua mwisho wa mzigo huu utamuangukia yeye, alichokijenga, alichokichuma na alichokinunua anaanza kukiuza. Lakini leo Mwanasheria Mkuu peke yake ndio anashtakiwa wala hajafanya kosa. Tusisahau Mwanasheria Mkuu ni Mwanasheria Mkuu ana jopo la wanasheria, sio ajabu kwamba Mwanasheria Mkuu na yeye kwa ufundi wake hivyo hivyo akaona kwamba alaa kumbe kila balaa naletewa mimi hapa. Basi na yeye kila kesi inayokuja anaipiga *ticktack*. Je, ni lini watu watapata haki zao mahakamani.

Mhe. Spika, serikali inashtakiwa, Mwanasheria Mkuu ndiye anayeshtakiwa na ndio serikali. Mwanasheria Mkuu huyo huyo kwamba ni mshtakiwa, lakini huyo huyo anaweka wakili wa kutetea serikali. Jamani mambo haya mmeona wapi. Serikali ni Mwanasheria Mkuu na Mwanasheria Mkuu mwenyewe ana jopo la wanasheria na mwengine utasikia huyu ni *state attorney*, amekuja kuitetea serikali, serikali ambayo imeshtakiwa na huyo, hii ni balaa kubwa na ni kizungu mkuti. Kasoro hii Mhe. Spika, ni kubwa.

Mhe. Spika, mimi nashauri kwamba Mwanasheria Mkuu abaki kama alivyokuwa anatetea kesi za serikali, lakini washtakiwa wawe *identified* kwamba hapa tunamshtaki fulani kwa cheo chake sio kwa jina bila shaka. Lakini nasema kwa sababu kile cheo saa zile kinakuwa *hold* na mtu yule mtu mwenyewe anaweza akafanya mpango kabisa kama ni kurudisha fedha akazirudisha, lakini kwa namna hii kubwa utakalolifanya wewe ni kumfukuza mtu serikalini. Mtu keshatuibia milioni hata ukimfukuza sio ndio utampa muda mzuri wa kufanya shughuli zake.

Mhe. Spika, hofu yangu katika mswada huu ni hiyo na sikutaka kwenda kifungu kwa kifungu, kwa sababu kamati imekwenda kifungu kwa kifungu haijafanya marekebisho ya maandishi, imefanya marekebisho ya hata maneno. Sisemi kwamba naunga mkono mswada huu, mimi nasema pafanywe marekebisho ili wakati wa kuunga mkono kwa pamoja na mimi ninyanyuwe mkono wangu.

La mwisho kabisa namshukuru sana Mhe. Waziri kwa semina ya jana fupi, lakini ilikuwa ndefu sana chai ilikuwepo, pilau na bahasha. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuja kufanya majumuisho juu ya Mswada wetu wa Sheria ya Kuweka Haki na Wajibu wa Serikali katika Kesi za Madai na Utaratibu wa Mwenendo wa Madai Dhidi ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, niwashukuru sana wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia na kuhoji mambo mbali mbali, kushauri, kuuliza na kutuelekeza jinsi ya kuendeleza mswada huu ili uwe bora zaidi na hatimaye sheria hii iweze kufanya kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, naamini wengi wangependa kuchangia lakini nafikiri kama alivyosema Mhe. Hamad Masoud Hamad baada ya semina ya jana, wengi wamefahamu hasa na walichangia leo wametuuliza na baadhi ya masuala tutayaweka sawa na sote tuko pamoja katika suala hili.

Isipokuwa kubwa nataka nilielezee mapema kwamba sisi sio wa mwanzo na wala sio kama tunaiga tu vitu aa! Na sisi kama ni *principle* na mwenzako anafanya jambo jema basi si vibaya kuliiga. Kwa hivyo, hili tayari wenzetu wanalifanya kama nilivyosema asubuhi sisi tumechelewa ndio maana tumeingia kwenye matatizo, kwa sababu tumechelewa.

Kwa maana hiyo, tunapozungumza utawala bora ni kweli wanavyo-*observe* waheshimiwa ni kwamba utawala bora ulikuwa haufuatwi. Mhe. Spika, ni kweli na sasa tunataka tuusimamishe vizuri na baadaye tuufuate sote na wala sio kwa kumuonea mwananchi tu, kwa sababu yeye anao utawala bora kwa upande wake na sisi serikali tunao vile vile kwa ajili ya kutomkandamiza mwananchi.

Sasa hili napenda kulisisitiza sana na kama serikali tunaheshimu sana Mahakama ni muhimili mmoja wa nchi hii pamoja na Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, hatuna lengo la ui-*undermine* Mahakama wala maamuzi yao aa! Isipokuwa tunachosema ni kwamba tunaweka utaratibu mzuri na wala sio kama tuna-*rollout* serikali isishtakiwe laa! Bado serikali itaendelea kushtakiwa, lakini kwa taratibu gani. Kwa kweli haya ndiyo madhumuni makubwa ya mswada wetu.

Mhe. Spika, nimeona nitoe utangulizi mdogo huo na niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote, kama nilivyosema waliopata fursa ya kuchangia ambao kwa jumla walikuwa kumi naomba niwatambue kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin — Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi
2. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji — Waziri Kivuli Wizara ya Fedha na Uchumi
3. Mhe. Rashid Seif Suleiman,
4. Mhe. Haji Faki Shaali
5. Mhe. Ali Abdalla Ali
6. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
7. Mhe. Juma Duni Haji
8. Mhe. Zakiya Omar Juma
9. Mhe. Mohammed Ali Salim na
10. Mhe. Hamad Masoud Hamad

Mhe. Spika, wote tunawashukuru sana na kwa jumla wengi waliochangia kwa kweli wamezunguka kwa baadhi ya mambo mawili au matatu, ambayo yote yalikuwa yanahitaji kutolewa wasi wasi juu ya madhumuni hasa makubwa ya mswada wetu huu.

Kwa hivyo, kama nilivyosema nitajaribu kwa kifupi kabisa kuchambua maswali au maoni ya mjumbe mmoja mmoja.

Kwanza nianze na Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi). Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na wajumbe wake, kama nilivyosema kazi ni nzuri sana ambayo tuliifanya kwa pamoja katika kuuchambua mswada huu na hatimaye kupata marekebisho pia yamesambazwa pamoja na mimi kuweza kuwasilisha katika hali hiyo leo hii *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ushauri alioutoa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa kiasi kikubwa umesaidia kuiendeleza au kufanya marekebisho sheria hii. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali halipendi neno kuboresha na wala sipendi kulitumia, kwa sababu ni mwalimu wetu tumheshimu, basi niseme kuifanya kuwa bora zaidi sheria hii.

Kwa hivyo, napenda kumthibitishia Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake kwamba ushauri wao walioutoa, tumeupokea na ninaamini utatusaidia sana katika kufanikisha kwenye utendaji pamoja na marekebisho ya mwisho ya mswada huu.

Anayefuata ni Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji (Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi). Vile vile napenda kumshukuru sana kwa mchango wake ambao ulikuwa ni mfupi uliojaa falsafa kama kawaida yake yeye ni mwanafalsafa. Kwa kweli ulisaidia katika ushauri na zaidi ulijikita kwenye

nyanja za kisheria na hii nathibitisha kwamba Mhe. Mjumbe amebobea katika fani ya kisheria.

Kuhusiana na hoja ya tafsiri ya kisheria kwa marekebisho yaliyofanywa, tayari yametoa tafsiri kuwa Waziri maana yake ni Waziri Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi, kama ilivyotafsiriwa kwenye mswada huu Sehemu ya Pili na wazo hilo tayari limeshafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, kuhusiana na hoja kuwa kwa nini Mahakama isipewe uwezo wa kutoa hukumu moja kwa moja na badala yake imepewa uwezo wa kumtangaza mmiliki tu. Lengo hasa ni kuipa nafasi serikali katika masuala ya ushughulikiaji wa mambo ya umma, yaani *Public Entrest* na hata kwenye Katiba ya Zanzibar kifungu 17 sheria imewekwa hukusiana na umilikaji au uchukuaji huo kutoa fidia inayolingana.

Vile vile kuhusiana na hoja ya kuwepo kwa ukiritimba katika utekelezaji wa amri dhidi ya serikali, kwa kweli mswada huu unamuwezesha waziri kuweka kanuni, ambazo pamoja na mambo mengine kutakuwa na muda wa kikomo cha utekelezaji wa amri hizo kwa kuzingatia mazingira yaliyopo.

Mhe. Mjumbe alishauri kwamba kwa nini tusiingize moja kwa moja kwenye sheria. Kwa sababu sisi kwa mtazamo wetu kwanza kuirekebisha sheria *process* yake ni ndefu, lakini unapompa uwezo waziri kutunga kanuni basi wakati wa kutekeleza kazi zake anaona kuna haja na tatizo lipo, ni vyema kumpa fursa ya kutunga kanuni na kuweza kurekebisha na mambo kwenda vizuri.

Nadhani si vizuri kusubiri tena kuja kuleta utaratibu wote wa kuibadilisha sheria. Lakini kama bado kunahitajika mabadiliko au marekebisho ya sheria basi tutafuata utaratibu. Mhe. Spika, vizuri kumpa waziri uwezo wa kutunga kanuni ni mzuri na utatusaidia sana na kama tulivyoshauri kwenye mswada wetu.

Pia kuhusiana na swali lake linalosema kwa nini sheria hii inakwenda *retrospective application* kama ni ukiukwaji wa Katiba. Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba sheria hii imezingatia Katiba, kimsingi Katiba ya Zanzibar haikatazi utumiaji wa *retrospective application* kwa mashauri ya jinai. Isipokuwa kifungu cha 12 (6) (c) cha Katiba ya Zanzibar Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 12(6)(c) cha Katiba ya Zanzibar kinasema hivi:-

> "ni marufuku kwa mtu kuadhibiwa kwa sababu ya kitengo chochote, ambacho alipokitenda hakikuwa ni kosa chini ya sheria, na pia itakuwa ni marufuku kwa adhabu kutolewa ambayo ni kubwa kuliko adhabu iliyokuwepo wakati kosa linalohusika lilipotendwa".

Mhe. Spika, nafikiri na sisi tumejaribu kwenda kwenye Katiba yenyewe na kuona hasa tunakusudia nini wakati tunapozungumzia *retrospective application*. Kwa hivyo, Katiba haikatazi na imeruhusu kabisa na sisi ndio maana tumekinukuu kifungu hiki.

Kwa kweli michango kwa ujumla iliyotolewa na Wajumbe wote ilikuwa na lengo la kuimarisha mswada huu, kama nilivyosema kwamba tunaipokea michango hiyo na tutaifanyiakazi. Waheshimiwa Wajumbe wengi walisema tuufanye uwe mzuri zaidi, basi tufanye marekebisho kwa yale mambo ambayo wameshauri. Kwa hivyo, tumesikia na kila tunapohisi itasaidia basi tutarekebisha.

Nikiendelea na Mhe. Rashid Seif Suleiman kuhusiana na mchango wake katika kifungu cha 11(4). Kwa kweli kifungu hiki labda itakuwa vyema nikisome kwa faida ya wajumbe. Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 11(4) kinachosema hivi:

> "Mahakama katika shauri lolote haitotoa amri ya kuzuia au kutoa amri yoyote dhidi ya afisi wa serikali iwapo kutolewa kwa amri hiyo kutaleta athari kwa serikali, ambapo isingepaswa kutolewa katika madai dhidi ya serikali".

Mhe. Spika, nadhani wajumbe wa kamati wanakumbuka kwamba tulikuwa na majadiliano marefu kuhusu kipengele hiki kuwa kiwepo au kiondolewe. Sasa kwa kufuatia ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe na sisi ndani ya wizara, Mhe. Spika tumekubali shauri kwamba kifungu hiki kiondolewe kwa kuzingatia suala zima la utawala bora, uwazi pamoja na uadilifu. Kwa hivyo, wazo lake Mhe. Mjumbe pamoja na wajumbe wengine tumesikia, tumezingatia na kutekeleza *(Makofi)*.

Azma kubwa ni kuipa Mahakama uwezo wa kutumia busara zake na kuhofia kwamba kifungu hicho kisijekutumika vibaya. Kwa maana hiyo, zaidi tunataka Mahakama ipewe upeo wake wa kutumia busara. Kwa hivyo, tumehisi bora tukiondoe hiki kifungu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala la Mhe. Haji Faki Shaali ambapo alitaka kujua idadi ya Mahakimu wenye *Extended Jurisdiction*. Hivi sasa tunao Mahakimu 7 ambao wenye uwezo wa ziada wa kusikiliza mashauri ya Mahakama Kuu.

Vile vile Mhe. Mjumbe alitaka kujua kwa undani suala zima la *two side of the coin*, kwamba tusiangalie upande wa serikali tu. Kwa kweli tunamhakikishia kwamba sheria hii imejitahidi kuangalia *other side of the coin* kuhusu mwananchi. Lengo letu ni kumlinda mwananchi na wala sio kumkandamiza na kama nilivyosema kwamba fursa zote atapewa kwa ajili ya kutetea haki zake.

Kuhusiana na wazo lake la kuishauri serikali kuajiri watu kwa kuzingatia uwezo na sifa zinazohitajika. Kwa kweli wazo lake ni zuri na hivi sasa serikali inaajiri kwa kuzingatia mahitaji na uwezo wa kiutendaji wa mfanyakazi.

Nikiendelea na Mhe. Mjumbe kuhusu hoja yake ya kwamba sheria inaonekana kuelemea upande mmoja wa shilingi. Kwa kweli kama nilivyosema kuwa sheria hii inakuhusia kuweka utaratibu mzuri wa kumuwezesha mwananchi kuishtaki serikali kama vile watu binafsi wanavyoshtakiana na wala si kama tunaiondoa ile fursa aa! Isipokuwa tunafanya utaratibu uwe mzuri zaidi sasa wa yeye kupata haki zake.

Waheshimiwa wajumbe wengi walizungumza kwamba labda kuna madai ya serikali, yaani mtu amedai siku nyingi na kuhangaishwa tu na wala huo si utawala bora. Kutokana na hali hiyo, huyo mwenyekuhangaisha hafanyi utawala bora na wala hawajibiki.

Sasa sheria hii nadhani tumezungumza kwamba itamuwajibisha yeye kuwa hafanyi wajibu wake, sheria hii imezungumza kwamba mpaka deni linazidi, yaani linakuwa kubwa na fedha anatiliwa. Kwa sababu tunao utaratibu wetu wa *MTEF* au *Public Finance Management*, sasa ikiwa afisa huyu hayafanyi basi na yeye tutamuwajibisha.

Kwa hivyo, suala zima la utawala bora tutalizingatia na wala si kwa mwananchi tu hata kwa maafisa wetu wa serikali. Lengo ni kuleta ufanisi mzuri kwa ajili ya kupata mafanikio, yaani huo ndio mtazamo wetu.

Mhe. Spika, nikiendelea na Mhe. Ali Abdalla Ali, tunamshukuru sana kwa mchango wake na kama alivyosema mwenyewe kwamba alifilisiwa mawazo na mjumbe aliyemtangulia. Kwa hivyo, nadhani mengi aliyotaka kuyajua nimeshayazungumza na nitaendelea kuyazungumza.

Lakini yeye alitakakujua maana ya neno mdaawa. Mhe. Spika, maana ya neno mdaawa ni mdai na mdaiwa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria Mama ya Mwenendo wa Madai Zanzibar.

Kuhusiana na swali lake la sheria hii kuzuia mdai kujikatizia kodi kwa ajili ya kulipiza deni. Mhe. Spika, kisheria kutokulipa kodi ni kosa la jinai, hivyo yakitokezea kama hayo basi serikali itakaa pamoja na mdai na kuangalia utaratibu wa kumlipa, lakini sio kama yeye anadaiwa kodi basi ajikatizie tu kwa kuwa anaidai serikali aa! Nadhani ni vyema kukaa pamoja na kuweza kuangalia utaratibu mzuri wa kutatua suala hilo, lakini kodi yetu ni lazima alipe vyenginevyo atakuwa anafanya kosa la jinai *(Makofi)*.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui naye tunamshukuru sana kwa mchango wake na pia alitoa tahadhari kwamba sheria hii itakuwa ni kikwazo kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba sheria hii si kikwazo kwa wafanyabiashara wa ndani na nje. Isipokuwa serikali imeweka sheria mbali mbali kama vile Sheria za Manunuzi na Ufutwaji wa Sheria za Mali za Serikali chini ya mwaka 2005 na kadhalika. Sheria hizo zinahusiana na masuala ya biashara na wawekezaji wa ndani na nje.

Zanzibar kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa *Multilateral Investment Guarantee Agency (MIGA)*. Taasisi hii ipo chini ya *World Bank*, ambayo kazi yake kubwa ni kusaidia wawekezaji binafsi wa nje na ndani ya nchi. Aidha sheria hii itatumika pale ambapo itatokea migogoro baina ya mtu binafsi na serikali, vyenginevyo sheria nyenginezo zitaendelea kutumika. Nadhani Mhe. Mjumbe anaifahamu taasisi hii na kama mfanyabiashara, basi naamini inatulinda sote.

Mhe. Juma Duni Haji naye tunamshukuru sana kwa mchango wake, zaidi alikuwa na hoja kubwa ya kuonewa mtu wa chini. Kwa kweli hilo si lengo letu kwa sheria hii, isipokuwa tunaweka utaratibu wa kumsaidia mtu wa chini, labda zaidi ni hilo suala zima la utalawa bora ambalo wamelizungumza Waheshimiwa Wajumbe. Kwa sababu utawala bora si kwa yeye mtu wa chini lakini hata sisi serikali tunawajibika kuufanya huo utawala bora.

Vile vile Mhe. Mjumbe napenda kumjuilisha kwamba sheria hii haijakiuka kwenye masuala ya mikataba, kwani yeye alisema kwamba sheria hii imekiuuka Katiba. Kwa hivyo, nataka kusema kuwa sheria hii haijakiuka katika masuala ya mikataba ambayo serikali imewekeana saini na wafanyabiashara au taasisi nyengine.

Kwa maana hiyo, kinawekwa kifungu cha usuluhishi ndani ya mkataba, ambapo endapo patatokezea mgogoro baina ya pande mbili za mkataba, basi pande hizo zitakwenda kwa msuluhishi kwa ajili ya kupatiwa usuluhisho.

Mhe. Spika, ni vyema kufahamu tunapozungumzia *arbitration* ni sehemu ya upatanishi au usuluhishi na mikataba mingi tunayowekeana na serikali au makampuni na kifungu hiki kipo, kwamba itakapotokea matatizo basi waanze kusikilizana wenyewe kwanza kabla ya kwenda Mahakamani. Kwa hivyo, nafikiri utaratibu uliowekwa mzuri tu na kama hakuna kifungu hiki tatizo lipo.

Mhe. Zakiya Omar Juma naye tunamshukuru sana kwa kuishauri serikali isikope kwa masikini na badala yake ikope kwa matajiri. Kwa utaratibu maafisa hawaruhusiwi kuingia mikataba ya kibiashara baina ya serikali na watu binafsi, endapo fedha za malipo ya bidhaa au huduma zitakuwa hazijaingizwa kwenye bajeti ya idara au taasisi husika.

Kwa kweli haya tumekuwa tukipata matatizo kwamba ah! Mtu anasema kama vile wanafunzi au wagonjwa watakaa na njaa hospitali au dakhalia, yaani hazijaingizwa fedha basi nakwenda kukopa na baadaye kulipa. Lakini wakati zinapoingizwa fedha halipi, kwa hiyo deni lipo na kuendelea kila siku. Sasa huo si uwajibikaji mzuri na wala sio utawala bora.

Kutokana na hali hiyo, tutamuwajibisha huyo afisi atakayeyafanya hayo na wala hatutaki tufikie huko kwamba aiweke serikali pabaya, fedha anatiliwa baada ya kutumia ipasavyo yeye anafanya anavyotaka na deni linaongezeka kila siku na wala si lengo letu hilo.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala la kwamba sheria hii inaingilia uhuru wa Mahakama. Kwa kweli hili tayari tumeshalizungumza kwamba kiujumla sheria hii haiingiliani kabisa na mamlaka ya Mahakama, isipokuwa inaweka utaratibu wa jinsi gani mtu binafsi au taasisi inaweza kuifungua kesi ya madai dhidi ya serikali.

Nadhani kama nilivyosema utaratibu huo ndio utakaotusaidia sana sasa kuwapunguzia shida hao wanaoidai serikali kuliko utaratibu uliopo hivi sasa. Kwa sababu tumeona mapungufu pamoja na matatizo yaliopo, ile hali ya kuuzwa kwa mali ya serikali ni jambo la mwisho kabisa kutokezea. Mhe. Spika, wajumbe wengi kwenye kamati walizungumza mtu mwenye kudai, basi atadai mpaka lini na wala hatumlipi.

Mhe. Spika, nikiendelea na hoja za Waheshimiwa Wajumbe sasa niende kwa Mhe. Mohammed Ali Salim kuhusu kesi ndani ya kesi. Kwa kweli utaratibu uliopo ni kwamba endapo kesi zinafanana na *course of action* pia zinafanana,

basi kesi moja inafutwa na na endapo *course of action* zinatofautiana basi kesi zote mbili zitasikilizwa.

Mhe. Mjumbe tunamshukuru sana kwa falsafa nyingi alizotupa, methali pamoja na mafumbo. Lakini naamini alikuwa akitoa yake katika kwa lengo la kuifanya sheria hii iwe bora zaidi na ametufahamu vizuri lengo letu.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya Mwanasheria Mkuu kupewa mamlaka ya kulipa madeni ya serikali. Kiutaratibu na kisheria Mwanasheria Mkuu ndiye mwenye mamlaka ya kusikiliza kesi kwa niaba ya serikali, hivyo jukumu la malipo amepewa mlipaji mkuu wa serikali, yaani Katibu Mkuu kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Zanzibar mwaka 2005.

Vile vile Mhe. Hamad Masoud Hamad naye namshukuru kwa *wisdom*, falsafa nyingi pamoja na hadithi nzuri. Kwa kweli nakubaliana naye na yeye pia mwisho amekubaliana na sisi kwamba sheria ni nzuri na inahitaji marekebisho madogo madogo. Kwa hivyo, marekebisho tumeyakubali na tutayafanya au tunaendelea kuyafanya.

Mwanasheria Mkuu haimaanishi kuwa yeye ndiye atakayebeba adhabu kwa afisa wa serikali aa! Kwa sababu tumeshazungumza kwamba afisa wa serikali mwenye dhamana kwa sehemu ile atawajibika yeye, ambaye amezembea. Kwa maana hiyo, afisa wa serikali atachukuliwa hatua kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 6 (7) (a) imeelezwa wazi wazi, kwamba akizembea basi yeye ndiye atakayechukuliwa hatua.

Mhe. Spika, naomba nifanye marekebisho kidogo kwamba Katiba haikatazi kutumika *retrospective* nadhani nimeshalizungumza hili kwa mashauri ya madai. Isipokuwa inakataza kutumia *retrospective* kwa kesi za jinai na hapa naomba mnifahamu vizuri kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 12(6) (c) cha Katiba ya Zanzibar.

Kwa kweli wengi Waheshimiwa Wajumbe na kama tulivyoiona michango ilikuwa zaidi ya kuiendeleza sheria yetu. Kwa hiyo, nawashukuru wote waliochangia na ninaamini wametufahamu pamoja na marekebisho haya, basi naomba tuipitishe, ili iweze kufanyakazi ipasavyo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu pamoja na marekebisho mbali mbali yaliyotajwa wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai za Serikali 2010

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima, ili kuweza kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai za Serikali 2010

Sehemu ya Kwanza
Utangulizi

Kifungu cha 1 Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu cha 2

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nimeona kitu kwenye marekebisho ya kamati kuhusu tafsiri ya Rais, naomba muiangalie na baadaye tuona kama tunaweza kufanya marekebisho mengine au vipi. Kwa hiyo, tafsiri ya Rais imeandikwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sijui kama ni sawa au vipi, sasa tunafanya marekebisho na hapo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, tunafanya marekebisho na sehemu hiyo.

Kifungu cha 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kifungu hiki tunachanganya na yale marekebisho tuliyofanya hivi sasa.

Sehemu ya Pili
Sheria ya Msingi

Kifungu cha 3	Serikali kuwajibika kama mtu binafsi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 4	Matumizi ya sheria kuhusiana na fidia na michango.
Kifungu cha 5	Kubakisha kwa yaliyofanywa chini ya uwezo wa sheria.

Sehemu ya Tatu
Mamlaka na Utaratibu

Kifungu cha 6	Madai dhidi ya Serikali na kadhalika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 7	Masharti kuhusiana na Idara Maalum pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 8	Madai ya kutaka kujua mmiliki.
Kifungu cha 9	Wadaawa katika madai.
Kifungu cha 10	Kuhamisha mashauri pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 11	

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Wakati nilipokuwa nikichangia mswada huu nilieleza kiliochangu au chetu kwa mara ya pili kuhusu kifungu cha 11(3), ambacho kinainyima uwezo Mahakama kumrejeshea mwananchi ardhi lakini badala yake kinatangaza tu kwamba mdai anastahiki ardhi lakini haitoi amri kwamba nipewe ardhi yangu. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, mimi bado linanipa mashaka. Nina wenzangu wengi waliochangia bahati nzuri, lakini kwa bahati mbaya sana Mhe. Waziri hili hakulitolea ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, nakiri kwamba kweli labda hili sikuligusia, lakini nafikiri tulilizungumza sana kwenye semina jana kwamba unapodai ardhi ambayo imechukuliwa na serikali, sasa ardhi ile serikali imeitumia kwa maslahi ya umma.

Mfano mzuri sana Kijito Upele pale, pale lilitokea tatizo kama hilo kuwa pamejengwa skuli kwenye ardhi ya mtu, yule mtu akaja akadai, sasa akaambiwa bwana wee! sisi kuvunja skuli haiwezekani kwa maslahi ya kizazi kilichopo na vizazi vijavyo, sasa tutakulipa ardhi. Basi kakubali kalipwa ardhi nyengine. Sasa hivyo ndivyo tunavyokusudia.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mheshimiwa sawa, lakini mimi nathamini zaidi maandishi kuliko maneno kwa sababu hapa katika maandishi labda niisome inavyosomeka inasema hivi, "katika madai yoyote dhidi ya serikali kwa ajili ya kurejesha ardhi au mali nyengineo, Mahkama haitatoa amri ya kurejeshwa ardhi au kurejeshwa mali. Lakini badala yake inaweza kutoa amri ya kutangaza kwamba mdai anastahiki ardhi, au mali au kushikilia mali".

Sasa Mahkama ikishatangaza kwamba mali hii ni ya Haji Faki Shaali nani atakayenipa hiyo mali yangu, au kutakuwa na utaratibu upi? Kwa sababu haya mambo yananing'inia ning'inia hayaeleweki. Sasa ile Mahkama ishatangaza pale kwamba mali hii mwenyewe Haji Faki, sasa nani mwenye dhamana ya kufuatilia na kuona napata ile haki yangu, sasa hili suala linaning'inia.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mimi namshukuru Mhe. Haji Faki kwamba ile *concept* kaikubali. Sasa kama inaning'inia hilo ni suala la uandishi tu, kwa hivyo nakiri tutakwenda kurekebisha ili iweze kuonesha hasa kuwa huyu mtu alipwe ardhi isining'inie tena. Tunakubali tutakwenda kurekebisha.

Mhe. Haji Faki Shaali: Ninakubali tuendelee.

Kifungu cha 11	Namna ya shufaa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 12	Gharama katika madai ambayo serikali ni mdaiwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 13	Rufaa na kucheleweshaji utekelezaji hukumu pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nne
Hukumu na Utekelezaji

Kifungu cha 14	Riba

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Bi. Zakiya ni kifungu gani vile cha 15, hebu twende kifungu cha 15.

Mheshimiwa samahani kabla ya Mhe. Zakiya. Kifungu cha 14 tulisema kinafutwa ndio. Sawa kwa hivyo pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 15 Utekelezaji wa amri dhidi ya serikali

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nilikuwa na wasi wasi mkubwa kuhusu kipengele hiki basi nilikuwa napenda nijue marekebisho

yake yalivyo, maana nikiambia tu pamoja na marekebisho yake sina uhakika yatakuwaje nilitaka angalau nijiridhishe.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, tunasema kwamba kwa kesi za jinai basi hizi hazina *retrospective*, hapa kesi zetu za madai ndio tunazozungumzia ndizo zitakazokuwa na *retrospective effects*.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, naona kama sijampata vizuri na zaidi nimeelemea katika hiki kifungu cha 15(4) na nitapenda nikisome kama kilivyo. "Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki hakuna utekelezaji wa hukumu, mauzo, ukamataji wa mali inayohamishika na isiyohamishika ya serikali au hatua ya aina hiyo ambayo itatolewa na Mahakama yoyote kwa ajili ya kuilazimisha serikali kulipa fedha zozote au gharama zilizotajwa katika kifungu na hakuna mtu atakayewajibika binafsi kwa amri yoyote ya serikali kulipa au idara yoyote ya serikali au afisa wa serikali kwa fedha au gharama hizo".

Kwa hivyo, hapa nahisi kwamba kama nilivyosema wakati nilipokuwa nikichangia niliona kwamba haki inakwenda sivyo na zaidi inaonekana Mahakama kama imenyooshewa kidole. Mimi nakubali marekebisho lakini angalau nijiridhishe yakoje, labda angeyaweka vizuri kwa faida na wanaotusikiliza.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, namshauri Mhe. Mwakilishi kwamba mimi naona iko *straight forward* sijui utata anaona uko wapi na hili ni moja ya madhumuni ya mswada huu. Kwa hivyo, sijui yeye angeshauri vipi mimi naona iko sawa labda angelituelezea tatizo analiona liko wapi. Kwa sababu nimezungumza kabisa mfano kwenye ukurasa wa 39 na hakuna mtu atakayewajibika binafsi kwa amri yoyote ya serikali kulipa au idara yoyote ya serikali au afisa wa serikali kwa fedha au gharama hizo. Naona iko wazi kabisa hebu tusaidie kidogo.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua hata kikiandikwa Kiswahili lakini katika fani ya kisheria inaweza ikakuzonga kwa maneno hapo hapo ukaona umeelewa kumbe amekufunga kamba. Kwa nilivyofahamu mimi ni kwamba hapa Mahakama kiasi fulani imefungwa kusema kitu chochote na pengine kuzuia haki kutendeka ndio wasi wasi wangu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, nasema isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki hakuna utekelezaji isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki kwamba hakuna utekelezaji wa hukumu, mauzo, ukamataji wa mali inayohamishika na isiyohamishika ya serikali au hatua ya aina hiyo ambayo itatolewa na Mahakama yoyote kwa ajili ya kuilazimisha serikali kutupa fedha zozote au gharama zinazotajwa katika kifungu hiki, na hakuna mtu atakayewajibika binafsi kwa amri yoyote ya serikali kulipa au idara yoyote ya serikali au afisa wa serikali kwa fedha au gharama hizo.

Kama nilivyosema labda twende pamoja kifungu hicho cha 15(1), (2), (3) na (4) hasa angalia kwenye kifungu cha (2) nafikiri imezungumzwa wazi wazi kinasema, "iwapo amri inataka malipo ya fedha kwa njia ya hasara au shufaa nyenginezo au gharama za hati itataja kiwango kinachopaswa kulipwa na Katibu Mkuu anayehusika na fedha au Afisa Mhasibu inavyoweza kuwa kwa sharti zilizotajwa humu atamlipa mtu anayestahiki au kwa wakili wake kiasi hicho kilichowekezwa katika hati kumstahikia yeye pamoja na riba kama ipo anastahiki sheria". Ndio nasema bora tukisome kifungu kizima ndio utaupata ule mtiririko mzima hatukusudii kwamba tutahalifu amri za Mahakama.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sitaki niwe mkaidi lakini hiki kifungu cha 2 nakubaliana nacho lakini cha 4 nahisi kama kinapingana na kifungu cha 2 na kwa fani ya mahesabu inasema *plus minus* ni *minus*. Sasa sijui hapa ikoje nahisi bado haijanikalia sawa Mhe. Mwenyekiti nataka nikipitisha nimenyanyua mkono niwe nimeridhika.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba tupate ushauri wa Mhe. Mwakilishi yeye anataka tufanye vipi, tunataka tupate mawazo yake tu.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mimi si mwanasheria inakuwa kidogo matatizo lakini naona kama tungelikitoa hiki kifungu cha 4 ili tukaondosha utata. Kwa sababu ikiwa kifungu cha 2 kinakubaliana na hiki kama alivyoeleza Mhe. Waziri basi kwa kuondosha wasi wasi nilionao hiki kifungu cha 4 kingeondoka ikawa hiki cha 2 kinaki-*support* hiki cha 4.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyoshauri Mhe. Mwakilishi mimi namwambia asijaribu kusoma hiki kifungu cha 4 asome vifungu vyote hivi vinakwenda kwa mtiririko. Kwa hivyo, mimi

nisingeshauri tukifute lakini tutakwenda kukizingatia zaidi na tutakitizama vizuri, lakini ukisema tukitoe tutaharibu mantiki ya hivi vyengine. Mimi nahisi labda tunakubali kuchukua *challenge* tutafakari na wanasheria pamoja tutizame maana zaidi ya hiki kifungu. Kwa sababu kama nilivyosema hili ni moja ya madhumuni hasa ya mswada huu sasa kukiondoa tutapoteza mwelekeo mzima wa mswada huu.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwa maelezo aliyomalizia Mhe. Waziri tungeelezea lakini ningependa na mimi nijue kitakachoendelea.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kwanza katika dibaji yangu nilinukuu misingi mitatu ya utawala wa sheria ambayo nimesoma kutoka kwa *Professor* mmoja wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mimi sikuchukua yote minane kwani yeye ametaja misingi minane, mimi nimechukua misingi mitatu. Msingi mmoja akasema sasa hivi sheria inakatazwa ku-*retrospective legislation* ndio nilianza mwanzo kwamba hii sheria haikuzingatia misingi ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, ukija katika hiki kifungu cha 15 (5) naomba nikisome. Kifungu hiki kitatumika kuhusiana na mashauri, hukumu au amri zilizopo ambazo zimetolewa kabla kuanza kutumika kwa sheria hii lakini bado hazijatekelezwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri alipojibu nafikiri alikuwa anamjibu Mhe. Juma Duni Haji akasema kwamba Katiba inakataza *retrospective* kwa *criminal offence* lakini Katiba hajaanishwa hivyo labda nikisome kifungu cha 12(6c) cha Katiba. Kinasema ni marufuku kwa mtu kuadhibiwa kwa sababu ya kitendo chochote ambacho alipokitenda hakikuwa ni kosa chini ya sheria. Lakini sasa tunapozungumza adhabu ni *criminal* tu au nini. Kwa sababu mimi ninavyofikiria hata katika madai mtu unapompa *penalty* naona vile vile ni adhabu.

Hili neno adhabu linavyokusudiwa katika Katiba labda wanasheria watusaidie zaidi, hii Katiba inaposema ni marufuku kwa mtu kuadhibiwa kwa sababu ya kitendo chochote ambacho alipokitenda hakikuwa ni kosa. Lakini hapa Katiba haijaanisha kwamba ni kosa la jinai. Mhe. Spika, mimi ninavyofahamu hata mtu unapomnyima haki zake kati kati ya madai au unapomtia adhabu, kwani adhabu sio gerezani tu hata katika mambo ya jinai adhabu zipo. Hapa naomba tungepata ufafanuzi lakini mimi ninavyofahamu nakubaliana na Mhe. Juma Duni kwamba Katiba inakataza *retrospective legislation in general* lakini haijaanisha kwamba kwa *criminal offence* tu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimefurahi sana kwamba Mhe. Haji Faki Shaali amekubaliana na mimi hasa alipokwenda kwenye Katiba. Lakini nataka kusema kwamba adhabu ni *criminal* sio madai. Nafikiri umenifahamu Mhe. Haji lakini haya ni madai kwa hiyo kama ni madai Katiba inaruhusu, lakini kwa *criminal* hairuhusu. Hivyo ndivyo Katiba inavyoeleza.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, uzoefu wangu katika Baraza huwa mara nyingi naona hata katika mambo yasiyokuwa ya jinai tunawekea adhabu. Miswada mingi ya sheria tunayoipitisha hapa inakuwa ina adhabu hata kama haihusiani na mambo ya kijinai. Hili neno adhabu kama linahusishwa na *criminal* wataalamu wapo hapa labda watusaidie lakini naona sheria nyingi tunapopitisha zinakuwepo adhabu hata kama sio masuala yanayohusiana na *criminality*.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, ninavyofikiria mimi suala la *retrospective application* hiyo ni *principle* ambayo kwa utaratibu wa uandikaji wa sheria siku hizi haikubaliki na lengo hasa *retrospective application* wanasema usimfanye mtu kuwa katika *position* ambayo sio aliyokuwa nayo wakati ule kitendo kilipofanyika. Kwa mfano, tulikuwa na kesi mimi na Saleh ya madai na kesi ile mimi nikaambiwa nimlipe Saleh shilingi milioni 50 *last interest* ya 5.5, lakini kwa sheria hii inaonesha kwamba ikiwa ile hukumu wakati ule haijatekelezwa sasa mimi nimlipe kwa mujibu wa utaratibu huu.

Kwa hivyo, *interest* hapo haitakuwa tena 5.5, itakuwa ni 8 *interest* ya leo kwa sababu ikenda Mahakamani sasa watatoa *interest* ilivyo hivi sasa, kwa hivyo itakuwa sasa ni 8. Kwa hivyo, ikiwa ulipe shilingi milioni 15 *plus interest* ya 5.5 wakati huo halafu hivi sasa unalipa shilingi milioni 15 *plus interest* ya 8.5 angalau huyu mtu umeshamuweka katika *position* ambayo siyo. Kwa hivyo, hiyo ndio maana ya *retrospective application* kwamba hairuhusiwi katika *drafting* ya sheria siku hizi. Kwa hivyo, inategemea tena mazungumzo ya hapa lakini *principle* ya *retrospective application* hai-*apply* kwa *criminal* tu, ina-*apply* kwa kitu chochote ambacho mtu kitamfanya *position* ile awe sio ile *position* aliyokuwepo. Kwa hivyo, huo ndio utaratibu Mhe. Mwenyekiti ninavyoufahamu mimi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, wengine sio wanasheria lakini tunajaribu tu. Mhe. Mwenyekiti, tukirudi kwenye mswada kwenye kifungu kile kinachozungumzia sehemu ya 4 kuhusu hukumu ya utekelezaji, kifungu cha 14 (2) kinasema kifungu hiki kitatumika

kote kuhusiana na mashauri yanayoendelea wakati sheria hii inaanza kutumika kwa madai yatakayofunguliwa baadae. Ndio pale niliposema kwamba ndio linapokuja hilo suala la *retrospective* kifungu hiki kitatumika kote kuhusiana na mashauri yanayoendelea wakati sheria hii inaanza kutumika na madai yatakayofunguliwa baadae.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kusisitiza tena kwamba sheria zetu bado hazijafutwa kwa mujibu wa Katiba yetu, Katiba hapa ndiyo inayo-*apply* na sisi tumei-*quote* inaruhusu vifungu havijafutwa kwenye Katiba yetu.

Mhe. Mwenyekiti: Labda kitu ambacho nitakisema hapa ni kuzingatia kwamba tukitaka kutumia sheria hii kwa mambo yaliyofanyika huko nyuma itiliwe maanani tu kwamba hakuna upande utakaodhulumika kwa kuchukua hatua hiyo. Nafikiria sijui sasa tunawekaje lakini mantiki ni kwamba upande wowote sio wa serikali wala sio upande wa yule anayeidai serikali, isije ikafika pahala kuna upande ukadhulumika kwa kuchukua hatua hiyo kwa kuja nyuma kwa kutumia sheria hii. Labda tungesaidia namna ya kuiweka tu lakini mantiki nadhani inatakiwa iwe hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kwa *concept* uliyotwambia nafikiri inakubalika na sisi tutaifanyia kazi, kwa sababu ya kusema hivyo itabidi tuzingatie sana kwa sababu kuna baadhi ya mikataba kwa mfano, imekosewa hapo mwanzo hiyo mikataba ina matatizo yake. Kwa hivyo, ndio itabidi kidogo twende kwa uangalifu sana lakini ulivyotuelezea nafikiri inakubalika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kwa busara za kiti chako naona sina sababu nisiseme tuendelee.

Kifungu cha 15	Utekelezaji wa amri dhidi ya serikali pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 16	Utekelezaji kwa serikali.

Sehemu ya Tano
Masharti ya Jumla

Kifungu cha 17	Kudhihirisha hati pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 18	Hati ya serikali kuegemea sheria iliyopo.
Kifungu cha 19	Kikomo cha muda wa madai.
Kifungu cha 20	

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, hii itakuwa ndio buti yangu ya mwisho lakini najua zitakuwa zinaendelea. Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia katika kifungu hiki ambacho kinazungumzia juu ya kujilipizia deni na madai ndani ya madai kwa ulipaji kodi. Nilizungumza wala sio kwa utani kwamba hii sheria inamruhusu mtu kujikatizia deni lake kama anaidai serikali, lakini nikasema je, mbona haiwi na mwananchi naye aka-*enjoy* fursa kama hii. Nafikiri hili Mhe. Waziri nalo hakulitolea ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nililitolea maamuzi pengine ni moja kwa moja au pengine nilisema sio vyema mtu ambaye anadaiwa kodi na serikali akasema naikata kodi hii nilipe deni, nikasema hilo ni kosa la jinai. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba unadaiwa kodi ya watu hujalipa ni kosa. Kwa hivyo, kwanza ulipe deni hilo halafu tena utafute mbinu ya kulipa hilo deni lako au kuna njia nyengine za kusuluhishwa. Mhe. Mwenyekiti, haiwi kwamba wewe unadaiwa kodi ya watu usilipe hivyo nafikiri sivyo.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, wacha tuendelee.

Kifungu cha 20	Kujilipizia deni na madai ndani ya madai kwa ulipaji kodi.
Kifungu cha 21	Mashauri yanayoendelea.
Kifungu cha 22	Kufutwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 23	Bakisho pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 24	Kanuni
Kifungu cha 25	Nguvu ya kushinda pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima limeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake sasa naliomba Baraza lako liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaoafiki mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai za Serikali ya 2010

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Mwenendo wa Kuweka Haki na wajibu wa Serikali katika Kesi za Madai na Utaratibu wa Mwenendo wa Madai Dhidi ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo pamoja na marekebisho yake usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaoafiki mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe shughuli zetu kwa leo naona zimekwisha kwa hivyo kufikia hapa sasa tusitishe mwenendo wa habari zetu ili tuje kesho kwa maana hiyo basi naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 25/03/2010 saa 3:00 asubuhi

(Saa 12:30 jioni Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 25/03/2010 saa 3:00 asubuhi)